Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tano – Tarehe 15 Juni, 2009**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Fedha na Uchumi, naomba kuwasilisha Mezani Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Uchumi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 33

**Athari za Milipuko ya Mabomu - Mbagala**

**MHE. KHADIJA SALUM ALI AL-QASSMY K.n.y. MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, tukio la tarehe 29 Aprili, 2009 la milipuko ya mabomu kwenye Kambi ya Jeshi la Wananchi – JWTZ, Mbagala Kizuiani, limesababisha hasara kubwa kama vile, watu kupoteza maisha, watu wengi kujeruhiwa, uharibifu mkubwa wa mali na

nyumba za wananchi, kuharibika kwa miundombinu na kadhalika. Na kwa kuwa, kuna Kamati maalum inayoshughulikia majanga yanapotokea ambayo iko chini ya Ofisi ya waziri Mkuu:-

Je, ni sababu zipi zilizofanya Kamati hiyo isifike kwa haraka kwenye eneo la tukio na kutoa msaada wa haraka uliotakiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili naomba kutoa mkono wa pole sana kwa Mheshimiwa Ania Chaurembo, kwa msiba wa Mama yake Mzazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ajali ya ya milipuko ya mabomu iliyotokea katika Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mbagala Kizuiani, tarehe 29 Aprili, 2009 ni tukio kubwa lililosababisha madhara na maafa kwa wananchi wa Mbagala.

Serikali kupitia Mkoa wa Dar-es-Salaam na Idara ya Maafa iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 1990 imeratibu Maafa hayo Kitaifa kupitia Kamati yake ya Kitaifa ya Maafa, *TANDREC*, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kuwahudumia majeruhi, waathirika na utoaji misaada.

Hivyo, Idara ya Maafa inashughulikia Uratibu wa Maafa Kitaifa na si Kamati Maalum kwa ajili ya Operesheni ya kukabiliana na maafa kama vile uokoaji, uhamishaji, kuzima moto au kugawa misaada. Kazi kubwa ya idara hii ni kuunganisha wadau mbalimbali wanaokabiliana na maafa wala siyo Mkuu wa eneo la tukio.

Mheshimiwa Spika, Kamati maalum ya tathmini iliundwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam. Kamati hiyo inajumuisha wataalamu kutoka *JWTZ*, Polisi, Chama cha Msalaba Mwekundu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Idara ya Maafa), na Wathamini majengo kutoka mikoa ya Dar-es-Salaam, Morogoro, Tanga na Pwani.

Taarifa ya tathmini ya ajali iliyotokea tarehe 29 Aprili, 2009 inaonesha kuwa jumla ya nyumba 9,049 zimeharibika; kati ya hizo nyumba zipatazo 286 zilibomoka kabisa na zilizobaki 8,763 zimeezuliwa paa, kuvunjika au kupata nyufa; Serikali inaandaa taratibu za kuwalipa fidia walioathirika. Katika tukio hilo madhara makubwa yalitokea. Aidha yapo madai mapya ya nyumba 813 kupata nyufa kutokana na mabomu yaliyotenguliwa tarehe 6 Juni, 2009. Kamati ya Tathmini imepewa muda hadi tarehe 19 Juni, 2009 iwe imeshughulikia na kubaini ukweli wa madai hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia tathmini ya awali, Serikali ilitoa kwa wahanga hao shilingi 200,000,000/= na vifaa mbalimbali kama vile mablanketi, huduma

za maji, magodoro, mikeka, sabuni, vyombo vya kupikia, mahema, maturubai, ndoo, na kadhalika. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea na jitihada za kukabiliana na maafa hayo ili kurejesha hali ya maisha ya waathirika kuwa ya kawaida. Aidha, hapa naomba nitaje pia kwamba Idara ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara ya Maafa ya Zanzibar huwa zinashirikiana bega kwa bega pale yanapotokea maafa kila inavyowezekana.

Mathalani, katika ajali ya meli *MV Fatih* iliyotokea tarehe 29 Mei, 2009 Idara ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilienda Zanzibar kuungana na Idara ya Maafa Zanzibar katika kufuatilia shughuli za kuokoa walionusurika katika ajali hiyo ambapo abiria 27 na mabaharia 13 walitoka salama na maiti 10 ziligunduliwa hadi tarehe 31 Mei, 2009. Suala hili la ajali ya *MV Fatih* linaendelea kushughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Natoa pole kwa walioguswa na ajali ya *MV Fatih.* Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

**MHE. KHADIJA SALUM ALI AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, watu wengi waliathirika afya zao na wamegundulika wamepata matatizo mengi ya masikio na macho. Je, Serikali ina mikakati gani zaidi ya kuweza kuwatibu watu hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Qassmy, Mbunge wa Viti maalum, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea katika jibu la msingi la swali hili kuwa serikali kwanza itawafidia waathirika wote wa ajali hiyo ikiwa ni pamoja na kushughulikia matibabu ya wale ambao walikuwa wameumia kwa namna moja au nyingine.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tukio hili ni *unique.* Je, serikali imejifunza nini na ina mikakati gani kuhakikisha janga kama hili halitokei tena hapa nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba tukio la maafa haya ya mbagala ni tukio la pekee na kama ilivyo maafa mengine yoyote huwa maafa hayarejei, hatuwezi tukafahamu ni ajali. Hivyo tunaweza kujifunza leo kwa kutumia uzoefu wa Mbagala, lakini pengine ajali nyingine itakayotokea haitafanana na hii ya Mbagala.

Lakini kwa ujumla naweza kusema kwamba ajali hii ya Mbagala ya mabomu, haikuwa inalenga mahala popote, haikuwa inalenga nyumba ya mtu wala haikuwa inalenga watu; ni bahati mbaya ilitokea.

Hivyo mojawapo tulilojifunza ni kwamba wananchi wasipendelee sana kujenga katika maeneo haya ambayo ni ya hatarishi.

Na. 34

**Manispaa ya Dodoma Kuongezewa Magari Imara ya Wagonjwa**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inayo magari mawili tu ya wagonjwa ambayo yaliletwa kama msaada wa wafadhili baada ya kutumika huko yalikotoka; na kwa kuwa, muundo wa magari hayo unasababisha yashindwe kuhudumia wagonjwa kutoka vituo vya Afya na Zahanati zilizopo Vijijini kutokana na ubovu wa barabara:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa gari moja la wagonjwa la aina ya *4WD* kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa Vituo vya Afya vya Hombolo na Kikombo na lingine kwa ajili ya Zahanati 30 za Manispaa ya Dodoma?

(b)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyahamisha magari ya wagonjwa yaliyopo yasiyomudu barabara za vijijini ili yapelekwe kwenye Halmashauri zenye barabara nzuri za lami ili yaletwe magari mbadala yenye *4WD?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ina magari mawili ya wagonjwa ambayo yote yametolewa na wafadhili kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Gari aina ya *Mercedes Benz* lilitolewa na *DUWASA* kwa ushirikiano na *Lions Club* kwa ajili ya kituo cha Afya Makole. Hata hivyo kwa sasa gari hilo lipo kwenye matengenezo kutokana na ubovu unaotokana na gari hilo kuwa chini na hivyo kushindwa kumudu njia za Changarawe zenye makorongo ya hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, Gari la pili ni la aina ya *Toyota Landcruiser "Hard Top"* ambalo ni maalum kwa kubeba wagonjwa yaani *Ambulance*, na limetolewa na *United Nations Joint Programme* kwa ajili ya Kituo cha Afya Hombolo. Gari hili ni jipya na linafanya kazi, hivyo ni jukumu la Halmashauri kulitunza wakati inatafakari uwekaji wa

mipango ya ununuzi wa magari mengine kwa ajili ya vituo vya afya vya Kikombo na Mkonze.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaelewa umuhimu wa kuwa na magari ya kubeba wagonjwa katika Vituo vya Kikombo, Mkonze na Makole na hata kwa kila Zahanati. Kutolewa kwa magari hayo mawili, *(Mercedes Benz* na *Toyota Landcruiser Hardtop)* ni matokeo ya ushirikiano na mipango mizuri ya pamoja kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na wafadhili. Hivyo ni vyema wananchi nao wakahamasishwa kutengeneza barabara ili magari yanayotolewa na wafadhili yaweze kuvifikia vituo vya afya na hata Zahanati vijijini na kurahisisha utoaji wa huduma za Afya kwa wananchi.

(b)Mheshimiwa Spika, kutokana na nia njema ya *DUWASA*, *Lions Club* na *UN-Joint Programme* ya kuwasaidia wananchi wa Manispaa ya Dodoma katika kuboresha huduma za afya kwa kutoa magari yaliyotajwa, ni vigumu kwa Serikali kuhamishia magari hayo katika Halmashauri nyingine kwani kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mikataba ya kutolewa magari hayo. Serikali inaishauri Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kuweka katika Mipango yake ununuzi wa magari na kutenga fedha katika bajeti yake ili kuanza kununua magari aina ya *4WD* kwa ajili ya Vituo vya Afya kwa awamu.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake kuhusu magari ya wagonjwa katika Manispaa yetu. Hata hivyo ninaomba ruksa yako niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kutokana na uchache na ubovu wa magari haya. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kununua na kuweka mtandao wa *Radio Call* katika magari haya na katika Zahanati mbalimbali ili iyawezeshe yatoe huduma ambayo ina ufanisi zaidi na huduma yenyewe iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, anachozungumza hapa kwa sababu anachoangalia hapa ni kwamba anaona tuna uchache wa magari haya na kama katika Manispaa utakuwa umeweka *Radio Call* maana yake ni kwamba unaweza ukaita gari lililoko katika kituo kingine likahamishiwa katika kituo kile ambacho mgonjwa yupo.

Kwa hiyo, kwa kweli kimantiki huwezi ukabisha kwa sababu ni la msingi sana. Sasa labda swali litakuwa ni kwamba gharama hizi tunafanyaje. Lakini mimi nadhani ni wazo zuri na ninadhani sio kwa Manispaa ya Dodoma tu hata kwa Wilaya nyingine ni wazo zuri ukiwa na *Radio Call* ili kuweza kukabiliana na hili tatizo ambalo analizungumzia Mheshimiwa Madeje.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, matatizo ya magari kwa ajili ya vituo vya afya ni maeneo mengi hapa nchini pamoja na vituo vya afya vya mkoa wa Singida na nchi nzima kwa ujumla hasa vituo vile ambavyo viko mbali na hospitali za wilaya na mkoa. Je, serikali ina mkakati gani wa haraka hasa kupitia Bajeti hii tunayoanza kuijadili kuhakikisha kila Tarafa za pembezoni kuwa na gari kwenye kituo cha afya ambalo litakuwa *standby* kukimbiza akina mama wanaoshindwa kujifungua na majeruhi wanaopatikana mara kwa mara kuwakimbiza katika hospitali ya wilaya ama mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani kwanza jambo ambalo linazungumzwa hapa ni jambo zito, kubwa. Tunaposikia habari ya vifo vya akina mama katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu kinachosababisha kimoja ni haya matatizo kwamba hatuna magari ya kuwawahisha na kuwapeleka katika maeneo ya huduma. Mheshimiwa Diana Chilolo anazungumza uwezekano wa kuwa na gari moja kwa kila Tarafa. Ni wazo zuri, mimi nataka tu niwape picha kamili ya mambo yalivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 kwasababu ya gaharama kubwa sana za kuendesha shughuli zetu hizi tulishindwa kabisa kupanga *Ambulance* katika vituo vyetu kwa maana ya Zahanati na Vituo vya Afya. Safari hii hatukuwa na mpango uliowekwa moja kwa moja kwenye Wizara, lakini Manispaa pamoja na Halmashauri mbalimbali zimetenga hela kwa kiasi cha bilioni 5.6 kwa ajili ya kununulia *Ambulance* katika maeneo mbalimbali.

Wazo analolizungumzia Mheshimiwa Chilolo ni zuri ila tatizo litakuwa ni namna ya kupata hizo pesa kwa sababu sasa tunapozungumza pos*ition* ya Serikali katika Bajeti hii ambayo imesomwa hapa imeshapitwa tayari. Lakini nadhani kuna haja ya kuliangalia jambo hili kwa undani zaidi ili kuona ni kwa namna gani tunaweza tukasaidia katika tatizo hili na kuhakikisha kwamba tunaweka walao *Ambulance* moja katika kila Tarafa kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

Na. 35

### Mpango wa Kuendeleza Mialo Kando Kando ya Ziwa Victoria

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya imeandaa mpango kabambe wa kuendeleza mialo kando kando ya Ziwa Victoria:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kujenga Sota kuwa Mwalo wa Kimataifa?

(b) Je, mradi huo utaanza lini, utakamilishwa lini na utagharimu fedha kiasi gani?

(c) Je, ni miundombinu gani itajengwa katika mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu**:-**

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mbunge wa Rorya, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikiali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya kupitia Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Ziwa Victoria *(Implementation of Fisheries Management Plan – IFMP/LVFO)* unaotekelezwa katika Ziwa Victoria utafadhili uboreshaji wa mialo sita na kujenga mingine mipya sita kwa lengo la kukidhi viwango vya Kimataifa vya usalama na ubora wa samaki. Mialo mipya itakayojengwa ni pamoja na mwalo wa Sato (Rorya). Mialo mingine itakayojengwa ni Bwai (Musoma Vijijini), Kigangama (Magu), Kahunda (Sengerema), Kikumbaitare (Chato) na Marehe (Misenyi). Aidha, mialo sita itakayoboreshwa ni Kisorya (Bunda)Izunge (Ukerewe), Igombe (Mwanza), Igabiro (Bukoba), Katembe-Magarini (Muleba) na Nkome Mchangani (Geita).

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa katika kujenga mwalo wa Sota pamoja na mingine mitano ni kama ifuatavyo:-

(i) Msimamizi Mshauri *(Consultant)* alishaandaa michoro, viwango *(specification)* na makisio ya gharama za ujenzi kwa ajili ya kutangaza zabuni.

(ii)Zabuni ya ujenzi wa mialo husika ilitangazwa tarehe 9 Machi, 2009 na ilifungwa tarehe 11 Mei, 2009.

(iii)Tathmini ya zabuni ilifanyika tarehe 12 – 15 Mei, 2009. Ripoti ya tathmini ya zabuni hizo imetumwa na Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria *(LVFO)* katika Jumuiya ya Ulaya Kampala kwa ajili ya kuidhinioshwa kwa wakandarasi waliochaguliwa.

(b)Mheshimiwa Spika, kazi ya ukarabati wa nialo sita na ujenzi wa mingine mipya sita iliyoainishwa inatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Julai, 2009. Ujenzi huo utachukua mwaka mmoja na inakadiriwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2010.

Kiasi cha fedha kitakachotumika katika ujenzi wa mialo sita mipya na kuboresha mingine sita ni *Euro* 1,500,000 ambapo ujenzi wa mwalo wa Sota pekee utagharimu takriban *Euro* 249,403.87.

(c)Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa mialo, miundombinu itakayojengwa ni pamoja na jengo la kupokelea na kunadishia samaki, tishari, *slab* ya zege zito la kuunganisha tishari na nchi kavu, uzio kuzunguka eneo la mwalo, ofisi, karakana na vyoo.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena. Nataka niipongeze Serikali, hususan viongozi wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya, nafikiri sasa Wizara imepata viongozi. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo nina swali la nyongeza la kwanza. Kwa kuwa wavuvi katika maeneo ya kandokando ya ziwa wana matatizo mengi ya kupata nyavu. Je, Serikali ina mpango gani mahususi kuwahamasisha wawekezaji kwa kujenga viwanda vya nyavu ili wavuvi waweze kupata nyavu hizo kwa bei nafuu na kwa haraka, hususan katika wilaya ya Rorya, Muleba, Biharamulo, Geita, Ukerewe na kadhalika.?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubali kufanya ziara tena katika wilaya ya Rorya kukagua mialo 31 ambayo bado haijaendelezwa, ili apokee shukrani za wananchi na waweze kumwandalia *Kichuri? (Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri; itategemea lakini kama Madiwani wa Rorya, wataacha kuchapana makonde. *(Kicheko).*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Profesa Sarungi, kwa kupongeza Wizara yangu. Nasema kwamba tutaendeleza hiyo kasi kwa kutumia kasi mpya na nguvu mpya kama ilivyo katika Serikali ya nne.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa kuhusu viwanda nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wavuvi wanapata zana zote ambazo zinatakiwa. Na Serikali imeshaweka sera ambayo kwa kweli inahakikisha kuwa nyavu na zana nyingine za uvuvi zinapatikana. Kwanza kabisa kilichofanyika ni kwamba kwa kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki, tumejaribu kuhakikisha kwamba zana za uvuvi ambazo ni boti, nyavu na injini za maboti hayo tumepunguza bei, tumepunguza ushuru mpaka 5%. Kwa hiyo, hii inavutia wawekezaji kuwekeza katika hii sekta ili wananchi waweze kupata hivyo vyombo kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda vya zana, vipo lakini tutaendelea kuhamasisha. Ningependa kuwaambia wananchi kwamba tunavyo viwanda viwili Tanzania ambavyo hutengeneza nyavu. Na kimojawapo ya hiki ni *FANACA* kilichopo

Mwanza na hiki hutengeneza nyavu za aina mbalimbali kwa ajili ya kuvulia samaki mbalimbali katika ziwa Viktoria. Na ninataka kuwahakikishia wananchi kwamba nyavu hizo za aina mbalimbali zinapatikana kwa mfano kiwanda hiki cha *FANACA* kinatengeneza nyavu zenye ukubwa wa macho ya milimita 10 kwa ajili ya kuvulia dagaa.

Kwa hiyo, hizo nyavu za dagaa zipo. Nyavu zenye ukubwa wa macho ya nchi tatu kwa ajili kuvulia samaki katika mabwawa mwalo na mito. Tatu wanazo nyavu zenye ukubwa wa macho ya nchi tano kwa ajili ya kuvulia samaki aina ya sato, tilapia. Pia wanazo nyavu zenye ukubwa wa nchi sita hadi nane kwa ajili ya kuvulia samaki wa sangara.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukija pwani kuna kiwanda kinaitwa *Imala Limited* na kiwanda hiki kinatengeneza nyavu kwa ajili ya kuvulia samaki baharini na maji mengine kama ifuatavyo; ya kwanza kabisa wana nyavu za ukubwa wa macho ya nchi moja na nusu hadi mbili na nusu kwa ajili ya kuvulia samaki aina ya kamba baharini. Nyavu zenye ukubwa wa macho ya nchi tatu kwa ajili kuvulia samaki katika maji ya ndani, *inner waters* maji mengine isipokuwa *Lake Victoria.* Tatu wanazo nyavu za aina ya jarife za ukubwa wa macho ya kati ya nchi sita hadi 16 na nusu kwa ajili ya kuvulia samaki wakubwa wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasahivi kumejitokeza kwamba nchi haina nyavu zinazoingiliana na ningependa kutoa wito kwamba wananchi wasitoe kisingizio hicho; nyavu zipo waende katika viwanda hivi wanunue. Sisi katika Wizara tutatekeleza kazi yetu kufuatana na Sheria Na. 22 ya 2003 na kanuni zake. Kwa hiyo tutakapopata mtu anatumia nyavu ambazo hazistahili tutazikamata na kuzichoma bila huruma.

Na. 36

**Tenda ya Viwanda vya Kusindika Nyama Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imejenga machinjio ya kisasa Mkoani Dodoma na kwa kuwa, Mkoa wa Dodoma una mifugo mingi ya kutosha mahitaji ya kiwanda cha kusindika nyama na kwa kuwa katika jibu la swali Na. 76 kwenye Mkutano wa 14 Kikao cha Sita, serikali ilisema kuwa imetangaza tenda kwa watu binafsi kujenga Viwanda vya Kusindika Nyama kwa kulenga Mikoa iliyotajwa ambayo ni pamoja na Arusha, Mara, Kagera na kadhalika bila kutaja Dodoma.

Je, Serikali haioni umuhimu wa Dodoma kuwepo katika Orodha hiyo ukizingatia kuwa kuna machinjio ya kisasa Mkoani Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika jibu la swali Na. 76 kwenye mkutano wa 14 Kikao cha Sita, mwezi Februari 2009, Wizara yangu ilitoa maelezo kuwa Serikali ilikuwa imetangaza zabuni za kutafuta wawekezaji wenye nia ya kujenga viwanda vya kusindika nyama wajitokeze kwa lengo la kuingia ubia na *NARCO* katika kujenga na kuendesha machinjio/viwanda hivyo katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo tathmini iliyofanywa ilionyesha kuwa wawekezaji waliojitokeza hawakuwa na sifa. Hivyo Serikali iliamua kufuta zabuni hizo na kwa kuanzia, kwa kupitia *NARCO*, kiwanda cha nyama kinajengwa katika ranchi ya Ruvu kwa gharama ya Tsh.10.7 bilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali bado ina nia ya kutimiza azma yake ya kuhakikisha kuwa machinjio/viwanda vinajengwa katika maeneo yenye fursa katika uzalishaji wa nyama hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Manispaa ya Dodoma iko machinjio ya kisasa inayomilikiwa na *Tanzania Meat Company Ltd.* Baada ya Serikali kubinafsisha kwa kuuza asilimia 51 kwa kampuni ya *National Investment Company Ltd. (NICOL)* na asilimia 49 zimetolewa kwa kampuni ya ranchi za taifa *(NARCO)*.

Machinjio hiyo ina uwezo wa kuchinja jumla ya ng’ombe 200 na mbuzi/kondoo 200 kwa siku, lakini hadi sasa inafanya kazi chini ya uwezo wake ambapo inachinja wastani wa ng’ombe 70 na mbuzi/kondo 10 tu kwa siku bila kujumuisha wanyama wanaochinjwa kwa ajili ya soko la nje.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha kusindika nyama ni pamoja na machinjio ya kisasa na sehemu ya kusindika nayama hivi sasa Dodoma kuna machinjio ya kisasa, *Tanzania Meat Company* kuweka mikakati mahususi ya kuimarisha shughuli za uendeshaji wa machinjio ili iweze kufikia uwezo wake wa kufanya kazi na hatimaye baadaye kupanua shughuli zake kwa kujenga sehemu ya usindikaji.

Aidha wakati tukisubiri haya yafanywe napenda nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge na wafugaji wa Dodoma kwa ujumla kutumia kiwanda hiki katika kuuza mazao yao ya mifugo ili uzalishaji wake wa ng’ombe 200 kwa siku uweze kufikiwa badala ya kuchinja ng’ombe 70 tu kwa siku.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri; nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imekubali

kwamba viwanda vya nyama vitajengwa katika maeneo yenye fursa ya uzalishaji wa nyama. Na kwa kuwa, Dodoma ina fursa ya uzalishaji wa nyama ya kutosha.

Je, serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuwahamasisha wawekezaji kujenga kiwanda cha nyama mkoani Dodoma ili kuinua uchumi wa wananchi wa Dodoma kwani wanapata tabu kusafirisha ng'ombe kupeleka Dar-es-Salaam kwa ajili ya kutafuta soko?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Tanzania ni nchi inayoshika nafasi ya tatu duniani kuwa na ng'ombe wengi. Na kwa kuwa, katika nchi yetu viwanda tulivyonavyo vya maziwa na nyama havizidi sita kitu ambacho ni aibu kwa taifa letu.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kujenga viwanda vya maziwa hapa nchini ili wananchi waache tabia ya kunywa maziwa ya *NIDO* kutoka nje na kiwanda hicho kikajengwa mkoani Dodoma ambako kuna mifugo mingi na *NARCO* ya taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema Dodoma inacho kiwanda cha machinjio ambacho kiko hapa karibu pale Kizota, kwa sasa hivi kiwanda hicho kinachinja ng'ombe 70 na kinatakiwa kuchinja 200 kwa siku na kondoo 200. Kinachotakiwa sasa hivi ni kuhamasisha hii *Tanzania Meat Company* kuweza kupanua shughuli za kile kiwanda, kwa sababu kiwanda kimoja cha nyama ukitaka kizuri kabisa na kusindika ni bilioni zaidi ya 60. Sasa kabla hatujapanua wigo katika Mkoa wa Dodoma ni vizuri tukaimarisha kile itakuwa ni makosa tukiwa na kiwanda kile bado hakijatimiza ile *capacity* yake ya *production* halafu tena tukaanza vingine. Lakini pale ambapo hali itakuwa imeruhusu na kijiji hiki kimefikia wigo ule sidhani kama Serikali itasita kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika viwanda vya nyama hapa Dodoma.

(b) Ni kweli kwamba Tanzania kwa sasa hivi viwanda vya maziwa vingi vimeadhirika na kinachofanya vizuri angalau kidogo ni kile cha *Tanga fresh,* nia yetu ni kuhakikisha kwamba tumehamasisha wananchi wawekezaji kuweza kuwekeza katika sekta ya maziwa. Na hii ndiyo maana hata juzi tumepunguza mfano Serikali imepunguza kodi katika yale matanki ambayo ni *cooling system* na vilevile katika zile *TIN* ambazo za kuweka maziwa. Nia ya Serikali sasa hivi tulivyo hivi tunahamasisha Wizara inaendelea kuhamasisha wawekezaji ili waweze kuwekeza katika sekta hii ya maziwa.

**SPIKA:** Basi nitachukua wawili mmoja ni mfugaji na mwingine sielewi kwanini labda ni mtumia nyama.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana mimi ni mfugaji pamoja na mtumia nyama, kwa kuwa bila hata kiwanda mwaka jana tumetumia nyama kiasi cha tani 218,000 ambayo kwa hesabu za haraka ni sawa sawa na ng'ombe wenye kakasi *weight* na 150 kama milioni 1.4 na kwa kuwa jumla ya ng'ombe wote walio ndani ya nchi ni milioni 2.5. Sasa namwuliza Waziri bila ya kuwa na mkakati wa kuongeza

ng'ombe hivi viwanda unavyotaka viongezwe vitatoa nyama au ng'ombe kutoka wapi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, napenda swali la nyongeza la kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo kama ifuatavyo. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Lakini ni kweli pia kwamba katika nchi yetu ina ng'ombe yaani ina ng'ombe zaidi ya milioni 18.8, ina mbuzi zaidi ya milioni 13.6, ina nguruwe zaidi milioni 1.4, ina kondoo zaidi ya milioni 3.6 ukiacha kuku ambao ni zaidi ya milioni 53 na mbwa zaidi ya milioni 4 na Iringa ikiwa inaongoza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya tatu kuwa na mifugo mingi katika Afrika na kwa sababu ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kuwa na mifugo mingi ndiyo maana kuna umuhimu wa kuwa na viwanda vingi. Hatua zinazochokuliwa na Serikali za kuwa na viwanda vingi vya nyama itasaidia kwa absolve hizi mifugo kwa ajili ya utumiaji mzuri wa wafugaji na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Tanzania tuna mifugo mingi lakini ni kweli pia kwamba ulaji wa nyama uko chini, kwa sababu kila Mtanzania kwa mwaka huu anakula karibu kilo 11 za nyama kwa mwaka ukilinganisha na tunavyotakiwa na *WHO* tunatakiwa kwamba tunatakiwa tule kilo 50 kwa kila Mtanzania kwa mwaka. Lakini hata unywaji wa maziwa nao uko chini tunakunywa lita 41 na sasa zimeongezeka zaidi kuwa angalau lita 42 kwa kila Mtanzania.

Na Wafipa kule wao wanakunywa lita nane pointi moja kwa mwaka ambapo ni kama kijiko kimoja. Kwa hiyo, hatua zinachukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba mchango mzima wa sekta ya mifugo unaimarishwa ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda vingi vya maziwa. Sasa hivi tuna viwanda karibu 32, Viwanda vya nyama na tukiwahusisha wananchi na wawekezaji tofauti katika kuhakikisha kwamba sekta hii inaimarishwa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa hakika unaijua sekta yako vizuri.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na pia niishukuru sana Wizara kwa mikakati madhubuti ya kuendeleza suala hili la usindikaji wa nyama. Mimi nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo; tunapotaka kufanya mambo ya kisasa na hasa kuendelea katika ulimwengu huu tulio nao namna ya uchinjaji wa ng'ombe ya kuwapiga *short* za umeme halafu ndiyo wakachinjwa, sio uchinjwaji wa kisasa. *(Makofi)*

Sasa na kwa sababu Tanzania inataka kuelekea katika ulimwengu ili tusindike nyama inunuliwe na wenzetu ulimwenguni kote. Mtindo huu ubadilike kwa sababu kuna wengine watakuwa hawanunui nyama ya Tanzania.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje katika kubadilisha mtindo huu wa kuchinja ng'ombe kwa kutumia umeme kwanza halafu akaja akachinjwa. Hatuoni kama tunachinja maiti?

**SPIKA:** Kwa mnyama nadhani anaitwa mzoga, sio maiti.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVIVU:** Mheshimiwa Spika, uchinjaji wa kupiga *short* ya umeme mnyama ndiyo uchijaji wa kisasa. Katika machinjio yote ya kimataifa katika dunia nzima unapotaka kumchinja mnyama na hasa kwa sababu katika Bunge hili limepitisha sheria Namba 19 ya mwaka 2008 ya kuzuia utesaji wa wanyama akiwa anachinjwa. Kwa hiyo, ni lazima apigwe *short* ya umeme kidogo azubae halafu ndipo anakuja anachinjwa vizuri kikamilifu. Kwa hiyo, uchinjwaji wa kupigwa *short* ndiyo uchinjwaji unaokubaliwa kimataifa na ndiyo huo tunaotumia katika viwanda ambavyo sasa hivi vinajengwa. Kiwanda cha *SAFI, triple S*, kiwanda cha Ruvu, kiwanda cha Dodoma na viwanda vingine vyote vya nyama ambavyo ni vya kisasa vinavyojengwa katika nchi hii. Kwa hiyo, kupigwa *short* ni muhimu katika kuhakikisha kwamba tunachinja nyama vizuri. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo, Kanuni.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Kanuni 68, Mheshimiwa Waziri alichosema si sahihi na hakujibu vizuri suala langu na analidanganya Bunge. Mheshimiwa sio ulimwenguni kote wanyama wanachinjwa kwa kupigwa *short.* Hiyo siyo kweli nenda nchi zote za Kiaarabu wanyama hawapigwi *short* na ukipiga *short* humwuzi katika nchi yoyote ya Kiarabu na dhamiria hapa sasa tunatofautisha mambo mawili ya Kidini. Ndiyo maana nikasema Tanzania tubadilike ili tuweze kuuza nyama zetu nje. Si kweli kwamba ulimwenguni kote wanyama wanapigwa *short.* Mheshimiwa Waziri asafiri aende nchi za Kiarabu au nyingine halafu akaone wanyama wanachinjwa vipi katika ustaarabu wa kuchinja wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hili sio suala ambalo la kuleta mabishano kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, alichoeleza yeye ni kwamba viwanda vyote vya kisasa vinatumia njia hiyo, yaani ng'ombe apate ganzi ndiyo achinjwe na mimi ninavyoelewa ganzi sio kifo. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, sio kwamba sasa tunachinja vibudu na hivi hapana sasa bahati mbaya tena Mheshimiwa Hafidh hakueleza huko Uarabuni wanafanyaje. Maana yake amesema wanachinja bila kupita *short.* Lakini mimi ninavyofahamu Uarabuni wananunua sana Kondoo kutoka New Zealand na mimi naelewa New Zealand wanapiga *short* pia. Sasa sijui nadhani suala hili tutakapofikia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo tunaweza kuingia kwa undani zaidi. Lakini hakuna lililoharibika hapo. (*Makofi*)

Na. 37

**Umaskini wa Watanzania**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ni nchi yenye neema nyingi kwani imejaliwa kuwa na rasilimali za kila aina, ambapo kila wilaya hapa nchini inazungukwa na rasilimali za aina moja au zaidi, kama vile madini yenye thamani, wanyamapori wa kila aina, misitu minene, maziwa makubwa, bahari, gesi asilia, makaa ya mawe, mafuta, milima mizuri, mabonde yenye rutuba, mifugo na kadhalika.

(a) Je, kwanini ndani ya miaka 48 ya Uhuru bado Watanzania walio wngi ni maskini?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu za hali halisi ya sasa ni Watanzania wangapi ni maskini kabisa, wangapi wako katika hali ya umaskini wa kati na ni wangapi wako hali ya juu?

(c) Kwa kuwa wakati wananchi wa Tanzania wakiendelea kutaabika na hali ngumu ya maisha zipo nchi jirani zinazotarajirika kutokana na rasilimali za Watanzania. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. OMAR YUSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) , (b) na (c) kwanza napenda kutoa maelezo ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa umaskini katika nchi nyingi dunia ikiwemo Tanzania umegawika katika sehemu kuu tatu (3).

(a) Umaskini wa Elimu.

(b) Umaskini wa Afya.

(c) Umaskini wa Kipato.

Kwa maelezo ya awali ya Mheshimiwa Mbunge, inaonyesha anataka kuelewa zaidi juu ya umaskini wa kipato kwa Watanzania na mimi nitajielekeza huko. Baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi ni maskini wa kipato kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Watanzania wengi ni wakulima na wanategemea jembe la mkono katika kilimo chao cha uzalishaji;

(ii) Kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo hasa mbolea;

(iii) Mabadiliko ya hali ya hewa kunaathiri uzalishaji kwani sehemu kubwa ya kilimo chetu kinategemea mvua;

(iv) Ukuaji mdogo wa sekta ya viwanda;

(v) Kukosekana kwa mitaji hasa kwa wakulima; na

(vi) Ukosefu wa ajira.

Kwa maelezo ya awali ya Mheshimiwa Mbunge, inaonyesha anataka kuelewa zaidi juu ya umaskini wa kipato kwa Watanzania na mimi nitajielekeza huko. Baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu za idadi ya watu na zile za utafiti wa hali ya matumizi ya kaya zinaonyesha hali ifuatayo:-

(i) Mnamo mwaka 1991 wakati idadi ya watu ilikuwa 24.8 milioni, asilimia 21.6 ya Watanzania walikuwa maskini kabisa, asilimia 38.7 walikuwa maskini wa kati na asilimia 39.7 walikuwa katika hali ya juu.

(ii) Mwaka 200, wakati idadi ya watu ilikuwa 31.9 milioni, asilimia 18.7 walikuwa maskini kabisa, asilimia 35.7 walikuwa maskini wa kati na asilimia 45.6 walikuwa hali ya juu.

(iii) Mwaka 2007, wakati idadi ya watu ilikuwa 38.3 milioni, asilimia 16.5 walikuwa maskini kabisa, asilimia 33.4 walikuwa maskini wa kati ya asilimia 50.1 walikuwa katika hali ya juu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina takwimu zinazoonyesha nchi jirani kutajirika kutokana na rasilimali za Watanzania. Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tusaidiane katika kutupatia taarifa ili Wizara yangu iweze kuzifanyia kazi ipasavyo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba asilimia 50.1 ya

Watanzania wana hali ya juu ya maisha hivi sasa. Na kwa kuwa katika majibu yake ameeleza kwamba umaskini Tanzania unapungua, Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali inafahamu kwamba asilimia kubwa ya Watanzania hivi sasa hawana uwezo wa kumudu mlo mmoja wa uhakika kwa siku? (Makofi)

Kwa kuwa ili nchi iweze kuendelea inahitaji vitu vinne muhimu, kwanza ni watu, pili ni ardhi, tatu siasa safi na uongozi bora na kwa kuwa Tanzania tuna ardhi kubwa sana na watu tunao wengi zaidi ya milioni 40, Serikali inaweza kukubaliana na mimi kwamba kinachokosekana Tanzania ni Siasa safi na mipango mizuri ya rasilimali za Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania wote? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza, anasema Watanzania waliowengi wanaishi kwa mlo mmoja nataka nimwambie takwimu nilizozitaja zinaonyesha kushuka kwa hiyo idadi ya Watanzania ambao wanaishi kwa mlo mmoja. Nimetoa takwimu mwaka 1991 nimeeleza asilimia 21.6 na nikatoa takwimu za mwaka 2007 nikaeleza asilimia 16.5, hizi sio takwimu za kwangu hizi ni takwimu kutokana na utafiti ambao tumeufanya sisi Watanzania.

Kwa hivyo nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wako Watanzania wengi wanaishi kwa mlo mmoja lakini huu ni mchakato. Umaskini ni mchakato unashuka siku kwa siku miaka kwa miaka lakini tutafika mahali hali ya watanzania itakuwa nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Sakaya anasema kwamba tatizo kubwa ni siasa yetu kutokuwa safi na mipango yetu kutokuwa mizuri ndiyo hali hii tumefikia hapa, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Sakaya kwamba siasa zetu ni safi, mipango yetu ni mizuri na ndiyo kwa maana hali hii inashuka ingekuwa siasa zetu ni mbaya ni chafu na mipango yetu sio misafi sio mizuri hali hii takwimu hizi zingetuonyesha vinginevyo lakini kwa sababu takwimu zinashuka mipango mizuri na siasa zetu safi. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumuuliza kama ifuatavyo; takwimu ambazo zinatumika kuonyesha upuguaji wa umaskini ni shilingi 641 kwa Dar es Salaam na shilingi 532 kwa maeneo mengine ya shamba. Hivi kweli katika hali ya kawaida mtu mwenye kupata 532 anautimiza angalau huo mlo mmoja kwa siku? napenda majibu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** (**MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Khalifa hakunieleza hizo takwimu amezitoa wapi, la pili nataka niseme tu kwamba kipato cha Mtanzania au kipato kwa kila Mtanzania mpaka capital income inatuonyesha ni zaidi ya shilingi 500,000 kwa mwaka hiyo hali ya uchumi anayoizungumza Mheshimiwa Khalifa kwa capital income ya laki tano kwa mwaka ukiigawa kwa siku 366 unapata zaidi ya shilingi elfu moja, ndiyoo! hiyo ndiyo hali halisi, sasa nitasema sijui hizo takwimu anazozungumza yeye ni zipi.

Lakini nataka niseme tu na taarifa hii hapa, nitamuomba Mheshimiwa Khalifa baadaye aje aingalie na ataona hali ya mtanzania zaidi ya shilingi ya 1000 kwa siku tunazungumzia tuko zaidi ya dola kwa sasa hivi dola moja nukta mbili kwa siku hiyo ndiyo kipato cha Mtanzania. Kwa hiyo namwambia Mheshimiwa aje anione nimpe ripoti hii aisome na ataelewa zaidi. (*Makofi*)

Na. 38

**Usafiri wa Mabasi kati ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. BASIL P. MRAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekusudia kufuta kabisa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha (*Non – Tariff Barriers*); na kwa kuwa, Serikali ya Kenya imezuia mabasi toka Tanzania kwenda Nairobi kupitia Rombo – Tarakea:-

Je, ni nini hasa sababu za kufanya hivyo na ni lini njia hiyo rasmi ya Afrika Mashariki itakuwa huru kupitisha mabasi toka Tanzania hasa kwa sababu barabara inawekwa lami upande wa Tanzania na Kenya?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba Mbunge wa Rombo napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala ya uchukuzi na usafirishaji yanasimamiwa na ibara ya IV (1) ya Mkataba wa usafirishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 200. Chini ya Mkataba huo mwananchi yeyote anayetaka kufanya biashara ya uchukuzi wa bidhaa abiria anatakiwa kuomba leseni kupitia mamlaka husika ndani ya Taifa lake kulingana na njia *(Routes)* zilizoainishwa katika mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuzitaja njia hizo kama ifuatavyo:-

Mombasa – Nairobi – Kampala; Mombasa – Horohoro – Tanga – Dar es Salaam; Dar es Salaam – Arusha – Namanga- Kajiado – Nairobi; Namanga – Arusha – Dodoma – Iringa – Tunduma; Nairobi – Isebania – Musoma – Mwanza = Biharamlo; Mombasa – Voi – Taveta – Holili – Moshi – Arusha, Dar es Salaam – Dodoma – Isaaka – Mtukula – Masaka – Kampala; Mbarara – Kikagati – Kayanga – Bukoba; Kampala – Mtukula – Kigoma – Tunduma; Mbale – Moroto – Londwa – Wamurupul na Nakuru – Kisumu – Busumu Busia – Kampala.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mkutano wa Mawaziri wa Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Januari, 2009 njia ya Marangu – Rombo – Tarakea – Loitoktok – Emali – Nairobi, iliingizwa kwenye orodha ya njia mpya ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa njia ya Rombo – Tarakea – Loitoktok – Emali – Nairobi imo kwenye orodha ya njia *(Routes)* zilizoongezwa katika mtandao wa barabara za jumuiya, mhusika anayo haki ya kupitisha mabasi katika njia hiyo kama ilivyokubalika kuanzia Januari, 2009 baada ya kupata leseni ya usafirishaji wa bidhaa na abiria kutoka mamlaka ya usafirishaji ya nchi husika.

Hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge awashauri wahusika wapeleke maombi yao rasmi kwenye mamlaka ya udhibiti wa usafirishaji wa nchi kavu na majini *(SUMATRA)* ambapo ombi hilo litashughulikiwa katika Bodi ya leseni ya Taifa *(Tanzania Licensing Board*) kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada anazochukua kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatoa huduma kwa wananchi.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliofanya ndani ya Afrika Mashariki na Kenya kwenyewe ili barabara hii iweze kutambulika kama ilivyokuwa imekusudiwa toka mwanzo.

Je, wanaweza sasa wakafanya maandalizi ili barabara hiyo ya Afrika ya Mashariki iweze kuzinduliwa kwa shangwa na vigelele na mbwembwe zote na viongozi wa Afrika ya Mashariki kama vile walivyofanya juzi kuweka jiwe la msingi kule Namanga?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kwa mikono miwili nizipokee pongezi zake na kwa niaba ya Wizara tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maandalizi ya kuzinduliwa barabara hiyo na viongozi wa Afrika Mashariki tunaona ni jambo nzuri na tunapokea ushauri na tunawapelekea wahusika ili hatua zichukuliwe.

Na. 39

**Barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na ucheleweshaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida:-

(a) Je, ni sababu gani hasa zilizofanya mradi huo kuchelewa?

(b) Je, ni hasara gani zimepatikana kwa kuchelewa kwa mradi huo?

(c) Je, ni lini hasa mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi ya ujenzi wa barabara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelzaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida, yenye urefu wa kilometa 244 umegawanywa katika sehemu mbili ambazo ni Dodoma hadi Manyoni (km. 127) na Manyoni hadi Singida (km. 117). Mpaka sasa jumla ya kilometa 173 za lami katika barabara hii zimejengwa na kukamilika.

Kutokana na mmakandarasi kuchelewesha na kushindwa kukamilisha mradi huo kwa wakati, Serikali ililazimika kukatisha mikataba yao. Kwa sasa kazi zilizobaki kati ya Mhalala – Manyoni (km. 17) na Manyoni – Isuna (km. 54) ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi kwa kutumia makandarasi wengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu sababu zilizofanya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma - Manyoni – Singida kuchelewa ni kushindwa kwa makandarasi kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba.

Aidha, mikataba hiyo ilisitishwa baada ya Serikali kuridhika kuwa makandarasi huyo asingeweza kukamilisha kazi hiyo.

(b)Mheshimiwa Spika, hasara iliyopatikana kutokana na ucheleweshaji huo kwanza ni wananchi kuchelewa kupata huduma bora ya barabara mapema kama ilivyokusudiwa.

Pili ni gharama za ujenzi kuongezeka. Awamu ya ujenzi huo ulipangwa kugharimu shilingi bilioni 63 kwa sehemu ya Dodoma – Manyoni na shilingi bilioni 30.429 kwa sehemu ya Manyoni – Singida. *(Makofi)*

Hivi sasa ujenzi huu unategemewa kugharimu shilingi bilioni 144.613 kwa sehemu ya Dodoma – Manyoni na shilingi bilioni 60.669 kwa sehemu ya Manyoni – Singida.

(c)Mheshimiwa Spika, mkandarasi anayejenga sehemu ya mhalala – Manyoni (km. 17) ni *Estim Construction Co. Ltd.* na anatarajia kukamilisha sehemu hiyo ifikapo Novemba 2009 na yule wa sehemu ya Manyoni - Isuma (km. 54) ambaye ni *China Geo Corporation (CGC)* atakamilisha ujenzi wa sehemu hii ifikapo Desemba, 2010.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi, Waziri amesema hapa kwamba Serikali imepata hasara ya bilioni 110 kutokana na ucheleweshwaji ambao umefanywa na wakandarasi, lakini kadri ninavyoelewa mikataba yeyote huingiwa kwa pande zote mbili, kwa yule anayechelewesha na kwa yule anayesababisha usumbufu huo.

Je, kwa hasara hiyo ya shilingi bilioni 110 ambayo Taifa hili imeipata hawa Wakandarasi wamechukuliwa hatua gani au kama ni watumishi wa Serikali wamechukuliwa hatua gani kufidia hasara hii kubwa? (*Makofi*)

Swali la pili ni kuhusu barabara ya kutoka Isuna kuja Manyoni ambayo ndiyo inajengwa na *Geo China*, Mkataba uliingiwa tangu 2008 wa kilomita zipatazo 60 hivi, lakini mpaka leo hata kilomita moja hajaweka lami na anatuambia mpaka 2010 barabara hiyo itakamilika.

Je, haoni kwamba kuna uzembe hapa kwanza wa Mkandarasi, *Consultant* na wenyewe Serikali wanafanya uzembe?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Luca L. Selelii, Mbunge wa Nzega kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua zilizochukuliwa kutokana na hasara hii iliyoainishwa hapa nataka niseme tu kwamba hapa tulichoainisha ni ile tofauti kati ya gharama za ujenzi zilizokuwa zimekusudiwa awali na gharama ambazo zitatumika katika ujenzi huu wa kukamilisha.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mchakato huu Serikali iliona kwamba kwanza ichukue hatua za haraka za kuhakikisha kwamba ujenzi wa barabara hizi unakamilika wakati taratibu na mwingine sasa wa kufuatilia haya mambo yaliyosababisha mpaka ucheleweshaji huu ukatokea zinaendelea kufuatiliwa.

Kwa hiyo, kwa hivi sasa pengine ingekuwa siyo rahisi sana kusema moja kwa moja juu ya hatua zilizokwisha kuchukuliwa kwa sababu bado mazungumzo na mashauriano kuhusiana na hii kesi ya kucheleweshwa kwa mradi huu inaendelea.

Lakini tuliona kwamba tuchukue kwanza hatua za haraka za kuhakikisha kwamba utengenezaji wa barabara hizi unakamilika ili wananchi waweze wakapata huduma ya barabara kwa wakati uliopangwa.

La pili, kuhusu Mkandarasi anayejenga hii barabara ya Kisuna Manyoni kwamba amechukua muda mrefu. Nataka tu niseme kwamba kwa mujibu wa Mkataba ambao Mkandarasi huyu aliusaini ndivyo unavyoonesha muda huo na kwa maelezo ya Mkandarasi pamoja na Wasimamizi wa mradi huu ni kwamba inayofanyika pale sasa hivi ya angalau kuweka lile tuta na kwa muda uliobakia tuna uhakika kabisa kazi itakamilika kwa muda uliopangwa kwenye mkataba. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, yatakuwa matumizi mazuri zaidi ya muda ikiwa tutamaliza maswali yaliyobaki ya Wizara ya Mawaziliano.

Kwa hiyo, sasa namuita Mheshimiwa Said Juma Nkumba kwa swali linalofuata.

Na. 40

**Mawasiliano ya Simu za Mikononi**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tarafa ya Kiwele yenye Kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda haina mawasiliano ya simu za mkononi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha Kampuni za Simu za Mkononi kuanzisha huduma hiyo kwenye Kata nilizozitaja?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Kampuni ya Simu ya *Zain* inaendelea na mkakati wake wa kufikisha huduma ya mawasliano kwenye maeneo ya Tarafa ya Kiwele katika Kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda sanjari na mkakati huo, Zain imepanga kujenga mnara katika kijiji cha Kitunda, ujenzi ambao umeidhinishwa kufanyika katika awamu ya pili ya Bajeti ya Kampuni hiyo ya mwaka 2010 yaani (robo ya pili ya mwaka 2010).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake, kampuni ya *VODACOM* imebaini maeneo ya Tarafa ya Kiwele kwenye Kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda pamoja na maeneo mengine yaliyo jirani na imeanza kufanya tathmini ya kiufundi kwa ajili ya kuweka mtambo wa mawasiliano katika eneo la Rungwa ili kukidhi mahitaji kwenye maeneo ya

Kipiri, Kiloli na Kitunda. Baada ya tathmini ya kiufundi kukamilika *VODACOM* itaingia katika hatua ya utekelezaji kwa kuweka mtambo wa mawasiliano kwa ajili ya maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kampuni ya *ZANTEL* haina mawasiliano katika maeneo ya Kata za Kipiri, Kiloli, na Kitunda yaliyopo kwenye Tarafa ya Kiwele. Kampuni hiyo imepanga kuyajumuisha maeneo hayo kwenye mipango yake ijayo.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, wakati wa kufikisha mawasiliano ya simu za mkononi kwenye Tarafa ya Sikonge, msaada mkubwa niliupata kutoka kwenye Wizara na Naibu Waziri huyu huyu alihusika zaidi katika kuhamasisha makampuni hayo kuleta simu za mkononi kwa uharaka zaidi kabla ya muda wa wakati uliokuwa umepangwa.

Je, katika kazi hiyo aliyoifanya katika Tarafa hiyo ya Sikonge anaweza vilevile akanisaidia kwa sababu hajabadilika ni yuleyule. Je, atanisaidia katika maeneo haya mapya sasa kuharakisha ili kazi hii iishe kabla ya muda uliopangwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, kama ifuatavyo:-

Napenda nimhakikishie kwamba kama ninavyofanya siku zote kwa Wabunge wote nitaendelea kusisitiza kampuni hii ihakikishe inajenga kama ilivyoahidi kabla ya 2010 mwishoni yaani kabla ya Oktoba. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

Kwa kuwa hapa, imejionyesha Mheshimiwa Waziri huyu ameweza kufanya kazi hiyo kwa umakini sana katika maeneo anayotoka Mheshimiwa Said Juma Nkumba. Lakini ameshindwa kufanya kazi ya namna hiyo hiyo katika maeneo ya muda mrefu niliyomweleza ya kule Mgazini kunakozalisha chakula kwa wingi, kwa ajili ya wananchi wa Tanzania, kule Ifinga kwenye Hifadhi ya Wanyamapori. Hifadhi kubwa sana na kule Muhukuru mpakani mwa Tanzania na Msumbiji.

Je, Mheshimiwa Waziri anataka kuniambia leo kwamba yeye ni mfanyakazi kwenye eneo la Mheshimiwa Saidi Nkumba tu na siyo kule kwenye Jimbo la Peramiho maeneo niliyoyasema? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, kama ifuatavyo:-

Nikiri kwamba juhudi zangu zote kwa makampuni haya kuomba mawasiliano ya simu katika maeneo ya Mheshimiwa Mbunge, Mgazini, Ifinga na kadhalika kote huko bado hazijazaa matunda.

Lakini nimefanya juhudi za kutosha na Mheshimiwa Mbunge naye anikubalie kwamba mimi sina Jimbo fulani, mimi ninatoka Pemba kote kwangu mimi ni mawasiliano yawafikie wananchi ili waweze kuyatumia.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hakuna nia mbaya yoyote ya kumnyima yeye mawasiliano inawezekana tu mipango ya makampuni hayo bado hayajatimia na tunapo waomba kufikisha maeneo fulani ni kwamba wananyofoa mipango yao waliyoipanga kwenda kukidhi mahitaji ya wale ambao tunawapelekea.

Lakini nimhakikishie Mheshimiwa kwamba nitaendelea kuwasisitiza kampuni ili mawasiliano yafike maeneo hayo hasa mpakani mwa Msumbiji na Tanzania. (*Makofi*)

Na. 41

**Kuhamasisha Kampuni za Simu Kujenga Minara Mlola**

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Kata ya Makanya, Mlola na Malibwi Tarafa ya Mlola Wilayani Lushoto kuna idadi kubwa ya watu na Taasisi mbalimbali za Serikali ambapo mahitaji ya simu za mikononi ni makubwa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzihamasisha kampuni za simu za *VODACOM, TIGO, ZAIN, TTCL* na *ZANTEL* kujenga minara ya simu za mikononi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya simu ya *VODACOM* tayari imeona umuhimu wa kuweka minara katika kata za Mlola, Ngwelo na Makanya ili kuwezesha mawasiliano katika maeneo ya Kwekongo, Kwekanga, Mlola, Ngwelo, Makanya yenyewe na Kwemkole. Tayari thathmini imefanyika katika maeneo hayo na mpango wa kuanza kufunga mnara katika kata moja ya Ngwelo ambao utawezesha mawasiliano katika kata hiyo na maeneo jirani ya Mlola, Kwekongo na Kwekanga unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *ZAIN* ina mpango wa kujenga mnara kwenye kata ya Mlola, Wilayani Lushoto mapema mwaka 2010, na hapa nitaendelea tu kumsisitizia Mheshimiwa ili shughuli hii ifanyike mapama.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *ZANTEL* inao mnara wa mawasiliano katika eneo la Soni, Mvurui uliopo umbali wa kilometa 1.6 kutoka Makanya na kilometa 14 kutoka Mlola.

Aidha, mnara huo upo umbali wa kilometa 14 kutoka Malibwi na pia imejenga mnara mwingine eneo la Vuli umbali wa kilometa 13 kutoka Malibwi. Huduma za mawasiliano za *Zantel* zimeboreka sana katika maeneo hayo. Napenda atukubalie kwamba maeneo hayo tutayasisitiza ili mawasiliano yaweze kufikishwa.

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA**: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na mimi naomba nitumie nafasi hii kutambua jitihada zake anazozifanya kutusaidia kufikisha mawasiliano ya simu katika maeneo ya wananchi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili tu madogo ya nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akanifahamisha ni vijiji na vilima vipi itakapowekwa minara hiyo ili niweze kufuatilia iwapo anafahamu?

Pili, kwa vile Nishati ya umeme ni muhimu sana kwa minara hiyo ya simu na wananchi kuweza ku-*charge* simu zao. Je, ni lini Serikali itafikisha huduma ya umeme katika maeneo haya?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, kama ifuatavyo:-

Kwanza nikiri kwamba hivyo vijiji na vilima ambapo mawasiliano hayo yatawekwa sivijui labda nimchukue tu Mheshimiwa Mbunge nimpeleke kwa kampuni zinazohusika ili apate *details* kutoka kule. Lah! Anataka mimi niwe Balozi wake kuwauliza kampuni ni vijiji vipi na vilima vipi kitu ambacho wataniona ni mtu wa maajabu lakini naweza kufanya kwa ajili yake.

Pili, minara ya mawasiliano kikawaida huwa wanaweka jenereta lakini kama ni masuala ya umeme basi tuombe tu mwenyewe anayehusika na masuala ya umeme aone umuhimu wa mawasiliano, na nina hakika anaona umuhimu wa mawasiliano hasa kwa kutumia umeme katika maeneo hayo.

Lakini kwa sababu umeme haupo chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, basi tutamwomba Mheshimiwa anayehusika aone umuhimu katika maeneo yale. Lakini niseme tu Lushoto *topography* yake ni ngumu kidogo na mawasiliano ni lazima wenye makampuni ya simu wachukue juhudi ya kufikiria ni teknolojia gani inafaa katika maeneo yale. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu matangazo. Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, nao ni Bi Nuru George na Bi Fatma Abdallah, karibuni sana. Hakueleza wanahusika vipi lakini basi ni wageni wake tu.

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anatangaza kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira saa saba katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati saa saba mchana katika ukumbi namba 231 jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea kutoka Serikalini kupitia Wizara ya Fedha, vitabu vilivyochapishwa upya. Kitabu cha pili na cha nne ni muhimu jamani kwa sababu wakati wa makadirio msije mkatumia vile mlivyopewa Dar es Salaam wakati wa Kamati. Imebidi vichapishwe upya kwa sababu vilikuwa na makosa, makosa ya uchapaji vile vya awali. Ilionekana si vema na isingeleta ufanisi wa tija kuweka *addendum* ndefu sana ya makosa ya uchapaji. Kwa hiyo, vitabu *volume II* na *volume IV* Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo nadhani vimekwishagawiwa katika visanduku vyetu kule tuvitumie hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina furahi kuwafamisha kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 10 June, 2009 pale *Kilimani Club* alipotuhutubia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Dodoma na kupitia kwao alilihutubia Taifa basi vitabu vya hotuba viko tayari na vitagawiwa kwa kila Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Huo ndiyo mwisho wa matangazo sasa naomba Katibu atuongoze kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2009/2010

*(Majadiliano yanaendelea)*

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa mujibu wa Katiba yetu Bunge limepewa dhamana kwa niaba ya wananchi

kuisimamia Serikali na kwa hivi siku za karibuni Bunge lako Tukufu limekuwa na limeaminika sana na wananchi chini ya uongozi wako.

Juzi tumefanya marekebisho katika Kanuni zetu mbalimbali kutokana na mtikisiko wa hali ya kiuchumi ya dunia. Tumetengua Kanuni kwa ajili ya mambo mengi sana ili Serikali iweze kuanza utekelezaji wa Bajeti yake ambayo tutaipitisha siku ya alhamisi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka uniondolee dukuduku na wasiwasi kwamba kumetoea sasa hivi baadhi ya miradi imeanza kutumika hata kabla ya Bunge lako Tukufu halijaidhinisha matumizi ya pesa hizo.

Sasa mimi najiuliza huu ni utaratibu mpya wa Kanuni mpya zipi?

**SPIKA:** Mfano!

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nadhani sasa nitumie tu vitabu vile vya zamani kile kitabu cha nne cha zamani maana yake umetutangazia kwamba vitabu vingine vipya vipo.

Katika kitabu cha zamani cha nne ukurasa wa 187 kuna hii barabara ya Chalinze – Segera – Tanga, ambayo imetengewa fedha za nje bilioni 22 na imetengewa fedha za ndani bilioni 100.

Mheshimiwa Slpika, hivi karibuni barabara hii imewekewa jiwe la msingi na Makamu wa Rais lakini ukiangalia kwenye vitabu humu imeombewa fedha. Sasa ni Bunge gani ambalo liliidhinisha hizi fedha ziweze kutumika?

Je, kama tuna mawazo tofauti na matumizi hayo, tuna nafasi gani sisi kama Wabunge ambao tumepewa wajibu na wananchi kurekebisha?

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni ile ya Same kuja Korogwe, imetengewa fedha za nje bilioni 44 ambayo inakwanguliwa upya. Kuna barabara zingine hazipo kabisa, hawa wenzetu wanakwangua upya, hivi tunayo nafasi gani sisi kama Wabunge ambao tumepewa dhamana na wananchi kuishauri Serikali na kuisimamia?

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu na mwongozo wako, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa lile la pili, nadhani Mheshimiwa Mbunge unatanguliza shughuli ambazo wakati wake haujafika. Kwa hiyo, ni kinyume cha Kanuni kwa hiyo hilo wala halihitaji mwongozo, wakati ukifika kwenye sekta ya Miundombinu unaweza ukipenda ukalileta. Lile la kwanza ni zito sana kama kuna matumizi ambayo yanafanyika sasa hilo ni tatizo lakini kwa sababu sijasikia kutoka kwa upande wa Serikali inawezekana kuna maelezo. Kwa hiyo, natoa muda wa kesho kwa Serikali ili keshokutwa niweze kutoa mwongozo wangu. Kwa hiyo, ni juu ya Serikali kuweza kuandaa maelezo ambayo tutayapata kesho na kwa sasa basi shughuli zilizopangwa ziendelee.

Mwongozo nitautoa keshokutwa baada ya kupata maelezo ya Serikali.

Niwakumbushe tu Waheshimiwa kama tulivyokubaliana na Mwenyekiti na pia msemaji kambi ya upinzani wana dakika 40 kila mmoja kwa sababu wanazungumzia mipango na Bajeti yaani fedha. Kwa hiyo, dakika 20 kila upande ingawa ni katika mtiririko wa hotuba moja.

Kwa hiyo, namwita mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa maoni ya Kamati.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA, MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 96(6) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2007, naomba kutoa Maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008; Malengo ya Uchumi katika Kipindi cha Muda wa Kati (2009/2010/2012), Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 na Mapendekezo ya Serikali Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote Kamati inapenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mhe. Mustafa H. Mkulo, (Mb.) kwa taarifa zake nzuri alizozitoa hapa Bungeni; ile ya Hali ya Uchumi ya Taifa *(The State of the Economy)* na ile ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2008/2009 na Mapendekezo ya Serikali Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010. Kamati yangu ilipitia na kujadili taarifa hizi tarehe 1 Juni 2009 na tarehe 4 Juni, 2009 kwa kufuatana. Kamati imezitathmini kwa kina taarifa husika na kutoa mapendekezo na ushauri unaopaswa kuchukuliwa na Serikali. Kabla ya kujadili taarifa hizi Kamati vilevile ilipata fursa ya kujadili utendaji wa Benki Kuu ya Tanzania na Hali ya Uchumi kwa Kipindi cha Julai, 2008 hadi Aprili, 2009, pamoja na taarifa kuhusu mafanikio, changamoto na mikakati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano na Wizara, hali dhahiri iliyojitokeza katika kutathmini taarifa zote mbili zilizowasilishwa, changamoto kubwa iliyojitokeza ni kukabiliana na mdororo wa Sekta ya Fedha Duniani ambao umesababisha msukosuko na mtikisiko wa Sekta hiyo na hivyo kufanya uchumi wa Dunia kuyumba pamoja na kuathirika kwa Sekta ya Kifedha.

Hapo awali, Kamati ilipata taarifa kuwa kutokana na Mabenki yetu kutokufungamana na mabenki ya Kimataifa, Sekta yetu ya fedha isingeathirika na hivyo kuifanya Serikali kuchukua hatua madhubuti za kujihami na msukosuko huo ulioleta athari mbali mbali kama vile mabenki kufilisika, kuanguka kwa biashara duniani, kuanguka kwa makampuni, Wakopaji kushindwa kulipa mikopo yao na ajira kuathirika kwa kiwango kikubwa, kutokana na *financial melt down* na *economic slow down* iliyotokea. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zote zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, msukosuko wa Sekta ya Fedha Duniani umeanzishwa na nchi tajiri za Ulaya na Marekani. Hali hii imeziingiza nchi zinazoendelea kama Tanzania katika mkanganyiko wa dhana na tafsiri ya jinsi ya kukabiliana na tatizo zima. Chanzo cha tatizo kilikuwa ni mtikisiko wa Sekta ya Fedha *(international financial Crisis)* tofauti na mtikisiko wa Uchumi duniani *(Global economic Crisis).*

Hata hivyo licha ya Sekta yetu ya Fedha kutokufungamana na Sekta ya Fedha Kimataifa, bado tuna mashirikiano katika Nyanja mbalimbali kiuchumi, mojawapo ya eneo ni lile la nchi zilizoendelea kuwa ni soko la bidhaa zetu muhimu tunazozalisha na chanzo kikubwa cha mapato ya fedha zetu za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati kutokana na hali hii ilishawishika kuishauri Serikali kuelezea haraka Mipango na Mikakati ya Dharura ya Kujihami na kujinusuru na athari zozote za kudorora kwa uchumi wetu utakaogusa moja kwa moja huduma nyingine za Kiuchumi na Jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri wa Kamati, tunapenda kuipongeza Serikali kuwa sikivu na ya kuwajibika kwa kueleza Mipango na Mikakati mizuri iliyoandaliwa kukabiliana na msukosuko wa uchumi iliyotangazwa Kitaifa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mipango na Mikakati iliyoandaliwa imejenga imani kubwa kwa Wananchi ya jinsi Serikali itakavyopambana na makali ya uchumi na hali ngumu ya maisha. Mheshimiwa Rais amefafanua vyema na kwa usahihi mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya kunusuru uchumi wetu pamoja na mbinu za kuokoa uchumi wetu. Hotuba ya Mheshimiwa Rais imewatendea haki wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara na wale wananchi wa kipato cha chini. Kamati inaishauri Serikali kumuomba Mheshimiwa Rais atoe idhini ya hotuba yake itolewe nakala ili zigawanywe kwa Wabunge hapa Bungeni nashukuru sana Mheshimiwa Spika umesema kwamba hili limeshafanyika ili itumike kama rejea pamoja na taarifa nyingine tulizopokea hapa.

Mheshimiwa Spika, Mipango na Bajeti ya 2009/10 iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, vimezingatia msukosuko wa uchumi duniani hasa kwa kuwalenga wale wenye uwezo mdogo kimapato. Maeneo kadhaa yaliyoangaliwa ni kuendeleza Sekta ya Kilimo inayoajiri wananchi wengi; imeangalia kwa kina eneo la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kupitia mifuko mbalimbali; imeweka msisitizo katika kuendeleza sekta ya huduma za jamii, Sekta ya Elimu imetengewa fedha nyingi na hatimaye hatua za kibajeti za mapato *(Revenue Measures)* ambazo pamoja na kufuta misamaha mbalimbali ya kodi, hazikuathiri au kuongezea ugumu yale maeneo yanayowahusu wengi wa Wananchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa bajeti yenye mwelekeo wa maendeleo. Pamoja na maoni ya Jumla ya Kamati, Kamati ingependa kugusia baadhi ya maeneo kama njia ya kuishauri Serikali katika kutekeleza Mipango na Bajeti katika kipindi kijacho cha Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Riba za Mabenki. Moja ya eneo ambalo Kamati inaishauri Serikali ni lile la kupunguza riba za mikopo. Hakuna uchumi unaoendelea duniani bila

ya matumizi ya mikopo na utaratibu mzuri wa kutoa mikopo. Kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu riba za dhamana za Serikali zimeanza kushuka kutoka asilimia 13.33 Machi 2009 na kufikia asilimia 9.73 mwezi Mei 2009. Hata hivyo, riba zinazotozwa na mabenki kwa mikopo ya Sekta binafsi bado ni za viwango vya juu kwa wastani wa asimilia 15.45 Mwezi Aprili, 2009. Viwango hivi vya riba havitoweza kuwezesha shughuli za uchumi kupanuka kwa kasi zaidi. Ipo haja ya hatua za makusudi kuchukuliwa katika Sera za Kifedha ili kupunguza viwango hivi vya juu vya riba. Kamati inaishauri Benki Kuu kuandaa mazingira ya kuyawezesha mabenki kuwa na vyanzo nafuu vya fedha. Uharakishwe utaratibu wa *Credit Reference* ili kupima hadhi ya wakopaji kutokana na viwango vyao vya hali ya uchumi hapo hapo ikizingatia vile vile viwango vya riba vya dhamana za Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuweka kipaumbele katika kusukuma utekelezaji wa maeneo yafuatayo, ili suala zima la upatikanaji wa huduma za mikopo ufanyike kwa ufanisi na tija. Maeneo hayo yanahusisha mikopo ya makazi *(mortgage finance)*, mikopo ya karadha *(finance leasing)*, mageuzi katika mifuko ya pensheni, Benki ya Raslimali ya Tanzania ambayo imeanzisha dirisha la kukopesha miradi ya Sekta ya Kilimo pamoja na uboreshaji wa *Microfinance.*

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa Bei. Bado mfumko wa bei utaendelea kuleta hali ngumu ya maisha hususan pale ambapo juhudi zaidi hazitaelekezwa kwenye kuongeza uzalishaji wa chakula. Mfumko wa bei *(headline inflation)* umekuwa wa kuongezeka kufuatia ongezeko kubwa la bei za vyakula, gharama za usafirishaji na mahitaji makubwa ya nafaka katika nchi jirani. Bei za vyakula huchangia asilimia 55.9 ya mfumko wa bei. Hadi Aprili, 2009 mfumko wa bei ulifikia asilimia 12.0 kutoka asilimia 13.0 Machi 2009. Hii ilitokana na kushuka kwa mfumko wa bei za vyakula kutoka asilimia 18.5 hadi asilimia 17.8. Ukiondoa bei ya vyakula, mfumko wa bei ulishuka toka asilimia 8.9 Septemba, 2008 na kufikia asilimia 2.9 Aprili, 2009 *(underlying inflation).*

Mheshimiwa Spika, picha hii inaeleza wazi kuwa jitihada zitakapowekwa katika kuongeza uzalishaji wa chakula, hali ngumu waipatayo wananchi itapungua kwa kiwango kikubwa. Aidha, kutokana na upungufu wa chakula katika mikoa kadhaa nchini kutokana na ukame uliojitokeza, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utaratibu wake wa kupeleka chakula katika maeneo hayo kutoka yale maeneo yenye chakula cha ziada kama Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya n.k. Kwa ujumla wake bado eneo la kuzalisha chakula cha kutosha na changamoto kwa Taifa. Njia pekee ya kupunguza hali ngumu ya maisha ufumbuzi wake ni kudhibiti mfumko wa bei, kuongeza uzalishaji wa chakula, kudhibiti ujazi wa fedha pamoja na kudhibiti viwango vya riba ili kupunguza gharama za mikopo. Aidha, maeneo hayo yashirikishwe na kuibua kwa uchumi, kuboresha miundombinu – barabara, reli na bandari na kubuni vyanzo vingine vya mapato ambavyo havitaongeza kero au ugumu wa maisha kwa wale wananchi wenye vipato vya chini, hususan wakulima vijijini.

Mheshimiwa Spika, mikakati wa kuboresha bandari, moja ya eneo ambalo Kamati imelisisitizia ni utendaji kazi wa Bandari zetu, hususan ile ya Dar-es-Salaam. Kwa mujibu wa takwimu zilizopokelewa na Kamati, Bandari yetu ya Dar-es-Salaam imepoteza kiasi kikubwa cha mgao wake wa soko *(market share)* kwa bandari shindani

ya Mombasa. Kati ya mwaka 2001 – 2007 mgao wa Bandari yetu umepungua kutoka asilimia 6 hadi asilimia 1 kwa shehena ya Uganda, asilimia 39 hadi 24 kwa shehena ya Rwanda, asilimia 93 hadi 75 kwa shehena ya Burundi ingawaje ongezeko la asilimia 40 hadi 49 liliripotiwa kwa shehena ya *DR Congo.*

Mheshimiwa Spika, udhaifu wa miundombinu ya reli ya *TAZARA* na reli ya kati umechangia hali hii pamoja na ukosefu wa vitendea kazi. Hili ni eneo ambalo licha ya bandari yetu kuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya takribani tani 15 milioni kwa mwaka, hivi sasa uwezo unaotumika ni tani 6 milioni tu (kwa maana ya pakuliwa/pakiwa).

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali, pamoja na mambo mengine, kutatua tatizo la kitengo cha Kontena *(TICTS)* la kushuka kwa tija ya kupakia na kupakuwa Kontena. Hivi sasa *TICTS* inafanya mizunguko 18 badala ya 25. Ipo haja ya kutatua tatizo la ukaaji wa makontena muda mrefu bandarini (siku 25 badala ya siku 7), ufanisi mdogo wa reli, urasimu katika uandaaji wa nyaraka, wateja kutochukua makontena yao kwa wakati na ufinyu wa nafasi ndani ya Bandari.

Aidha, Kamati imeishauri Serikali kuhuisha baadhi ya sheria ambazo zinakwaza ufanisi wa Bandari zetu hususan Sheria ya *TRA – East African Community Customs Management Act*, 2006 (R.E.), Sheria ya *TRA – VAT Act* 1998 ile ya ulipaji wa VAT katika huduma za *Stevedoring* na Sheria za Bandari *(Ports Act, 2004).* Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuta ulipaji wa *VAT* kwa huduma za *Stevedoring* ambazo kwa muda mrefu zilikuwa hazitozwi kwenye bandari shindani ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza taratibu za kupata maeneo ya kufanyia kazi nje ya bandari *(peri-habour)* na uanzishwaji wa *Inland Container Depots (ICD).* Ni muhimu mazingira ya ushindani yakaimarishwa katika Bandari kwa kukaribisha Sekta binafsi, pamoja na Serikali kugharamia miundombinu muhimu ya Bandari moja kwa moja, badala ya kuiachia Bandari yenyewe kugharamia miundombinu ya msingi. Bandari nyingi za nchi jirani Serikali zinafuata utaratibu huu.

Sera ya *Public Private Partnership,* wakati wake wa kutekelezwa na Serikali katika maeneo muhimu ya kujenga uchumi hasa Bandari ni sasa.

Mheshimiwa Spika, mapato ya serikali, Kamati inaendelea kuipongeza TRA kwa juhudi kubwa za ukusanyaji wa mapato katika uchumi, licha ya kuwa katika kipindi cha 2008/09 makusanyo ya mapato hayakufikia lengo kwa asilimia 9.2 (trilioni 3.4 badala ya trilioni 3.8) kutokana na sababu mbalimbali pamoja na ile ya msukosuko wa uchumi wa sekta ya fedha duniani, Kamati imeishauri TRA kuendelea na utekelezaji wake wa Mpango Mkakati unaolenga kuboresha tija na ufanisi. Upo umihimu wa TRA kuendelea kufanya marekebisho ya viwango vya kodi mbalimbali (*Adjustment of Excise Duties for non petroleum products)* kufuatana na mfumuko wa bei pamoja na kuhuisha kikamilifu eneo la sheria ya madini linalogusa misamaha ya mafuta kama ilivyopendekezwa na Tume ya Bomani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa, marekebisho haya yafanywe kwa uangalifu mkubwa ili kuepuka kuathiri uzalishaji na upatikanaji wa mapato katika Sekta husika, hasa ikizingatiwa kuwa ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za Madini kwa bei za mwaka 2001 imeshuka kutoka asilimia 10.7 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 2.5 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza Viwanda vya kuhudumia Sekta ya Madini ambayo haijaendelezwa sana kwa mantiki ya kuongeza thamani ya madini yetu *(Value Adittion)*. Shirika la Madini Tanzania (*STAMICO*) lina mpango wa kuanzisha Kituo cha Uhandisi wa Migodi kwa ubia hapa Dodoma. Mpango huu uungwe mkono na Serikali kwa lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ipo haja ya kuboresha mwendelezo wa miundombinu kwenye maeneo ya madini. Hii itapunguza utoaji wa misamaha ya kodi kwa Wawekezaji na hivyo kubakiza faida na mapato katika Uchumi wetu. Tujifunze wanavyofanya Botswana. Serikali ya Botswana inachangia hisa zake katika sekta ya madini na shughuli zinafanyika bila ya kutoa misamaha kama inavyofanya Tanzania. Pamoja na hatua hizi kwa sababu Sekta ya Wachimbaji wadogo inazidi kupanuka, upo umuhimu wa Serikali kuendeleza kujenga mazingira bora ya utendaji kwa wachimbaji hawa.

Hili ni eneo la kujenga ajira na ndio maana hata katika kuhakikisha Sekta ya Madini ya Vito inachangia katika kunusuru uchumi, Serikali imeamua Wachimbaji hawa wasilipe mrahaba kutokana na mapato yao kwa kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuondoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika maeneo kadhaa. Katika kipindi cha Julai 2008 hadi Aprili 2009, misamaha ya kodi ilifikia asilimia 30 na asilimia 17 kwa Idara ya Forodha na Idara ya Kodi za ndani kwa kufuatana, Tanzania Bara. Misamaha ya Kodi Zanzibar ilifikia asilimia 65.4 ya mapato yote. Viwango hivi ni vikubwa, na mara nyingine misamaha hii imefungua mwanya wa ukwepaji kodi na hivyo kuvuja kwa mapato. Misamaha ya kodi ni asilimia 3.5 ya Pato la Taifa Tanzania wakati Kenya ni asilimia 1 na Uganda ni asilimia 0.4 tu. Kwa hali hii, mapendekezo ya Serikali kurejea sheria zinazotoa misamaha ya kodi na taratibu za usimamizi ili kubadilisha mwenendo wa ukuaji wa misamaha ya kodi ni vyema tukayaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya uamuzi wake wa kuondoa msamaha maalum wa VAT kwa asasi zisizo za kiserikali *(NGOs)* na Mashirika ya dini. Hatua ambayo itahusisha madhehebu yote ya dini. Kwa yale mashirika ya dini ambayo yamejikita moja kwa moja katika maeneo ya utoaji na uchangiaji wa huduma za jamii hususan elimu, afya na maji, Kamati inashauri yasiondolewe msamaha huu. Kwa sababu maeneo haya yanawagusa moja kwa moja Watanzania walio wengi, na kufutwa kwa msamaha huu kunaweza kuathiri kwa kiwango fulani uchangiaji na utoaji wa huduma hizi hasa vijijini. Ni vyema Serikali ikakaa na Mashirika haya ya dini na kutoa mwongozo na ufafanuzi mzuri wa namna ya kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi ili msamaha huu uendelee kutolewa si kwa vifaa vya

kiroho na ibada tu, bali iguse pia yale maeneo yanayoisaidia Serikali katika uchangiaji wa kukua kwa elimu, afya na huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kuboresha miundombinu ya reli, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mkakati wa kuiboresha reli ya kati kwa ujumla wake. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Fedha na Uchumi, mkakati huo unalenga vile vile kuimarisha Bandari na vitu vinavyoendana navyo na bandari kama lango kuu la biashara. Kamati imearifiwa kuwa nchi jirani nazo zimeonyesha shauku ya kuchangia nguvu katika kuboresha reli yetu ya kati. Changamoto kubwa ni ili reli ya Kati iweze kusaidiwa na wafadhili, iko haja ya kukarabati reli kutoka Isaka hadi Dar-es-Salaam. Upembuzi yakinifu Kamati imearifiwa unatarajiwa kukamilika Agosti 2009 unaofanywa na Kampuni ya *BNSF* (*Burling Norton Santa Fe*). Serikali vile vile ina mikakati ya kuendeleza *North - South Corridor* ambayo itagusa eneo la ukanda wa Shaba na kuiingiza kwenye mfumo wa *TAZARA* kutokea Lubumbashi. Mtandao huu utagusa Malawi, Zimbabwe na Msumbiji. Uko utaratibu wa kuboresha *Central Corridor* na hatimaye Bandari ya Tanga ikiunganishwa na reli kutoka Tanga hadi Kisumu. *Programme* hii ni mgodi wa hadhina kwa uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Miradi hii itagharimu fedha nyingi hivyo Serikali iendeleze jitihada ya kuwasiliana na wafadhili pamoja na watakaogharamia *(financiers)* miradi hii ikizingatia kuepukana na urasimu pamoja na gharama nyingine za uwekezaji katika kutekeleza miradi hii *(cost of doing business).* Mikakati ya kupata dola za Marekani milioni 44 kutoka *IFC* iendelezwe wakati huo huo Serikali itafute dola za Marekani milioni 43 kutokana na vyanzo vyetu ili Benki ya Dunia ikamilishe ahadi yake ya kutoa mkopo wa dola za Marekani milioni 40 ili kuboresha reli ya kati. Mradi huu utakapokamilika utachangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi wetu. Hivi sasa mzigo unaopitishwa na reli ni asilimia 7 tu na usafiri wa barabara ni asilimia 93. Kwa kawaida usafirishaji mizigo kwa kutumia reli unatakiwa uwe mkubwa zaidi kuliko barabara. Serikali inabidi ijidhatiti kubadilisha hali na mwelekeo huu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikia maamuzi ya kutoa kipaumbele kwenye Sekta ya Kilimo, tukizingatia kukumbuka na kurejea historia yaa kuendeleza kilimo nchini, maamuzi haya tumeyatoa muda mrefu tokea enzi za Baba wa Taifa. Bajeti ya mwaka ujao imejengwa kwa Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza. Kauli Mbiu ya Kilimo kwanza, ni nzuri na iwe ni chombo cha kisera cha kuchochea maeneo ya kuleta maendeleo. Kauli Mbiu hii sasa imetoa jibu kwa swali lililokuwa linaulizwa na Kamati, la kwanini mchango wa Kilimo katika Pato la Taifa umekuwa ukipitwa na sekta ya ya Huduma kwa miaka minne mfululizo? Je, uwezo wa kuzalisha katika sekta ya Kilimo tumeutumia ipasavyo kwa viwango vyake vyote? Tumefikia ukomo?

Mheshimiwa Spika, hoja inayojengwa hivi sasa kuwa mchango wa kilimo kupitwa na sekta ya huduma katika kuchangia pato la taifa eti ni dalili za kukua kwa uchumi wetu haziendani na nadharia za uchumi (*economic theories*) na maendeleo ya kilimo chetu nchini.

Hata kwa kuangalia tu historia ya uchumi *(economic history)* hailingani na mwenendo wetu ukilinganisha na zile nchi nyingine zilizoendelea na hatimaye kuchangiwa pato la taifa kwa uhaba na Sekta ya Kilimo katika uchumi. Hatujajitosheleza vizuri kwa chakula, hatujaweza kusindika mazao yetu ya kilimo kwa upeo wote, hatuna viwanda vidogovidogo vya kuhudumia sekta ya kilimo ipasavyo, bado hatujajidhatiti katika upatikanaji wa pembejeo muhimu kama vile maji, mbolea, madawa, mbegu bora na hata zana za kilimo, tunahitaji kuboresha zaidi huduma za masoko na usafiri n.k. Kwa changamoto zote hizi, kupitwa kwa uchangiaji wa sekta ya Kilimo na Sekta nyingine katika uchangiaji wa pato la Taifa si dalili ya Uchumi kuendelea bali, ni dalili kudharau kilimo *(neglect)*, udhaifu katika utendaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa programu na miradi ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa bado mazingira ya uwekezaji katika kilimo hususan, kile cha chakula bado hakijapata vivutio vya kutosha. Hatua ya Serikali ya kusamehe ada ya mwaka ya Leseni kwa matrekta ya kilimo na ile ya kusamehe ushuru wa forodha kwenye majembe ya mkono haitoshi. Ipo haja ya Serikali kubuni vivutio vipana zaidi hasa kwenye eneo la kodi ili kuvutia wawekezaji na kuongeza ari ya wakulima. Kama mfano tu, uamuzi wa Serikali wa kununua matrekta madogo kwa wakulima *(Power tillers)*, si lazima wanunue au wakope kutokana na udhaifu wa kutotimiza masharti has aya kibenki, inawezekana kabisa Serikali ikaanzisha utaratibu wa kuwawezesha Wakulima hawa kukodisha zana hizi, kwa kulipa kwa fedha taslimu au hata kwa kulipa kwa mazao watakayozalisha (*payment in kind*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya maamuzi ya kukopa fedha za ndani ili kufidia pengo la Bajeti. Hata hivyo, Kamati imetahadharisha kuwa kukopa huku kwa Serikali kusifikie hatua ya kuwatoa nje Sekta binafsi (*crowding out*) katika kufikia Mikopo ya Soko la ndani.

Hali hii inaweza kusukuma riba kuwa za viwango vya juu na hivyo kutokuvumilika kiuchumi. Ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali haitokopa kutoka Benki Kuu ili kuepukana na matatizo ya mfumko wa bei au ujazi wa fedha usiohimilika kutokana na uchapichaji wa fedha. Ipo haja ya Serikali kuona kuwa fedha zinazopatikana kutokana na mikopo hii zinaelekezwa kwenye matumizi ya uzalishaji wa moja kwa moja – (*directly productive sectors*). Kwa maana hii Serikali itakopa kwa kuendeleza uzalishaji na hatimaye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, bado Kamati haijaridhishwa na azima ya Serikali ya kukopa ili kulipia madeni yaliyoiva au kulipia matumizi ya kawaida. Serikali ikope ndani lakini igharamie matumizi ya uzalishaji na uwekezaji, hasa katika barabara tukizingatia kuwa, kutokna na msukosuko wa kiuchumi duniani utaratibu wa kutegemea *foreign bonds* kujenga barabara umekuwa ni mgumu kutokana na viwango vikubwa vya riba na masharti magumu ya *credit ratings* kimataifa. Serikali ikope ndani, lakini igharamie matumizi ya uzalishaji na uwekezaji. Serikali ikope iwekeze, isikope kwa matumizi ya kawaida (*borrow internally but finance productive expenditure, Borrow for investments not for consumption).*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Mipango ya kunusuru uchumi iliyotangazwa na Serikali itagharimu Shilingi trilioni 1.7 ili kusaidia uchumi wetu. Kamati inapongeza Serikali kwa kuonyesha mipango ya vyanzo vya fedha vya kugharimia athari za kupunguza makali ya msukosuko na kulinda uwekezaji katika mpango. Kamati inatambua kuwa mipango hii si mbadala wa Bajeti ya Serikali. Huu ni mpango wa kulinda ajira, kujitosheleza kwa chakula, kulinda uwekezaji kwenye Sekta muhimu na kinga ya makali ya maisha kwa wananchi wa viapato vya chini (*safety nets*). Kamati inaishauri Serikali kwanza: kuwa makini mipango hii, vitendo sasa vifuate maneno ama sivyo uchumi wetu utayumba. Hili ni jukumu kubwa la Serikali, Bunge na Wananchi wote wa Tanzania kwa maslahi ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili kwa vile fedha hizo ziko kwenye Bajeti ya Serikali kinachohitajika ni Uimara wa Menejimenti na Uendeshaji wa mipango tajwa kwa vitendo, tija, ufanisi na hatimae matokeo. Aidha, jitahada zifanywe kidharura ili kupata fedha za kugharmia baadhi ya hatua zilizoonyeshwa. Hatua nyingine zinahitaji kutekelezwa sasa na si za muda mrefu. Kwa mfano tu, Sh.21.9 bilioni zilizotengwa kufidia hasara waliyopata wanunuzi wa mazao, musimu wa mwaka 2008/2009 kama vile Vyama vya Ushirika, Makampuni na sekta binafsi ni fedha zinazohitajika sasa hivi. Msimu wa mavuno hausubiri kupatikana kwa fedha. Hili ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, yapo baadhi ya maoni yanayoulizia utegemezi wa Bajeti hii wa misaada kutoka nje. Katika matumizi ya Maendeleo Shilingi trilioni 1.9 au asilimia 65.7 itatokana na fedha za Wahisani. Aidha, katika jumla ya mapato yote ya Bajeti ya Sh.Trilioni 9.513 misaada na mikopo ya nje ni Sh.Trilion 3.181 au asilimia 33.4.

Kamati inaishauri Serikali kufuatilia upatikanaji wa fedha hizi kwa nguvu na jitihada kubwa. Kwanza, ni kwa sababu nchi tajiri za Ulaya na Marekeni ndizo chanzo cha msukosuko huu wa uchumi na zimetufikisha hapa tulipo. Pili, Benki ya Dunia na Shirika la fedha Duniani (IMF), wameshaonyesha nia ya kusaidia juhudi zetu za kunusuru Uchumi. IMF wako tayari kutoa fedha kupitia (*oxogenous shock facility*), Benki ya Dunia ipo tayari kutoa Shilingi 46 bilioni kwa ajili ya Mfuko wa mbolea na shilingi 40 bilioni kwa Uwekezaji katika Reli na kadhalika.) na tatu, ni kwa sababu kwa kipindi cha Julai, hadi Machi 2009, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilifikia shilingi 867.6 bilioni sawa na asilimia 59 tu ya Makadirio ya Mwaka 2008/09. Upatikanaji wa fedha za nje ukishirikishwa na jitahada za kuamsha fedha kutoka vyanzo vyetu vya ndani, vitasaidia sana katika kunusuru uchumi wetu katika kipindi hiki cha msukosuko.

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile inaishauri Serikali kuwa, mpango wa kunusuru uchumi ni wa dharura, maanake huu ni mpango wa kunusuru. Hata kama si mpango mbadala wa Bajeti ya 2009/2010, ni vyema Serikali itambue kuwa utaratibu wa kunusuru (*rescue or bail out package*) sio wa hali ya kawaida kwa mantiki kwamba, hauwezi kufuata utaratibu wa kawaida wa Kibajeti, hususan katika mtiririko wa rasilimali. Hatua za *bail out programme* zizingatiwe ili kuendana na dhana nzima ya kunusuru uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaunga mkono maamuzi ya Serikali yaliyotokana na wito au Kauli Mbiu ya Kilimo kwanza. Katika kipindi cha mwaka 2009/10, Kilimo kimetengewa Shilingi bilioni 666.9. Kamati inaishauri Serikali kupitia kwa kina mfumo wa matumizi ya fedha hizi katika Kilimo ili kuhakikisha kuwa, fedha hizi zinaelekezwa kwa wakulima moja kwa moja ili ziwe na matokeo (*impact*) katika kuongeza mazao hasa ya chakula. Ni vyema kama mfano tu, Serikali ikaangalia Kitabu cha Matumizi kwa Bajeti ya Kilimo katika eneo la umwagiliaji na kutathmini ni asilimia ngapi ya fedha zilizotengwa zinaenda moja kwa moja kwenye kuboresha miundombinu ya umwagiliaji.

Hili ni eneo moja tu, na Kamati inaiachia Serikali zoezi hili kama changamoto. Kamati imeishauri Serikali kwa vile sasa imeamua kutoa Shilingi 20 bilioni kusaidia Benki ya Raslimali kugharimia Kilimo na kwa vile inatoa Shilingi 40 bilioni kwa utaratibu wa (*lease financing*) kwa riba nafuu kwa ajili ya zana na vifaa vya kilimo, iwe ndio fursa ya kuwapatia nafasi Wakulima wa ndani Watanzania nao sasa kujiingiza katika Kilimo cha uhakika. Ni wakati sasa wa kutenga maeneo na yagawanywe kwa Watanzania wote pamoja na Wabunge ili kujiingiza kikamilifu katika Kilimo cha mashamba makubwa ya kuzalisha chakula. Utaratibu huu utaleta ufanisi na tija kubwa.

. Mheshimiwa Spika, kwa vile nia ni kuendeleza kilimo – mazao na viwanda vidogo vya kusindika chakula, Serikali haina budi kubuni mikakati ya kupunguza riba ya mikopo ili kuwafanya Watanzania wengi kupata huduma hii. Kilimo hakiwezi kuendelea bila mikopo. Uzoefu unaonyesha kuwa, wananchi wenye kipato cha chini wanaoweka amana ndogondogo na kwa muda mfupi ndio wanaotozwa riba kubwa wakati wa kulipia mikopo yao. Hawa ndio wengi na ndio wateja wasiofahamika. Kamati inaishauri Serikali kuangalia Sera za kifedha na kuzihuisha ili zisaidie upatikanaji wa mikopo kwa Wananchi wa vipato vya chini.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sheria ya Karadha, Sheria ya Mikopo ya Nyumba, Mifuko ya Dhamana na kadhalika hazitasaidia ikiwa hazitawalenga wazalishaji walio wengi. Kipindi cha 2009 viwango vya riba vimefikia kati ya asilimia 15.0 hadi 22.0 Amana za muda mrefu (*longtime deposits*) zinatozwa riba ya 6.79. Mwezi Machi, 2009 (*negotiated deposit rate*s) zilikuwa ni asilimia 10.99 na (*negotiated lending rates*) zilikuwa asilimia 12.85. Viwango hivi ni vya waweka amana wakubwa, ambao ni wachache. Kwa utaratibu huu Serikali ina changamoto kubwa ya kuanzisha na kuhamasisha utaratibu wa kuwaingizia wengi katika mkondo wa kupata mikopo (*accessing credit*).

Mheshimiwa Spika, wigo wa kodi (*tax base*), Kamati imetambua azma ya Serikali ya kupanua wigo wa Kodi kama mkakati wa kuongeza makusanyo ya mapato. Hili ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa katika kipindi hiki, bado ulipaji kodi unagusa sehemu ndogo ya uchumi na hivyo kusababisha mapato madogo. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia yale maeneo ambayo ingawaje yana mchango mkubwa katika Pato la Taifa, hayaingizwi kwenye mfumo wa kifedha pamoja mchango wa sekta isiyo rasmi, inayokua kwa kasi. Eneo hili linaweza kuongeza mapato kwa asilimia 30 ambacho ni kiwango

kikubwa. Eneo lingine linalohitaji jitahada za Serikali ni lile la kuboresha taratibu za kukusanya mapato yasiyo ya Kodi (*non tax revenue*), linalosimamiwa kwa karibu na Wizara ya Fedha na Uchumi. Eneo hili bado ni dhaifu na halijawekewa mikakati thabiti. Ipo haja ya Serikali kuona ni jinsi gani maeneo ya Maliasili – uvuvi, misitu, mbao, asali n.k. yanaweza kutozwa kodi kwa tija. Hili litaongeza mapato ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika bajeti hii imejumuisha shilingi milioni 138,052 zitokane na vyanzo vya Halmashauri. Kamati imeishauri Serikali kuchukua tahadhari kuwa vyanzo hivi visihusishe marudio ya kodi na tozo zenye kero (*nuisance fees and taxes*) ambazo zilifutwa awali na Serikali. Kurudishwa kwa kodi na tozo hizi kutavunja ari na motisha kwa wananchi ambao sasa wanategemewa sana katika mpango mzima kunusuru uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali inatarajia kuamsha takribani shilingi trilioni 6.33 kutoka vyanzo vya ndani, hiki ni kiwango kikubwa. Ili kupanua wigo wa kodi Kamati imeishauri Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka hisa zake za baadhi ya Mashirika katika soko la hisa ili iweze kuongeza mapato ya ndani na wananchi wengi waweze kumiliki uchumi ikiwa ni pamoja na kuongeza "*Capitalization*" ya soko la Hisa la Dar es Salam.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wananchi, Kamati inaipongeza Serikali kwa mkakati wake wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Mkakati huu ndio njia pekee ya kuwawezesha wananchi kupata ajira na mapato *(employment creation and income generation)* Mfuko wa dhamana kwa Benki za NMB na *CRDB* ulitoa mikopo ya shilingi bilioni 31 kwa Wajasiriamali 65,508, *SACCOS* 192 na Vikundi 86. Mwananchi *Empowerment Fund*, SELF na kadhalika. Pia imechangia katika lengo hilo la uwezeshaji. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali katika eneo hili ihakikishe kuwa inaweka utaratibu mzuri wa kuwafikia walengwa wenye hadhi ya kuwezeshwa, wale wananchi ambao vipato vyao ni vya chini. Hawa wakifikiwa matokeo (*impact*) yake itakuwa ni kubwa. Suala zima hapa ni lile la *"Targetting"*, kuwalenga wale walengwa. Kupunguzwa kwa kiwango cha Kodi ya Ongezeko la thamani kutoka asilimia 20 ya mauzo hadi asilimia 18, ni kitendo cha kuipongeza Serikali, kwani zoezi hili litawagusa wananchi walio wengi wanaopata bidhaa zao za msingi kwa kununua.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengi mazuri yaliyoainishwa katika Mipango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010. Kwa mfano lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; kuboresha sera za ununuzi wa Umma; kudhibiti hali ya kutoridhisha ya usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa; kuboresha udhibiti na usimamizi wa Fedha za Umma; kutoa kipaumbele uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo kwa kuhusisha sekta binafsi; kuvutia wawekezaji wakubwa katika Kilimo cha mashamba makubwa ya chakula, kukamilisha Sera ya Taifa ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi (*PPP*) n.k. Kamati inaishauri Serikali kuwa, pamoja na uzuri wake maeneo kama haya yana hatari ya kupambana na adui mmoja, adui Urasimu. Athari kubwa ya urasimu ni tatizo la kutokutoa maamuzi kwa wakati kwa wahusika. Hili lisiporekebishwa Kamati inatabiri ugumu wa kunusuru Uchumi wa Nchi unaopita kipindi kigumu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha ukuaji katika Sekta ya umeme na gesi umeshuka toka asilimia 10.9 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 5.4 mwaka 2009. Sekta hii ni muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi na mahitaji ya umeme yanaongezeka kwa MW 70 kila mwaka. Hatua zinazochukuliwa na Serikali kukabiliana na changamoto hizi zinaonekana.

Uamuzi wa kukamilisha mradi wa kusambaza umeme Mtwara na kuunganisha hadi Tandahimba upongezwe. Fedha za *MDRI* zikitumika vyema maeneo mengi vijijini yatapata nishati hii. Moja ya ushauri wa Kamati kwa Serikali ni kusisitiza suala zima la ukarabati (*maintanace*) wa mitambo iliyopo kwa kutumia vipuri vyevye viwango bora ili kufikia uwezo uliopo wa kuzalisha umeme katika gridi ya Taifa ( *at full capacity utilization).* Hii itawezesha kuzalisha zaidi ya MW 1000, kwa kutumia tu utaratibu wa ukarabati mzuri ikilinganishwa na MW 500-600 zinazozalishwa sasa, ili kupunguza uhaba wa huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati imeishauri Serikali kuwa kama imepania kuendeleza matumizi ya nishati mbadala ya umeme wa jua, upepo na gesi asili, ni lazima uwepo mkakati wa maksudi wa kuvutia na kuwezesha matumizi ya vifaa vinavyotumika na vyanzo hivi. Moja ya hatua ni ya kifedha kwa maana yakuondoa kodi au kutoa ruzuku kwenye vifaa husika, ili wengi wa wananchi wajiingize katika matumizi ya nishati mbadala. Kamati imependekeza ushauri huu kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, hakuna nchi yeyote inayoendelea bila ya msukumo katika uwekezaji (*investment drive*). Eneo hili bado halijaangaliwa kwa makini (*seriously*). Serikali haina budi kutumia eneo hili kama fursa itokanayo na msukosuko wa uchumi duniani kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji. Katika nchi za Afrika Mashariki, Tanzania tunachukua nafsi ya 3 au ya 4 katika kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Taarifa ya (*Doing Business* 2009) imeonyesha Tanzania imerudi nyuma katika kuboresha mazingira ya uwekezaji. Maeneo yanayolalamikiwa ni urasimu na mlolongo mrefu katika kutoa vibali vya ujenzi, kusajili mali, biashara na Kampuni, upatikanaji wa ardhi n.k. Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa karibu eneo hili. Kamati inatambua kuwa, hata kuchelewa kwa kukamilishwa kwa sera ya (*Public Private Partnership,*) kuwa ni moja ya sababu ya kudumaza msukumo wa uwekezaji nchini. Katika kipindi hiki *change of atitudes* na *right mind set* ni muhimu vikaongoza *commitiment* ya kuendeleza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kujikita katika maeneo machache (sita) ya vipaumbele. Kamati imefarijika kuwa sekta ya Huduma za Jamii zimetengewa fedha za kutosha. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kuongeza jitihada za kuboresha huduma zinazoendana na Sekta hizi hususan ile inayohusisha upungufu wa Waalimu na Wauguzi. Kamati inachelea tusijikite zaidi kwenye wingi (*quantity*), badala ya ubora (*quality),* na mkakati wa Serikali wa kuongeza Walimu,

Wauguzi, ujenzi wa maabara, ujenzi wa Nyumba za Walimu, wauguzi vijijini uendelezwe.

Mheshimiwa Spika, mwishowe kwa vile Serikali imeanza kazi ya kuandaa awamu ya pili ya MKUKUTA unaotarajiwa kutekelezwa Julai 1, 2010, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu wa kuwahusisha Wabunge kikamilifu ili zoezi zima liwe na tija na ufanisi. Ni vyema matokeo ya tathmini ya awamu ya kwanza ya MKUKUTA yakajadiliwa ili kuwa na *input* ya kuboresha programu ya pili ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha taarifa yangu napenda kwanza kuwatambulisha Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga , Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence B. Liamba, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Felix Mrema,Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Richard Ndassa , Mheshimiwa Dr. Omary Nibuka Mzeru, Mheshimiwa Murad Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe binafsi kwanza, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu.

Pia kukushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii, kufanyakazi ya kuchambua Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008; na Malengo ya Uchumi katika kipindi cha muda wa kati (2009/2010-2010/2012), Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, nawashukuru sana.

Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Waziri, Mheshimiwa, Jeremiah Solomon Sumari, na Mheshimiwa, Omar Yusuf Mzee, Katibu Mkuu na wataalam waliotusaidia sana katika kuchambua Bajeti ya Serikali. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Lawrence Robert Makigi kwa kazi nzito katika kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na kuandaa maoni ya Kamati kwa wakati unaotakiwa.

Nawashukuru Waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwasilisha taarifa na maoni yaliyomo sasa kwa mujibu wa utaratibu wetu naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani na si mwingine ni Kiongozi mwenyewe wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Kifungu cha 99(7) toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa katika kutayarisha bajeti hii, wakiongozwa na Dr.Wilbrod Slaa (Mb.), Naibu Kiongozi wa Upinzani waliofanikisha hadi kuniwezesha kusimama mbele yenu kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kambi ya Upinzani, kutokana na hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi tarehe 11.06.09.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Upinzani na Wabunge wote kwa ujumla wao, kwa pamoja tuna wajibu wa kushirikiana katika kuwatumikia Watanzania kwa lengo kuu la kuwaondolea umasikini uliokithiri, maradhi na ujinga pamoja na kujenga Utaifa wetu wa dhati. Mwenyezi Mungu aziweke pamoja nia zetu na kuzibariki katika kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kukushukuru wewe, naibu Spika, wenyeviti wa Bunge na watendaji wa Ofisi yako, wakiongozwa na Katibu wa Bunge, kwa kutupatia fursa mbali mbali sisi Wabunge kujifunza shughuli za Mabunge ya wenzetu jinsi ya kuwahudumia vyema wadau ambao ni wananchi na wapiga kura kwa kusimamia vyema utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Wawi kwa kuendelea kuniunga mkono na kwa juhudi zao za kujitafutia maisha licha ya vikwazo vikubwa sana na ukiritimba wa kuuza mazao yao ya karafuu. Kama wananchi wa Wawi na Wazanzibar kwa ujumla wangeliruhusiwa kuuza karafuu zao bila pingamizi, wao wenyewe wangepunguza umaskini wao kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Fedha Mhe. Mustafa Mkullo (Mb), Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake, pamoja na Wakuu wa vitengo na asasi zilizo chini yao kwa kazi nzito ya maandalizi ya Bajeti hii. Nawashukuru sana na sasa naomba wasikilize uchambuzi wa Kambi ya Upinzani. Kambi ya Upinzani inafanya uchambuzi wake ikiamini kuwa Waziri atakuja kutoa ufafanuzi zaidi katika baadhi ya maeneo kwa kadiri tutakavyoainisha. Uchambuzi wetu nitauelezea baadae kwa kifupi na kwa kirefu utaelezewa na Mawaziri Vivuli wa Wizara mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ni zaidi ya urari wa mapato na matumizi ya Serikali. Bajeti ni tamko la kisera lenye lengo mahsusi katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi. Hivyo maoni haya ya Kambi ya Upinzani yana lengo la kuonesha mapungufu ya Mpango wa Serikali na kutoa sera na mikakati mbadala pale inapowezekana ili kulinusuru Taifa letu. Tunafahamu kwamba Bajeti ya Mwaka huu inakuja wakati mgumu sana kiuchumi katika Taifa. Hivyo, tutajielekeza zaidi katika jinsi ya kuongeza uzalishaji wa ndani ili kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Malengo ya Uchumi, kila mwaka, Serikali inaeleza katika hotuba ya bajeti kuwa Misingi na shabaha ya Bajeti imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ambayo inalenga kuwa Tanzania iwe ni nchi yenye kiwango cha kati cha mapato (*middle income country)* na hali bora ya maisha kwa wananchi; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005; MKUKUTA; Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania (*Tanzania Mini Tiger Plan 2020*); na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Hata hivyo Waziri hafanyi uchambuzi wa kina kuonyesha jinsi sera za bajeti na matumizi ya Serikali yanatekeleza mikakati hiyo, mafanikio yaliyofikiwa, vikwazo vilivyopo na vinavyokabiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ilibuniwa kwa kuzingatia maendeleo makubwa ya uchumi ya nchi za Kusini Mashariki ya Asia kama vile Malaysia na hususan ukuaji wa sekta ya viwanda, uuzaji wa bidhaa za viwanda nchi za nje na ongezeko kubwa la ajira katika sekta rasmi lililosaidia kupunguza umaskini kwa kasi kubwa. Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ni kuhakikisha kuwa ifikapo 2025, Tanzania itakuwa na uchumi unaotegemea sekta nyingi na ulioendelea kwa kuwa na wastani wa viwanda vingi, uchumi mpana ulio tulivu (*macroeconomic stability),* miundombinu imara na Pato la Taifa linakua kwa asilimia 8 au zaidi. Tanzania ya 2025 itakuwa inamudu ushindani wa Kikanda na Kimataifa kwa kuwa na nguvukazi yenye elimu na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, kigezo muhimu cha kupima kama malengo ya Dira ya Taifa yanafikiwa ni ukuaji wa Pato la Taifa na mabadiliko ya mfumo wa uchumi na hasa ukuaji wa sekta ya viwanda na ongezeko la ajira katika sekta hiii. Wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa miaka minane iliyopita ni asilimia 7, lakini mchango wa sekta ya viwanda bado ni mdogo sana. Viwanda vilichangia asilimia 9.4 ya pato la Taifa mwaka 2008 ukilinganisha na asilimia 8.5 mwaka 2000. Katika Nchi za Kusini Mashariki ya Asia, sekta ya viwanda inachangia asilimia 25-30 ya Pato la Taifa. Katika miaka 4 iliyopita uuzaji wa bidhaa za viwanda umeongezeka kwa kasi kubwa lakini toka kiasi kidogo.

Mwaka 2008 thamani ya bidhaa za viwanda zilizouzwa nje (dola milioni 662.3) zilizidi bidhaa asilia (dola milioni 418.4). Katika nchi yenye nguvu kazi ya zaidi ya watu milioni 20, wananchi walioajiriwa katika sekta rasmi ya viwanda mwaka 2008 ni 92,015 tu. Lengo muhimu la kubadilisha mfumo wa uchumi kwa kuongeza ajira viwandani halijafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini unalenga kufanikisha kufikia malengo ya milenia. Hata hivyo utekelezaji wa MKUKUTA umesuasua kwa sababu gharama za mkakati hazikukadiriwa mapema. Ukadiriaji wa gharama za MKUKUTA katika baadhi ya sekta muhimu ulikamilika mwishoni wa mwaka 2006 na gharama zake zikabainika kuwa ni kubwa mno kuliko uwezo wa Serikali kwa hiyo MKUKUTA hautekelezeki. Kwa mfano gharama za kutekeleza MKUKUTA katika sekta ya nishati ilikadiriwa kuwa wastani wa dola milioni 911 kwa mwaka kati ya 2006/7 mpaka 2009/10. Sekta ya kilimo ilikuwa inahitaji wastani wa dola milioni 300 kwa mwaka. Sekta ya afya ilihitaji wastani wa dola milioni 476 kwa mwaka. Sekta ya barabara ilihitaji wastani wa dola milioni 922 kwa mwaka. Sekta nne za nishati, kilimo, afya na barabara zilikadiriwa kuhitaji wastani wa dola milioni 2,609 kwa mwaka. Mahitaji haya ya sekta 4 ni zaidi ya asilimia 70 ya matumizi yote ya Serikali ya mwaka 2006/07. MKUKUTA haukutekelezwa kama ipasavyo kwa sababu gharama za mpango hazikukadiriwa mapema, na ukadiriaji ulipomalizika gharama zilikuwa kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, Mwaka huu wa bajeti ni wa mwisho wa utekelezaji wa MKUKUTA. Waziri kaeleza kwamba Serikali inaandaa MKUKUTA namba II. MKUKUTA wa kwanza haujafanyiwa tathmini ya kina ili kujifunza kutoka mapungufu yaliyojitokeza. Ni wazi MKUKUTA wa pili hautakamilika na kuanza kutekelezwa mwaka wa bajeti wa 2010/2011. Ikiwa Serikali ina lengo thabiti la kuwa na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini unaotekelezeka inastahili kujipa muda kutathmini MKUKUTA na kushirikisha wadau wote katika kuandaa mpango mbadala wa kukuza uchumi kuongeza ajira za uhakika na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Maendeleo ya Milenia yamekubaliwa na Jumuia ya Kimataifa yawe dira ya mipango ya maendeleo ya nchi maskini kama Tanzania. Malengo halisi yako saba na yanakusudia ifikapo mwaka 2015:-

(a)Kutokomeza umasikini uliokithiri na njaa. Kupunguza kwa asilimia hamsini idadi ya watu maskini ambao kipato chao ni chini ya dola moja kwa siku na kupunguza kwa asilimia hamsini idadi ya watu wanaokumbwa na njaa.

(b)Elimu ya Msingi kwa wote kuhakikisha watoto wote wa kike na wa kiume wanahitimu Elimu ya Shule ya Msingi.

(c)Usawa wa kijinsia na fursa sawa kwa wanawake kuondoa tofauti ya uwiano wa wasichana na wavulana katika Elimu ya Msingi ifikapo mwaka 2005, na katika ngazi zote za elimu ifikapo 2015.

(d) Kupunguza vifo vya watoto wachanga. Kupunguza kwa theluthi mbli vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano.

(e) Upatikanaji wa huduma bora za uzazi.

(f) Kupambana na Ukimwi, Malaria na magonjwa mengine kuzuia kabisa na kuanza kupunguza maambukizo mapya ya Ukimwi, kuzuia kabisa na kuanza kupunguza milikkkp;uko ya malaria na magonjwa mengine hatari.

(g) Kulinda mazingira yetu kujumuisha misingi yote ya maendelkeo endelevu kati ka Sera na programiu za kila nchi, kuzuia kupotevu wa raslimali ya m azingira.

(h) Lengo la nane linahimiza ushirikiano wa kimataifa kuziwezesha nchi maskini kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Bajeti za Kaya wa mwaka 2007 (2007 *Household Budget Survey*- HBS) unaonyesha kwamba umaskini umepungua kidogo sana toka asilimia 38.6 mwaka 1990, asilimia 35.7 mwaka 2001 mpaka asilimia 33.3 mwaka 2007. Kwa kuwa idadi ya Watanzania inaongezeka kwa asilimia 2.9 kila mwaka. Idadi ya watu maskini imeongezeka kwa milioni moja na nusu toka watu milioni 11.4 mwaka 2001 na kufikia watu milioni 12.9 mwaka 2007. Izingatiwe kuwa kigezo kilichotumiwa na *HBS 2007* cha mtu mzima kutohesabiwa kuwa siyo maskini ni kutumia shilingi 641/- au zaidi kwa siku ukiwa Dar es Salaam, shilingi 532/- au zaidi kwa siku ukiwa katika miji mingine na shilingi 469/-au zaidi kwa siku ukiwa vijijini. Ni wazi kigezo hiki ni cha chini mno na bado idadi ya watu maskini imeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Uchumi alipowasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2008 alieleza kuwa Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 7.4. Kwa kipindi cha miaka minane 2001-08, Pato la Taifa limekua kwa wastani wa asilimia 7.1 kwa mwaka. Ikiwa ongezeko la watu ni asilimia 2.9, wastani wa pato la kila mwananchi limeongezeka kwa wastani wa asilimia 4.2 kwa mwaka.

Kutopungua kwa umaskini kwa kasi kunaashiria kwamba uchumi wa Tanzania haukui kwa wastani wa asilimia 7.1 kwa mwaka kama takwimu za Serikali zinavyoeleza.

Mheshimiwa Spika, kigezo kilichokubaliwa Kimataifa kuwa matumizi ya chini kabisa kwa mtu mzima asihesabiwe kuwa ni maskini wa kutupwa ni dola moja kwa siku. Benki ya Dunia inakadiria kwa kutumia kipimo hiki, umaskini Tanzania umeongezeka toka asilimia 73 ya Watanzania wote mwaka 1990 mpaka kufikia asilimia 89 mwaka 2000. Kwa kutumia kigezo hiki cha Kimataifa na takwimu za uchunguzi wa bajeti za kaya wa 2007, zaidi ya Watanzania 90 katika kila Watanzania 100 ni maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Spika hali hii inatisha, hatuwezi kuwa na mshikamano wa kweli wa Kitaifa ikiwa ukuaji wa uchumi unawanufaisha watu wachache na kuwaacha zaidi ya

Watanzania milioni 36 wakiwa maskini wa kutupwa. Kwa Watanzania walio wengi kauli mbiu ya Maisha Bora kwa Kila Mtanzani ni kitendawili cha kejeli kwani maisha yao ni ya dhiki kila kukicha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo ya milenia ni pamoja na kupunguza kwa nusu asilimia ya Watanzania wenye njaa. Watanzania wenye lishe duni na utapiamlo wameongezeka toka asilimia 28 ya Watanzania wote mwaka 1990 na kufikia asilimia 41 mwaka 1995 na kupungua kiasi kufikia asilimia 35 mwaka 2007. Wakati Chama Tawala kinaendelea kupongezana kwa kuonyesheana vidole gumba, Watanzania wanaolala na njaa karibuni kila siku iendayo kwa Mungu wameongezeka toka milioni 7.4 mwaka 1990 na kufikia milioni 14.4 mwaka 2007. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza umaskini tunahitaji kuongeza ajira bora na za uhakika (*decent work*). Benki ya Dunia inakadiria kuwa Watanzania wengi mno wanategemea ajira zisizokuwa na uhakika. Watu wenye ajira zenye mashaka wamepungua kidogo toka asilimia 92 ya Watanzania wote wenye umri wa kuajiriwa mwaka 2000 na kufikia asilimia 88 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, lengo la milenia ambalo tunaweza kulifikia ni elimu ya msingi kwa wote na usawa wa kijinsia katika Elimu ya Msingi. Hata hivyo ni muhimu kuboresha Elimu ya Msingi ili wanaoanza shule wamalize kwa sababu elimu wanayopata in manufaa. Bila kuiboresha Elimu ya Msingi tunaweza kurudi nyuma kama ilivyotokea miaka ya themanini kuhusiana na elimu ya *UPE.*

Mheshimiwa Spika, lengo la milenia kuhusu vifo vya watoto wadogo ni kuvipunguza kwa theluthi mbili kati ya mwaka 1990 na 2015. Vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua toka 96 kwa watoto 1000 waliozaliwa na kufikia 89 mwaka 2000 na 73 mwaka 2007. Lengo la Milenia ni kupunguza vifo vya watoto wachanga kufikia 32 kwa watoto 1000 ifikapo 2015. Kwa miaka 6 iliyobakia, tukiendelea na uzoefu tulionao, lengo hili haliwezi kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, vifo vingi vya watoto wachanga vinatokea kwa watoto wenye umri wa chini ya mwezi mmoja. Kila mwaka watoto wanaozaliwa (*newborn)* 51000 wanafariki kabla ya kufikisha mwezi mmoja. Watoto wengine 43,000 wanazaliwa njiti (*still born).* Vifo vya watoto wa chini ya mwezi mmoja ni asilimia 29 ya vifo vya watoto wote wa chini ya umri wa miaka 5. Utafiti wa Madaktari wa watoto unaonyesha kuwa theluthi mbili ya vifo vya watoto - sawa na watoto 34,000 vinaweza kuepukika ikiwa huduma za msingi za afya zitawafikia kina mama wajawazito na watoto wao. *(Makofi)*

Serikali inabidi iweke mkakati na fedha kuwahudumia kina mama wajawazito na watoto wachanga. Vifo vya uzazi havijapungua bali vinaongezeka. Kuna vifo vya uzazi 578 katika kila wajawazito 100,000 wanapojifungua. Wataalam wa Benki ya Dunia wanakadiria kuwa katika mwaka 2007 kulikuwa na vifo 950 kwa kila kina mama laki moja waliojifungua

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo unaoonekana katika uchunguzi wa Bajeti za Kaya 2007, na takwimu za Benki ya Dunia, Tanzania, pamoja na kupata misaada mingi toka nje, haitafikia malengo ya milenia ya kupunguza umaskini na kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunahitaji tutafakari hali halisi tuliyonayo na tubuni sera na mikakati ya pamoja ya kujikwamua toka dimbwi la umaskini. Misingi muhimu ya sera na mikakati hiyo iwe:-

- Kuitumia vizuri mali ya asili ya Tanzania kwa manufaa ya wananchi wote huku tukilinda mazingira yetu.

- Kuwekeza kwenye afya ya watoto wa Tanzania toka wakiwa katika mimba za mama zao kwa kuhakikisha kina mama waja wazito na watoto wachanga wanapata lishe bora.

- Kuwekeza katika elimu ya watoto wa Tanzania toka shule za chekechea na kuendelea. Kuweka msisitizo maalum katika elimu ya hesabu, sayansi na teknolojia.

- Kuwekeza katika kilimo hasa cha chakula kama vile mahindi, mpunga, maharage, jamii ya kunde na mbegu za mafuta kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza masoko ya nje hasa nchi za jirani na hususan Congo,Comoro, Kenya na kadhalika.

- Kuwekeza katika miundombinu ya barabara, umeme, maji na mawasiliano.
- Kuweka mkakati madhubuti wa kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi ya ndani na kuajiri watu wengi kama vile viwanda vya nguo na mavazi, viatu na bidhaa za ngozi, vifaa vya matumizi ya nyumbani na vifaa vya umeme na electroniki.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali inaendelea kutegemea wafadhili wa nje bila ya kuweka mkakati wa kujikwamua toka kuwa nchi tegemezi. Theluthi moja ya matumizi ya Serikali yanategemea mikopo na misaada kutoka nje. Mikopo na misaada ya nje ya shilingi trilioni 3.2 ni zaidi ya matumizi ya shilingi trilioni 2.8. Kimsingi Serikali haitoi fedha yeyote kugharamia matumizi ya maendeleo na inategemea wafadhili kulipia matumizi ya kawaida. Mfumo huu wa kutegemea nje ni aibu kwa Taifa letu hasa ukizingatia kuwa tuna miaka 48 tangu tumejitawala. Walau wahisani wangetusaidia bajeti ya maendeleo na sisi tukaichangia kwa kiasi kikubwa bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaweza kukusanya asilimia 20-25 ya pato la Taifa kama kodi kwa kuondoa misamaha holela ya kodi hasa katika sekta ya madini, kukusanya kodi zinazokwepa katika bidhaa za mali ya asili ikiwa ni pamoja na madini, misitu na samaki. Inakadiriwa kuwa Serikali inapoteza mapato ya dola milioni 50 kila mwaka katika sekta ya dhahabu na dola milioni 58 katika sekta ya misitu.

Takwimu za biashara zinaonyesha kwamba Uchina imeingiza bidhaa za misitu toka Tanzania ambazo ni mara 10 ya mauzo ya bidhaa hizo zilizo katika kumbukumbu ya takwimu za Tanzania. Kwa hiyo Serikali inakusanya asilimia 10 tu ya kodi ya mauzo ya mbao zinazosafirishwa kwenda China. Waziri ameeleza kuwa misamaha ya kodi ni asilimia 3.5 ya pato la Taifa. Ikiwa misamaha ya kodi itapunguzwa mpaka kufikia asilimia 0.5 ya pato la Taifa, ukusanyaji wa kodi utafikia asilimia 20 ya pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kushuhudia Serikali inavyoyaogopa na kuyakumbatia Makampuni yanayochimba madini. Serikali imependekezwa kuondoa msamaha wa Ushuru wa Mafuta ya Petroli kwa mafuta yanayotumiwa na kampuni za madini kwa kufuta Tangazo la Serikali namba 99 la mwaka 2005. Marekebisho haya yanahusu Kampuni za madini zitakazoingia mkataba na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2009. Kwa nini ufutaji wa misamaha hii usiyaguse Makampuni yaliyopo hivi sasa. Serikali inaendelea kulinda mikataba ya kifisadi kwa manufaa ya nani?

Mheshimiwa Spika, Bunge hili liazimie na liitake Serikali katika bajeti hii kuyatekeleza mapendekezo ya Jaji Bomani ya kuiongezea Serikali mapato ikiwa ni pamoja na kufuta misamaha ya kodi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushuru wa mazao ni kero kubwa kwa wakulima inawapunguzia motisha wakulima, inachochea rushwa ya Watendaji wa Vijiji, Kata na Halmashauri. Waziri anapendekeza kupunguza kiwango cha ukomo cha kutoza ushuru wa mazao kutoka asilimia 5 ya bei ya kuuza mazao shambani hadi asilimia 3 ili kupunguza makali ya athari za msukosuko wa kiuchumi duniani kwa wakulima nchini.

Hata hivyo anapendekeza hatua hii ianze kutekelezwa mwaka wa fedha 2010/2011 ili kutoa nafasi kwa Serikali za Mitaa kujiandaa kupata vyanzo mbadala vya mapato. Kwa nini Serikali isufute kabisa ushuru wa mazao hivi sasa, na itumie misaada ya mtikisiko wa uchumi kufidia Halmashauri kwa mwaka mmoja wakati Halmashauri zinajiandaa kutafuta vianzio vingine vya mapato? Badala yake inafidia madeni ya Mabenki na wafanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Misamaha yote ya kodi, asilimia 83% inahusu Makampuni yaliyosajiliwa *T.I.C* na asilimia 17 ni Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali, Taasisi za Dini na Asasi zisizo za Kiserikali na misaada inayotoka kwa wafadhili. Hivyo sehemu kubwa ya misamaha ni ile ambayo Waziri ameendelea kuisamehe na sio hiyo ya kidini na Asasi zisizo za kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa kujali huduma zinazotolewa na Taasisi hizi, pamoja na mapungufu yaliyopo ya baadhi yao kuitumia vibaya fursa hizi, kwani zipo Taasisi zinapata misamaha lakini huduma zake ni ghali kuliko zile zisizopata

misamaha, hata hivyo ni vyema misamaha hii ikaendelea na wale wanatumia vibaya fursa hizi wanyimwe kabisa fursa hii ikiwa wako wanaovunja sheria wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali inakusudia kukopa shilingi trilioni 1.08 katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya mapato ya Serikali na kulipia dhamana zinazoiva. Katika mwaka wa bajeti wa 2008/2009, Serikali iliendeleza sera ya kutokukopa kutoka vyombo vya fedha kugharamia bajeti yake hasa matumizi ya kawaida.

Hata hivyo riba ya Hawala za Hazina (*treasury bills*) za siku 91 mwishoni wa Desemba 2008 ilikuwa asilimia 11.2. Utafiti wa Shirika la Fedha la Kimataifa *IMF* umebaini kuwa mabenki ya nje yaliyomo Tanzania yanakula njama kuhakikisha kuwa wanapata faida kubwa kwa kununua Hawala za Hazina. Kuongezeka kwa ukopaji na mapungufu yaliyopo katika kusimamia soko la Hawala za Hazina kutaongeza gharama za riba kwa Serikali. Wakati serikali inaongeza kukopa na riba inapanda juu Rais Kikwete ameeleza kwamba “Serikali itayakopesha mabenki fedha kwa riba nafuu ya asilimia 2 ili na wao wawakopeshe wafanyabiashara fedha za mitaji ya uendeshaji kwa riba nafuu.” Serikali itakopa na kulipa riba ya asilimia 11 na kuyakopesha mabenki kwa asilimia 2. Benki Kuu haina mamlaka ya kupanga riba kwa wateja wa Benki za Biashara. Mikopo ya Serikali itawaongezea mapato wenye mabenki bila kuwasaidia wafanya biashara wadogo na wa kati kwani mabenki bado inawaona kuwa hawakopesheki.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kufidia Vyama vya Ushirika na Makampuni yaliyonunua mazao ya wakulima na kuyauza kwa hasara. Katika soko huria kuna kupata faida na kupata hasara. Wafanya biashara makini wa mazao hupanga bei zao za kununulia mazao kwa kuzingatia bei walioipata katika *futures markets*. Hata hivyo wengine hawapendi kuchukua tahadhari kwa kutegemea kwamba bei itapanda na kwa hiyo watapata faida kubwa. Bei imeshuka kwa hiyo wamepata hasara.

Je, hakuna wafanya biashara wa mazao waliolipa mikopo waliokopa kwa kujibana. Serikali ina uhakika gani kuwa mikopo hii ilitumiwa vizuri? Mkaguzi na Mdhibiti wa Serikali ayakague Makampuni haya kuthibitisha kuwa hasara waliopata haikutokana na matumizi mabaya ya mikopo. Gharama ya ukaguzi huu ulipiwe na Mabenki yaliyokopesha. La sivyo Serikali inaweza kuliingiza taifa katika *EPA* namba mbili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kusaidia wafanya biashara, makampuni na mabenki yaliyopata hasara. Lakini, hakuna hatua zozote zilizoelezwa za kuwasaidia wafanyakazi waliopoteza ajira na wakulima wanaopata bei mbaya ya mazao isiyorudisha gharama. Hivi sasa wakulima wa pamba hawavuni pamba yao kwa kuwa bei ya pamba ni ya chini sana na hakuna soko la uhakika. Si hotuba ya Rais wala ya Waziri wa Fedha iliyotoa matumaini kuwa walalahoi pia wanakumbukwa na watafidiwa hasara na athari walizozipata kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani lakini matajiri wanafikiriwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kutoa udhamini wa madeni ambayo wakopaji kwa sababu ya msukosuko wa uchumi wa dunia wanapata matatizo kulipa kwa wakati. Madeni hayo yanafikia Shs.270 bilioni.

Kuna hatari ya Serikali kujiingiza katika kudhamini madeni ambayo hatimaye yatabidi yalipwe na Serikali. Serikali inajiongezea mzigo wa madeni yanayoweza kutokea *(Contigent Liabilities).*

Serikali imeamua madeni haya yadhaminiwe kwa miaka miwili na siyo mwaka mmoja ili shughuli za Uchaguzi Mkuu wa 2010 ziwe zimemalizika. Hii itatoa mwanya kwa wanaodhaminiwa madeni wachangie kwenye kampeni na baada ya uchaguzi mzigo wa madeni ubebwe na Serikali. Kuna hatari ya *EPA* nyingine kuzinduliwa. Ukaguzi wa kina wa mahesabu ya Makampuni husika ufanywe na *CAG* kwa gharama za Mabenki yaliyokopesha kabla ya Serikali kuyadhamini Makampuni haya.

Mheshimiwa Spika, Waziri ameeleza kuwa kauli mbiu ya bajeti hii ni Kilimo Kwanza. Hata hivyo Serikali imetenga shilingi bilioni 667 kwa sekta ya kilimo sawa na asilimia 7.0 ya matumizi yote ya Serikali. Mwaka wa fedha wa 2008/2009 sekta ya kilimo ilitengewa shilingi 513 bilioni sawa na asilimia 7.1 ya matumizi yote ya Serikali ya bajeti hiyo.

Kibajeti mchango (*share*) wa matumizi ya sekta ya kilimo umebakia kama bajeti ya mwaka jana. Ubadilishaji wa msamiati toka kilimo ni uti wa mgongo na kuwa kilimo kwanza hauonekani katika fedha zilizotengwa na Serikali katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Rais alieleza kuwa Serikali itatoa shilingi bilioni 20 kwa ajili ya mkopo wa riba nafuu kwa zana za kilimo kama matrekta madogo. Fedha hizi hazionekani katika bajeti ya Serikali, labda hivyo vitabu vipya vitakavyokuja, hivi vya sasa hamna.

Fungu lililotengwa kwa ajiri ya *Agricultural Mechanization* ni shilingi milioni 700 zinazotosha kuagizia matrekta makukuu 18 na zana zake kutoka Uingereza. Waziri ameeleza kuwa “Fedha hizi zitapatikana kufuatia kusainiwa mkataba wa mkopo baina ya Serikali ya Tanzania na India.”

Je hana uhakika kiasi ambacho kitapatikana kingeingizwa kwenye bajeti? Vile vile Rais alieleza kuwa chini ya mkakati wa kujihami na kunusuru uchumi, Serikali itatoa shilingi bilioni 20 kwa Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa ajili ya kuongeza akiba ya chakula na kudhibiti mfumuko wa bei. Fedha hizo hazikutengwa katika bajeti tunayoijadili. Pia hakuna bajeti ya kuongeza maghala ya kuhifadhia chakula.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme usio wa uhakika linaeleweka. *TANESCO* imeishatutahadharisha kuwa nchi inaweza kuingia gizani. Wizara ya Nishati na Madini imetengewa shilingi bilioni 285.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 378.8 zilizotengwa mwaka 2008/09, sawa na upungufu wa asilimia 24.6. Sababu aliyoitoa Waziri ya

kupunguza Bajeti ya wizara ni "kumalizika mikataba ya kuzalisha umeme kwa Makampuni ya kukodi ya *Dowans, APR na Aggrekko."* Serikali inatenga fedha ikiwa kuna mikataba ya kuifilisi nchi lakini hatuwekezi raslimali yetu ya kuzalisha umeme wa uhakika. Waziri kaeleza kuwa Serikali itaikopesha fedha *Artumas* ili waweze kuendelea kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme kwa mikoa ya Mtwara na Lindi ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa mikoa hiyo.

Hata hivyo fedha za kuwakopesha *Artumas* hazimo ndani ya bajeti. Kwa nini Serikali iikopesha *Artumas*. Kama Serikali ina fedha kwa nini isingie ubia na kununua hisa za kampuni hiyo? Mhes spika Serikali ilikataa kuyapa ruzuku Mashirika ya Umma hata yaliokuwa yakifanya vizuri, na hatimae kuyauza kwa bei chee, jee sasa inakuwa bora kuzipa sadaka kampuni binafsi kwa kisingizio cha hali mbaya ya uchumi duniani?

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii haieleweki na haitabiriki. Mkakati wa Kunusuru Uchumi wa Tanzania dhidi ya Msukosuko wa Uchumi Duniani uliolezwa na Rais Kikwete haukuanishwa waziwazi katika bajeti na kutengewa fedha.

Bajeti isiyotabilika inahujumu vipaumbele vya sera na matokeo ya malengo ya matumizi ya Serikali. Misingi mizuri ya Bajeti inataka Bajeti ya Serikali ijumlishe mapato na matumizi yote ya Serikali bila kujali taratibu maalum za kuendesha baadhi ya miradi na programmu, taratibu za kuidhinisha matumizi na vyanzo vya mapato. Kwa ujumla mapato yote yakusanywe na matumizi kupangwa bila kuzingatia chanzo cha mapato. Utayarishaji wa bajeti hii haukufuata misingi muhimu ya bajeti ya serikali.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa utaratibu wa kutumia kadri tunavyopata *(cash budget*) utaendelea katika mwaka huu wa fedha makadirio yaliyomo ndani ya bajeti hayatafanana na matumizi halisi. Utaratibu wa *cash budget* unadhoofisha sana nidhamu ya bajeti. Mara kwa mara miradi ya maendeleo inaathirika sana na utaratibu huu kwani ndiyo huwa ya kwanza kupunguziwa matumizi. Utayarishaji wa bajeti unakuwa siyo makini kwani bajeti zilizopangwa haziheshimiwi.

Bajeti hii imeweka mianya mipana ya rushwa hasa katika maeneo ya kulipa madeni na kufidia hasara na kudhamini mikopo ya Makampuni. Serikali itabeba mzigo mkubwa wa madeni haya, hivyo kuendelea kuwabebesha Watanzania mzigo kila uchao.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuhami uchumi (*Stimulus Package)* Siku moja kabla ya kusomwa kwa Bajeti, Rais Kikwete aliwahutubia Wabunge na Wazee wa Dodoma kuhusu mtikisiko wa uchumi duniani na jinsi unavyoweza kuathiri uchumi wetu. Hotuba ya Rais ililenga kuelezea hatua zilizochukuliwa na serikali kukabiliana na mtikisiko wa uchumi na ilikuwa inafafanua bajeti ya Serikali iliyotangazwa na Mheshimiwa Waziri ambaye alieleza kuwa hotuba hiyo kwa kiasi kikubwa imerahisisha kazi yake ya kuieleza Bajeti ya 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Rais alieleza kwamba Serikali iliunda kamati chini ya uongozi wa Gavana wa Benki Kuu. Matokeo ya kamati ya Gavana Ndulu ni kuwepo kwa mkakati wa Kunusuru Uchumi wa Tanzania dhidi ya Msukosuko wa Uchumi Duniani.

Katika mkakati huo mpango wa utekelezaji wa malengo na hatua mbalimbali za kuchukua zimeanishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wabunge kupata fursa ya kujadili Mwongozo wa Mpango na Bajeti mapema mwaka huu ambayo ni hatua muhimu katika maandalizi ya bajeti, kwa kuwa unatoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa michango yao mapema kabla ya mapendekezo ya bajeti hayajakamilika na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa rasmi.

Waheshimiwa Wabunge hawakupata fursa ya kujadili Ripoti ya Gavana Ndulu na Mkakati wa Kunusuru Uchumi wa Tanzania dhidi ya Msukosuko wa Uchumi Duniani. Wabunge kama wawakilishi wa Watanzania wanastahiki kupata na kuujadili Mkakati wa Kunusuru Uchumi wa Tanzania dhidi ya Msukosuko wa Uchumi Duniani.

Kwa bahati mbaya hotuba ya Rais haijatolewa Rasmi asubuhi sasa hivi ndio umetutangazia Mheshimiwa Spika, kwamba ipo tayari. Kwa maandishi lakini ilikuwa na taarifa nyingi zinazohusu bajeti na baadhi ya taarifa hizo hazimo katika bajeti iliyowasilishwa na Waziri. Rais ameeleza Mpango wa Kunusuru Uchumi wa Tanzania utagharimu shilingi bilioni 1,692.5 na pesa hizo zimetengwa katika Bajeti. Waziri hakuanisha waziwazi mpango huu katika bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, mtikisiko wa uchumi ulipoanza mwisho wa mwaka 2007 na kuendelea 2008, Serikali ilieleza kuwa mtikisiko huo hautathiri uchumi wa nchi yetu. Wachambuzi wengine walipoeleza kuwa uchumi wetu utaathirika, Serikali haikuwasikiliza na kwa hiyo haikuchukua tahadhari mapema.

Takwimu za Serikali zinaonyesha kwamba mtikisiko wa uchumi duniani hakuathiri ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Pato la Taifa limeongezeka kwa asilimia 7.4. ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2007.

Hata hivyo Waziri ameeleza “Kutokana na msukosuko wa kifedha na kiuchumi unaoendelea duniani, mwenendo wa makusanyo ya mapato umekuwa si wa kuridhisha katika kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka 2008/2009 na mwelekeo ni kwamba hadi kufikia mwisho wa mwaka 2008/2009 mapato hayatafikia lengo kwa asilimia 10;” imekuwaje ukusanyaji wa mapato uathirike kiasi hicho wakati Pato la Taifa limekua zaidi ya mwaka jana. Hicho ni kitendawili, ni vyema waziri ukakitegua. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upungufu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali unachangiwa na misamaha holela ya kodi. Kama Waziri alivyoeleza asilimia 30 ya mapato ya Serikali sawa na zaidi ya shilingi trilioni 2 yanapotea kwa sababu ya misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kutoa mtazamo wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Tshs.9.5trn, wakati Tshs.1.7trn zinarudi kusaidia sekta binafsi kupitia mpango wa kuhami uchumi (*stimulus package*) ambao kwa jinsi ulivyo ni “stabilization package”. Hivyo Bajeti halisi ni Tshs.7.8trn. (kiasi halisi kitakachoelekezwa kwenye shughuli za maendeleo na utendaji wa Serikali).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imefanya utafiti kuona nchi zingine za dunia zinafanya vipi hiyo "*stimulus package*". Katika hotuba hii tumeambatanisha mipango hiyo kwa nchi za Asia, sifa moja kubwa ya mipango hiyo ni kwamba mipango hiyo imetungiwa sheria ya Bunge ili utekelezaji wake uweze kusimamiwa na Bunge ili kuzuia matumizi mabaya.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inakataa kutoa "*an open blank cheque*" kwa Serikali kulipa Makampuni binafsi. Tunataka sheria ya "*Appropriation Act"* iwe na *Schedule* maalum ya "*Stimulus Package"* na iseme waziwazi nani atapata nini, Kamati ya Fedha na Uchumi iwe inapata taarifa kila miezi 3 ya utekelezaji wa hiyo "*stimulus package"*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli uliowazi kuwa "*stimulus package*" inazinufaisha benki tu, kwa kuzipa mwanya wa kufanya biashara nzuri na Serikali kwa kutumia fedha za Serikali yenyewe, na ndio maana nchi nyingine Serikali imelazimika kuwa na hisa ili kuhakikisha kuwa fedha iliyotolewa ambayo inatokana na kodi za wananchi inadhibitiwa na kurudi kwa walipa kodi na wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2007/08 na ile ya 2008/09 Serikali ilikuwa imejizuia kukopa kwenye Mabenki, kwa kigezo kikubwa kuwa Mabenki yaweze kufanya biashara ya kukopesha Sekta binafsi.

Zuio hili liliongeza ufanisi kwa Mabenki kukopesha sekta binafsi kwani mikopo kwa sekta binafsi ilipanda hadi kufikia 40% (taarifa ya Sera ya Fedha-Gavana wa Benki Kuu ya Juni, 2009). *Stimulus Package* itapunguza mikopo ya Benki kwenda kwenye sekta binafsi, na yale mafanikio yaliyokwishafikiwa yatayeyuka, vinginevyo Mabenki yawekewe viwango vya kufikia katika kutoa mikopo nje ya "*stimulus package*" otherwise tutakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Sera ya Fedha ya BOT Serikali itazikopesha benki kiasi cha Tshs.270 Billion kwa minajili ya kuzikopesha Sekta binafsi. Aidha itatoa T.Bill za Tshs. 205 Billion ili kukopa kwenye mabenki hayo hayo.

Je Mabenki yatashindwa kutumia fedha zile zile ambazo Serikali imeziweka ili kukopesha sekta binafsi kutumia fedha hizo kufanya biashara na Serikali kwa fedha za Serikali? Hili litadhibitiwa vipi? Waziri ni vyema ukatueleza.

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu wa mwaka huu wa bajeti ni ile inayoongeza matumizi, madhara yake makubwa ni kwamba mpango huu utaongeza "*inflation"*, na kwa kuwa mfumuko wa bei hapa kwetu hautokani na sera za fedha bali bei za mazao ya chakula, ni dhahiri uwezo wa kudhibiti ni mdogo mno. Hasa tukielewa kuwa kauli mbiu ya "KILIMO KWANZA" kama zile za "Siasa ni kilimo", "Azimio la Iringa" na kadhalika ambayo hadi leo hatujaweza kuwa na chakula cha uhakika.

Mheshimiwa Spika, Wito wa Kilimo Kwanza umeweka vipimo vya ufanisi *(Benchmarks*) au itakuwa kama Siasa ni Kilimo?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi mkubwa na kuongezeka kwa mfumko wa bei hadi kufikia asilimia 30. Kama hatua za uhakika za kudhibiti hazikuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuzalisha chakula cha uhakika, kama nitakavyoelezwa hapo baadae.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hiyo ya Gavana (*Policy Statement* ya *BOT)* inasema kuwa *BOT* itaikopesha Serikali Tshs.300 billion, na kitabu cha mapato (*volume I*) inaonyesha kuwa mwaka huu *BOT* haitatoa mrabaha (*devidends*) kwa wanahisa wake, Kambi ya Upinzani inauliza, hii maana yake ni kuwa zile Tshs 300 billion ni malipo tangulizi "*advance*" ya Mrabaha kwa Serikali?

Kama hivyo ndivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata nini katika mpango huu, Waziri atueleze.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasema kuwa Serikali haina haja yoyote ya kukopa kutoka kwenye Mabenki ya Ndani, jambo la kufanya ni kuweka hisa zake inazomiliki katika makampuni ya fuatayo kwenye soko la hisa.

Hii itaenda sambamba na sheria ya kodi ya mapato kifungu cha 73 cha hotuba ya bajeti ya Waziri kuwa Kampuni zitakazo jioorodhesha katika soko la mitaji kuuza angalau 30% ya hisa zake itapunguziwa kodi ya mapato toka 30% hadi 25%.

Hii ni motisha kwa kampuni kuuza hisa kwa wananchi, inatekeleza sera ya ujasirimishaji wa Watanzania na kupanua "*middle class income*", hivyo kuongeza uwezo wa watu wetu wa kununua na kupanua wigo wa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri wetu, Serikali itapata kiasi cha Tshs. 475 billion kwa kuuza hisa zake kwenye Makampuni yafuatayo:-

- *Celtel (Zain)* hisa 25%.. …………...Tshs.200billion.
- *NBC* hisa 20% ……………………Tshs.150billion.
- *BP* hisa 25% ………………………. Tshs. 90billion.
- Kilombero *Sugar 25%*......................Tshs.35billion.
- Jumla ya Mauzo ni…………… Tshs. 475billion.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona hapa tayari Serikali inawezakupata fedha ambazo walitaka kukopa kwenye Mabenki, yaani Tshs.205 billion,

ambazo zingezidi kutokana na malipo ya riba, hivyo kuongeza deni la Taifa kinyume na sera ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati muafaka kwa Serikali kulieleza Bunge kuwa ina mkakati gani madhubuti wa kuwawezesha wananchi kuwa na fursa za kukopa katika Taasisi za fedha na hasa benki, kwani haitoshi kuiachia Benki kuu kuzipa Benki za Kibiashara kuweka viwango vya riba huku faida yote inayopatikana na biashara hiyo inapelekwa nchi za nje.

Ikumbukwe kwamba sekta isiyo rasmi ndiyo yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Ni kwa njia ya mikopo yenye riba nafuu tu ndio uwiano huu wa mchango wa sekta isiyo rasmi katika Pato la Taifa unavyoweza kukua.

Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu riba nafuu ni kiasi gani, ili wasiachie Benki kuamua wakati fedha ni za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa katika sekta ya afya, pamoja na yale ambayo yanafanyika, ukweli ni kwamba viwango vya huduma za afya bado ni duni sana, lakini kubwa zaidi ni uchache wa wataalam wa afya katika ngazi zote. Serikali ionyesha mpango mkakati wa kukabiliana na tatizo hili. Aidha Sera ya Afya ina upungufu mkubwa, kwani hadi sasa hakuna mkakati wowote wa kuwa na viwanda vyetu vya madawa na vichache vilivyopo vina kiwango kidogo cha uzalishaji wa dawa.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kwa Serikali kuwekeza katika kuwa na Hospitali Kuu za Rufaa, ambazo zitakuwa na viwango vya kimataifa. Utaratibu wa kupeleka wagonjwa nje kutibiwa ni gharama kubwa kwa Serikali, ni vema uwekwe utaratibu mbadala na huo, tuna uhakika hilo linawezekana na faida zake zitaonekana kwa Watanzania. Hivyo juhudi zinazofanywa na NSSF na *Apollo Hospital* ziharakishwe ili kupunguza gharama hizi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonesha kuwa mabadiliko ya maendeleo hupatikana zaidi pale panapokuwapo mabadiliko ya chama kinachoshika Serikali, hivyo hivyo mabadiliko ya kiuchumi huongezeka kasi pale huduma za usafiri wa watu na mizigo zinapokuwa za kuaminika na kutosha.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kuwa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli umeteremka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, usafirishaji wa mizigo kwa *TRL* umepungua toka tani 1,169,000 mwaka 2005 mpaka tani 429,000 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi, hivi kweli Serikali iko makini katika kutumia jiografia yetu kujiongezea mapato kama programu zetu za *vision 2025*, MKUKUTA, *Mini Tiger* na kadhalika zinavyofafanua? Je, nchi yetu itaondokana na kilema cha kutegemea mikopo na misaada?

Mheshimiwa Spika, mbali na udhaifu huu, Serikali ililipa Tshs.4.4billion kwa *RAHCO* ili kufuta madeni mbalimbali ya lilikokuwa Shirika la Reli bila ya idhini ya

Kamati ya Madeni ya Taifa *(NDMC)* na hakuna ushahidi kuwa kampuni hizo zilirejesha kiasi hiki (Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, ukurasa wa 17).

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inatafuta fedha kuiokoa *TRL*, bado tunatoa fedha bila ya nyaraka muhimu za kuthibitisha malipo hayo. Hadi sasa Serikali haijatueleza ni fedha kiasi gani wawekezaji wamewekeza kwa sababu ukisoma Taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali, inasema Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji inaendelea kutafuta fedha ili kutekeleza miradi hii, (ukurasa 227). Ni kutokana na uthibitisho kama huu, ndio tunaitaka hii *Stimulus Package* iwe wazi kwa umma kwa kupitia Bunge lako Tukufu ambalo kwa niaba yake Kamati ya Fedha na Uchumi na kwa kushirikiana na baadhi ya wajumbe wa Kamati za Kisekta husika wafanye tathmini na kutoa baraka, vinginevyo tunaweza kuwa na *EPA No.2*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari, sote tunaona aibu kuambiwa nchi yetu ni maskini huku ikiwa imezungukwa na nchi nane, tuna bandari kubwa na ndogo kadhaa zikiwemo za Dar es Salaam, Mtwara, Zanzibar, Tanga, Pemba, Mafia, Kigoma, Mwanza, Musoma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wakati tuko katika ushindani wa kibiashara ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika ya Mashariki na *SADC*, bandari yetu ya Dar es Salaam mwaka 2008 ilihudumia shehena yenye jumla ya tani 2,316,000 ikilinganishwa na tani 5,703,000 mwaka 2007 sawa na upungufu wa asilimia 59.4, sababu kubwa ikiwa ni kushuka kwa tija ya kupakua na kupakia mizigo na ushindani wa bandari za jirani, Mombasa, Beira na Durban. Meli zilizohudumiwa mwaka 2008 ni 697 ukilinganisha na 3,038 mwaka 2007 sawa na asilimia 77.1. Hivyo hivyo kwa bandari ya Mtwara ilihudumia tani 82,000 mwaka 2008 kulinganisha na tani 112,000 mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 26.8. Meli zilizofika bandarini, ni 36 mwaka 2008 ukilinganisha na 99 mwaka 2007 sawa na upungufu wa asilimia 63.6. Bandari ya Tanga ilihudumia shehena ya tani 178,000 mwaka 2008 ukilinganisha na tani 542,000 mwaka 2007 sawa na upungufu wa asilimia 67.2%- (Hali ya Uchumi Uk.196/197). Meli zilizokuwa zinasafirisha mizigo na abiria kwa kutumia bandari ya Dar zimepungua toka 5,232 mwaka 2000 na kufikia meli 4,154 mwaka 2006 na 697 mwaka 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati washindani wetu wanapanua na kuboresha bandari zao, mfano, Kenya wamewekeza US$200 milioni kwa upanuzi wa Bandari ya Mombasa na ina uwezo wa kuingiza meli zenye uzito wa tani 100,000 sisi bandari ya Dar es salaam haiwezi kuingiza meli yenye ukubwa huo. Hivyo, hata ule mpango wetu wa kuleta mafuta *"in bulk"* unaweza kuwa ghali ukilinganisha na Kenya, kutokana na ukubwa wa meli inayoweza kufunga gati.

Mheshimiwa Spika, leo hii Malawi wameanza kupeleka mizigo yao Beira-Msumbiji na Uganda wanatumia bandari ya Mombasa, sisi tunalaumu hali ya uchumi Duniani. Kama tulipata pesa za kuwapa makampuni binafsi, hivi tumeshindwaje kupanua bandari ya Dar es salaam, Mtwara na Pemba? Au tunaendeleza utamaduni wetu wa kutoa sadaka?

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu za udhaifu wetu wa kusimamia maamuzi yetu na wa Serikali yetu wa kushindwa kuona fursa zilizopo tuzitumie ili kujijengea uwezo wa haraka wenyewe, tunaimba wimbo wa hali ya uchumi duniani zaidi kuliko kujielekeza kwenye udhaifu wa Serikali yetu katika kuamua na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yake, haya yataligharimu Taifa letu kwani wenzetu wanatenda, hawaongei.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka uchambuzi wa kina, uliowazi na wa kushirikishwa Bunge katika kutumia 1.7 trilioni za *"Stimulus Package"*, msisitizo Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa tuangalie changamoto za bajeti ya Serikali kwa sekta zinazotakiwa kuwa kiongozi katika kuondoa umasikini. Ingawa zipo juhudi kubwa za uhamasishaji na utashi wa Serikali kufufua kilimo, bado kuna upungufu mkubwa katika eneo hili. Serikali ambayo haina uhakika wa kuwa na chakula cha kutosha, ni sawa na kiongozi wa familia kutokuwa na uwezo wa kuilisha familia yake. Hali hii inalipunguzia Taifa heshima yake mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Kila inapotokea kipindi kifupi cha ukame, mara moja unaona Serikali na wananchi wake wakihangaika kutafuta chakula kwani akiba haitoshi. Hii ni aibu!

Mheshimiwa Spika, tunapokumbushana haya, hatusemi kwamba Tanzania hakuna maendeleo au mabadiliko, lakini maendeleo hayo ni endelevu kiasi cha kumhakikishia Mtanzania kwamba baada ya Azimio la Iringa la mwaka 1972 la "Siasa ni Kilimo" na kufuatiwa na "Sera ya Kilimo ni Uhai" ya Mwaka 1976, ikaja tena kauli nyingine ya "Kilimo ni Uti wa Mgongo", tunajitosheleza kwa chakula cha kutosha na hata ukame ukitokea tuna chakula cha akiba au chakula kinapokuwa bidhaa adimu duniani tunaweza kuuza na kubakiwa na akiba au bado tunaendelea kuhemea chakula?

Mheshimiwa Spika, katika hayo yote, tunaona Waziri Mkuu kaanza kuyavalia njuga mapendekezo hayo, lakini jambo kubwa ambalo tunaliona kuwa litaendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa mapinduzi ya kilimo ni Sera ya Kilimo ambayo haiendani na hali halisi ya wananchi wa Tanzania. Katika madhumuni ya Sera ya Kilimo ya mwaka 1997 ni kukifanya kilimo kuwa endelevu na cha kisasa. Katika hali ya sasa, pembejeo za kilimo zinapatikana kwa vipindi maalum na pengine nje ya msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Taifa ni chombo muhimu na pekee cha kutafsiri na kutekeleza sera za Chama Tawala na Serikali kwa vitendo. Katika bajeti Serikali inapata fursa ya kupanga matumizi ya fedha kidogo zilizopo katika maeneo na sekta zinazohitaji kupewa kipaumbele ili malengo makuu ya Serikali yatekelezwe. Aidha, Rais Mstaafu Mkapa katika hotuba zake za kila mwezi alisema:-

*"Bajeti ni kipimajoto cha uhai wa mtu, na afya ya uchumi wa Taifa…. Daktari mzuri wa uchumi ataitumia bajeti kutoa tiba ya kupambana na umasikini na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi…..". Mwisho wa kunukuu.*

Katika nchi maskini kama Tanzania, malengo ya Sera za Serikali yanapaswa kuwa ya kujenga mazingira mazuri ya kukuza uchumi na kuongeza ajira ili kupunguza

na kuutokomeza umaskini. Katika kuendeleza uchumi, matumizi ya Serikali yanapaswa kuwa na malengo matatu makubwa:-

(a) Matumizi ya Serikali yalingane na uwezo wa mapato ya Serikali na yawe endelevu, pasiwe na nakisi kubwa ya bajeti inayojazwa kwa kuchapisha fedha, kukopa ndani au kukopa nje. Bajeti ya Serikali lazima ilenge katika kupunguza kutegemea misaada na mikopo;

(b) Bajeti ya Serikali igawanywe katika sekta mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi na kutoa kipaumbele katika maeneo yanayokuwa chachu katika kukuza uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umasikini na kuwa na chakula cha kutosha na nishati ya uhakika; na

(c) Matumizi ya fedha za Serikali katika sekta zilizopewa fedha hizo yaendeshwe kwa ufanisi na kwa kuongeza tija. Darasa linalogharimu shilingi milioni moja lisijengwe kwa gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, je, malengo haya ni kwa kiasi gani yamefikiwa na Serikali? Sote ni mashahidi wa wafanyakazi wetu waliotumikia Taifa hili kwa maagizo na miongozo ya Serikali yao wanavyosumbuka na kutaabishwa katika kudai haki zao zilizotokana na ahadi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti ya mwaka 2008/2009. Katika Bajeti ya mwaka 2008/2009, Serikali ilipanga kutumia jumla ya Tshs. 7.3 trilioni. Kati ya hizo, jumla ya shilingi 2.43 trilioni zilikuwa ni fedha za wafadhili. Matumizi ya kawaida yalipangiwa Tshs.4.8 trilioni. Matumizi ya Maendeleo yalipangiwa Tshs.2.5 trilioni. Kati ya hizo Tsh. 1.55 trilioni ni fedha za wafadhili. Sambamba na hilo Serikali ilikuwa na upungufu wa ukusanyaji wa mapato yake wa Tshs.330,080 millioni.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia mwenendo wetu wa matumizi na nidhamu nzima ya Serikali kubakia kwenye mstari wa kile ambacho kimepitishwa na Bunge kuwa ndiyo hicho kitakachotekelezwa bado hatujafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida ambayo hayaendani na yale yaliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge katika bajeti, ni matokeo ya udhaifu wa wazi kwa kushindwa kwa bajeti kama chombo cha kusimamia utekelezaji wa sera za mikakati na maamuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika ukisoma Hansard ya tarehe 16 Juni, 1994, ukurasa wa 80 na 81, Marehemu Prof. Kighoma Malima akisoma bajeti ya Serikali alitoa suluhisho la jinsi ya kukabiliana na ugonjwa wa kupanda kila mara kwa matumizi ya kawaida dhidi ya makusanyo ya Serikali, kuwa ni kupunguza ukubwa wa Serikali. Serikali iliunda Tume iliyoongozwa na Mheshimiwa Basil Mramba kutatua tatizo hilo. Hadi sasa toka Tume ya Mramba iundwe ni takriban miaka 19, hakuna lililofanyika na nchi inazidi kuwa na bajeti tegemezi kwa sasa utegemezi wa bajeti ni 33.45% pamoja na kuwakopa wafanyakazi

hasa Walimu, Askari na watumishi wa afya ambao hadi sasa wanaidai Serikali Tshs. 8.46 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa kuliona hilo na kuendeleza maamuzi ya Serikali ambayo hayakutekelezwa ikaleta hoja ya kubadilisha Katiba ili kuwa na ukubwa wa Serikali unaotajwa na Katiba, lakini kwa masikitiko makubwa Mheshimiwa Spika unaelewa nini kilitokea hata Waheshimiwa Wabunge hawakupata nafasi ya kuona hoja yenyewe, kuisoma na kuielewa na kisha kuitolea maamuzi. Kambi ya Upinzani inaona upo umuhimu wa kuwa na kifungu katika Katiba kinachoweka ukomo wa ukubwa wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinazotumika kwa shughuli za kila siku kama vile kuandaa takwimu za pato la taifa hazipewi kipaumbele kwani hazina posho na magari ya mradi. Mipango yetu ya kukuza uchumi ni dhaifu kwa kutokuwa na takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2007/2008, baada ya kuelezea kwa uthibitisho upungufu katika takwimu zetu za Taifa, tulishauri kuundwa kwa Jopo la Wataalam wa ndani na nje kutathmini usahihi wa takwimu mpya za pato la Taifa na kupendekeza taratibu za kuboresha ukusanyaji wa takwimu hizo. Je, Mheshimiwa Waziri, utekelezaji wake ukoje?

Mheshimiwa Spika, hoja yetu hii inapewa nguvu na mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, ukurasa wa 162 kuwa, pamoja na mambo mengine, Serikali inakuwa na vipaumbele vingine ambavyo haviainishwi kwenye bajeti inayopitishwa na Bunge na hivyo kusababisha matumizi ya Serikali kutokuwa kama vile inavyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa kuzingatia Sheria ya Fedha *(Finance Act)* na Katiba ya nchi, ni Bunge tu ndilo lenye mamlaka ya kuidhinisha mapato na matumizi. Inashangaza kuona kuwa baadhi ya Idara za Serikali zinaweza kutumia fedha bila ya kuzingatia utaratibu wa kifedha. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa iliidhinishiwa kutumia Tshs.34,516,361,130.74 lakini ikatumia Tshs.40,820,717,484.65 ikiwa ni ziada ya Tshs.7,914,996,040.27 kwa Balozi zetu bila ya Bunge kuidhinisha. (Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Uk.176).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda ielezwe hatua zinazochukuliwa kwa wanaokiuka Katiba, Sheria na Kanuni za Fedha bila ya wasiwasi wowote na kwamba kitendo hicho ni kunyang'anya madaraka ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa uwekezaji toka nje. Ni kweli kutokana na msukosuko wa kiuchumi duniani, uwekezaji kutoka nje kwa miradi yetu mikubwa kama mradi wa Kabanga-Nikel kule (Kagera) na mradi wa uchimbaji Aluminium wenye thamani ya $3.5Billion. Miradi ambayo inaweza kufutwa kabisa ni ujenzi wa Bandari ya nchi kavu Dar, Ujenzi wa kinu cha kuzalishia umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* pamoja na ujenzi wa kiwanda cha saruji Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema ukiona mawimbi makali ndio unaingia gatini, uhodari ni wa nahodha tu, katika hali hii, shirika letu la *NDC* limeweza kwa mfumo wa *PPP* kuanzisha mradi wa uchimbaji wa mkaa wa mawe Ngaka, Songea na kuanzia mwezi wa Januari wataanza uzalishaji na wanakisia kutoa tani milioni moja kwa mwaka. Cha kusikitisha shirika hili halijapewa hata senti moja na Serikali na zaidi hata kuruhusiwa kuendelea kufanya "*exploration*" kwenye mgodi wa Mchuchuma ili waweze kuzalisha umeme na kuuza mkaa wa mawe nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hali inaonesha kuwa pamoja na matatizo yaliyopo Duniani lakini zipo bidhaa bado zina soko zuri kama vile dhahabu na makaa ya mawe kwani, mbiu ya mgambo ya mataifa makubwa ni "*energy*" nishati. Je, tunazitumia fursa hizi vizuri au tutaendelea kuimba hali ya uchumi duniani tu? Tunahitaji Kuzinduka.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kisekta katika uchumi, sekta ya kilimo. Ukuaji wa uchumi wetu unachangiwa na sekta kadhaa, sekta ya kilimo ikiwa haiongozi ila ni muhimu sana, lakini kwa hali ya kawaida na kwa kufuatana na nadharia za uchumi ni kwamba kadri uchumi unavyokuwa sekta ya kilimo inatakiwa kupungua na kutoa mwanya kwa sekta nyingine za uchumi kama viwanda kushika kasi, lakini kwa Tanzania ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa kilimo ndiyo sekta pekee yenye nguvu na uwezo wa kuiwezesha nchi yetu kuondokana na lindi la umaskini wa kipato. Hivyo basi, ni dhahiri kilimo kinaweza kufanywa kuwa endelevu na chenye manufaa (*sustainable agriculture*) kwa wakulima na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Sera ya Kilimo ya mwaka 1997 inatamka bayana kuwa ni kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na endelevu. Kwa maana hii ya madhumuni ya sera ni kwamba kilimo kilitakiwa kuwa ni kwa wale wenye uwezo mkubwa kiuchumi na ukweli ni kwamba Watanzania wanaojihusisha na kilimo ni wale wenye uwezo hafifu sana kiuchumi na hii ni kasoro ya kisera kwani sera haikuwapa kipaumbele wakulima,wafugaji na wavuvi wadogo. Mfano mzuri wa sera hii ni kama huu, wa wakulima wawili; mmoja ana uwezo kiuchumi na mwingine hana. Ikitokea teknolojia ya kuongeza uzalishaji imeletwa pale kijijini, ni yule mwenye uwezo atakayeipata na kuzidisha uzalishaji na wakulima wenye uwezo katika vijiji vyetu wapo wangapi? Aidha, kilimo cha kisasa na endelevu ni kile kisichotegemea mvua na pembejeo hazitakiwi kungojea msimu wa mvua ili matumizi yake yawepo.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Serikali yalenge katika kuzindua mapinduzi ya kilimo na hasa kuongeza uzalishaji wa chakula ili tuondokane na aibu na adha ya baa la njaa. Tujifunze kwa wenzetu wa Malawi namna ruzuku ya mbolea ilivyoongeza uzalishaji wa mahindi ambako mfuko mmoja unauzwa kwa Tshs 8,000/=. Ni muhimu mbolea na pembejeo za kilimo ziwafikie wakulima kwa wakati. Mbolea husika iwe imefanyiwa majaribio. Wakulima wa Mbeya waliotumia mbolea ya Minjingu walipata hasara kwani mimea yao ilikauka. Serikali inawafikiria vipi wakulima waliopata hasara hiyo kutokana na mbolea?

Mheshimiwa Spika, *ASDP* ni programme ya miaka saba ambayo bajeti yake ni Tshs 2.7 trilioni kuanzia mwaka 2006-2013 hadi sasa ni takribani miaka mitatu imekwishapita, tulitakiwa kuwa tumeshatumia shilingi bilioni 578.6 sawa na asilimia 21.4, lakini tumetumia Tshs.198 bilioni tu sawa na asilimia 7.3, ni jukumu la Serikali kuwaeleza wadau wake hadi sasa mafanikio gani yamepatikana au *programme* imeshindwa hata kabla ya ukomo wake kufika?

Mheshimiwa Spika, Jambo la kustaajabisha ni kwamba kabla ukomo wa *programme* hiyo tunaanza tena *programme* nyingine, ambayo inakuja na kauli mbiu ya "Kilimo Kwanza" hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kuna kitu ambacho kinapigiwa upatu nacho ni kilimo cha mkataba "*contract farming"*, kabla ya kuingia, kwanza tuangalie mpango huu umemnufaisha vipi mkulima wa tumbaku ambaye amekuwa mtumwa wa Makampuni ya Tumbaku kwa miaka zaidi ya 40 sasa? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia kwa mtazamo wa kuinua hali ya mkulima na sio kwa upande wa mwekezaji peke yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaona ni busara kwanza kutumia miundombinu ya viwanda vya mazao ya kilimo iliyopo kabla ya kuanza kuhamasisha kilimo cha mazao ambayo viwanda vyake vya usindikaji havipo. Mfano viwanda vya bia, viwanda vya ngano, korosho, viwanda vya kukoboa na kusaga nafaka na pia viwanda vya kukamua matunda. Kwanza tuangalie viwanda hivyo vina upungufu wa malighafi kwa kiasi gani, kwa njia hii tutakuwa na uhakika mazao yote ya wakulima yatapata soko. Ni vyema viwanda vya Zana za Kilimo vya UFI (Dar) na ZZK (Mbeya) vifufuliwe kwa gharama yoyote ile, ili dhana nzima ya kilimo kwanza iwe na maana kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuna zao la muhogo ambalo ni zao linaloweza kustawishwa katika eneo lolote katika nchi yetu, zao hili ni hazina kubwa lakini Serikali bado haijawa na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kuwa linakuwa zao mkombozi kwa kuuzwa nje ya nchi na pia kwa matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Spika, tuna uhakika Chuo cha Ukiriguru na Naliendele vikisaidiwa, zao hili linaweza kuwa zao kubwa la kuingiza fedha za kigeni kama ilivyo katika nchi za Afrika ya Magharibi hasa Nigeria. Takwimu za uzalishaji wa zao hili kwa kipindi cha takribani miaka 21 iliyopita, kutoka 1986 hadi 2007 inaonyesha tofauti ya tani 88,000. Wakati tofauti ya idadi ya watu kwa kipindi hicho ni 4,706,612 (kitabu cha hali ya uchumi mwaka 2007). Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani kilimo hicho kisivyotiliwa mkazo. Mfano mzuri wa uzalishaji wa muhogo ni Wilaya ya Newala, wananchi wa Newala wanavyotumia zao hilo kuwanusuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara katika vipindi vya uhaba wa chakula. Tatizo ni kuwa Serikali haijaona umuhimu wa zao hilo kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati sisi tunalalamika kuhusiana na kushuka kwa usafirishaji nje wa mazao asili na mazao ya nafaka, wenzetu Uganda takwimu zinaonyesha kuwa kulikuwa na ongezeko la usafirishaji nje kwa mazao yao, kama

ifuatavyo: Kahawa iliongezeka kwa 5.2%, Pamba kwa 8.9%, Chai kwa 7%. Mazao ya nafaka, mahindi na maharage yaliongezeka kwa 55% na 34% kwa mfuatano. Kambi ya Upinzani inajiuliza ni vipi jirani zetu Uganda wanakuwa na ongezeko kama hilo na sisi tunashindwa?

Mheshimiwa Spika, kulingana hali ya uchumi ilivyo kwa sasa Duniani, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwekeza katika kilimo hasa cha chakula ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza masoko ya nje hasa nchi za jirani. Swali kubwa la kujiuliza ni kwa vipi bonde la mto Rufiji limetumika kuzalisha chakula? Mito isiyokauka zaidi ya 140 iliyopo katika Mkoa wa Morogoro maji yake yanatumikaje?

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa kwa sasa Tanzania inaweza kujivunia soko la takribani watu 100 milioni au zaidi kwa nchi jirani pamoja na zile mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Hii ni pale kama Serikali itakuwa na mtazamo chanya kuhusiana na biashara.

Mheshimiwa Spika, nishati. Ili kilimo kiende, nilazima nishati ya umeme iwe ya uhakika, kwani huwezi kuwa na viwanda vya kusindika mazao bila ya kuwa na nishati. Hivyo kutokana na kauli mbiu ya kilimo kwanza, Kambi ya Upinzani tunasema kwanza "Kilimo na Nishati".

Mheshimiwa Spika, katika kubuni njia za kumpunguzia mzigo wa maisha Mtanzania, Kambi ya Upinzani imefanya utafiti kuona wenzetu ambao wameamua kubana matumizi wanafanyaje katika kupunguza matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi nyingi ambazo wamepanga mipango madhubuti ya kutumia "*energy saving bulbs*" kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji mfano mzuri ni nchi ya Uganda ambao wana mpango wa kusambaza balbu 800.000 ili kuweza kuokoa kiasi cha zaidi ya US $ 1,000,000 kwa punguzo la MW 30 na Serikali ya nchi hiyo tayari wameondoa *VAT* ya asilimia 18 na *import duty* ya asilimia 25 katika bajeti ya mwaka jana kwa kampuni ya Osram ya Ujerumani kwa uingizaji wa taa hizo ili kupunguza gharama za ununuzi na kutoa bure kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kununua balbu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tafiti zilizofanywa nchini Kenya, zinaonesha kuwa nchi hiyo inapoteza kiasi cha shilingi bilioni 10 za Kenya kwa mwaka kwa kutumia taa ambazo zinatumia umeme mkubwa ambazo fedha hizo zingeweza kuwasomesha Wanafunzi wa Shule zote za Msingi nchini humo. Laiti kama kila nyumba itatumia "*energy saving bulbs*" basi wangeweza kuokoa kiasi cha MW 131 ambazo ni sawa na punguzo la asilimia 80. Hii inaonyesha kwa kupitia mpango huu "*line*" yenye uwezo wa kuwahudumia wateja wapatao 1,000 basi ingeweza kutoa huduma kwa watu 5,000.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mpango huu pia nchi ya Ghana wameweza kuokoa kiasi cha fedha US$ 12 milioni kwa kuweza kupunguza GW 2. Nchi ya Australia tayari wameshapitisha sheria ya upigaji marufuku uuzaji wa taa za zamani ambazo

hutumia umeme mkubwa na badala yake kuhamasisha utumiaji wa “*energy saving bulbs”* nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiona nchi mbali mbali duniani zinafanya juhudi hizo ni dhahiri kuna nafuu kwa mfano, mtu mwenye kipato cha wastani na anayeishi kwenye nyumba ya kawaida yenye familia ya kiafrika huwa anatumia wastani wa unit 380 za umeme kwa mwezi kwa wale wanaotumia balbu ya *watt* 60 lakini familia hiyo hiyo inapotumia balbu ya watt 20 *(energy saving bulb)* angetumia wastani wa *unit* 125, ikiwa ni punguzo la matumizi la asilimia 67. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kuifanyia kazi taarifa hii ili tupunguze matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi. Sekta ya uvuvi na hasa ile ya uvuvi wa bahari kuu (*deep sea fishing)*, ni sekta ambayo kwa miaka mingi tumekuwa tukiipigia kelele nyingi sana kuwa Tanzania haijaitumia vizuri katika kukusanya mapato. Haya ni baadhi ya yale tuliyoshauri, katika kuhakikisha kuwa Sekta Uvuvi inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla. Inashauriwa bandari za Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar zitenge maeneo ya bandari za samaki (*Fish Ports and Fish Processing Plants*) ili meli zote za uvuvi wa bahari kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula wanapo kuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato. Aidha, njia hii itakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa maana ya kuwepo kwa kile kinachoitwa “*forward and backward linkage”*. Kwa uamuzi huu, mapato yanakisiwa kuwa Tshs.3bn ambayo Serikali ingekusanya.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo. Sekta hii imekuwa ikichukuliwa kama vile mtoto wa mitaani, ilikuwa haipewi heshima inayostahiki. Ni matumaini ya wafugaji, baada ya kuwa na Wizara maalum, hali ya wafugaji itabadilika kwa kuwa na madawa, majosho na maeneo maalum ya malisho ya mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa mazao ya baharini na kwenye maziwa, mifugo inaweza kuwa kichecheo kikubwa cha mapato ya haraka haraka kama ushirikiano wa wafugaji na Serikali utaimarishwa zaidi ili kutumia masoko kama ya Saudi Arabia ambao kwa wastani huagizia milioni za mbuzi, kondoo na nyama kutoka nchi mbalimbali duniani kwa matumizi yao, ibada ya Hijja na Umra.Uganda imepewa *order* ya mbuzi 10,000 kwa mwaka na sisi tunaweza kutumia fursa ya masoko haya kama tutawapa huduma stahili wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, kama zilivyo Serikali karibu zote Duniani, Serikali ndio mnunuzi mkubwa wa vifaa mbalimbali na huduma kwa wananchi wake kwa kila mwaka. Manunuzi hayo uhusisha kuanzia vifaa vya maofisini hadi mitambo mikubwa ya hospitalini. Manunuzi haya hutumia mabilioni ya shilingi kila mwaka, ambapo hufanywa kwa njia ya kutoa zabuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kadhia hiyo yote ya kufanya manunuzi, Serikali imejikuta ikitumia gharama zisizo za lazima kama vile kutoa matangazo kwenye vyombo vya habari, kama utaratibu na kanuni za zabuni za Serikali zinavyotaka, uchapishaji wa “*tender documents”* na kadhalika. Kama hiyo haitoshi muda wa vikao ambao zinatumia

Kamati za Manunuzi katika kuangalia nyaraka za zabuni na vikao hivi wanakaa watu wa kada ya juu ya watumishi wa Serikali, maana yake posho za vikao zinalipwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatumia asilimia 80 ya fedha za matumizi katika kufanya manunuzi ndani na nje. Kwa kuweka kumbukumbu sawa katika bajeti za Kambi ya Upinzani kwa miaka ya nyuma kuanzia bajeti ya mwaka 2004/2005 tumekuwa tukiishauri Serikali kuanzisha mfumo wa ununuzi kwa kutumia njia ya Mtandao, (*E-procurement)*, ambao ungefanyika vizuri zaidi kama Serikali ingetenga fedha kwa Mgongo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia takriban 70-80% ya matumizi ya kawaida katika zabuni za bidhaa na huduma. Kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006, Serikali ilitumia Tshs. 2,018 bilioni kama matumizi ya kawaida, kati ya hizo Tshs.1,140 bilioni zilitumika katika zabuni.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ingetumia njia rahisi ya kutoa zabuni ambayo ingepunguza 10% ya gharama nzima ya zabuni ingeokoa Tshs. 141 bilioni kwa mwaka katika ngazi ya Serikali Kuu na kiwango hicho kingekwenda sambamba katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, inaonyesha kuwa Serikali bado haijaelewa ni kwa jinsi gani utaratibu huu utaokoa ubadhirifu na ufisadi wa hali juu unaotokea katika sekta nzima ya manunuzi yanayofanywa na Serikali. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ikubali kutumia utaratibu huu wa *E-Procurement*, wasiwasi wa kuwa wafanyabiashara wetu bado hawajaweza kutumia mtandao, ni woga ambao unazidi kutoa mianya ya Serikali kuendelea kupoteza fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya *CAG*, ukurasa wa 122, unaonyesha hasara ya Tshs. 11,233,987,843.37 iliyotokana na udhaifu katika uingiaji na usimamizi wa mikataba ya manunuzi. Hizi ni fedha nyingi sana kama zingeingizwa katika mipango ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, itaendelea kuikumbusha Serikali kuwa utaratibu wa *Electronic Procurement,* ndiyo utaratibu pekee ambao utakaoipunguzia Serikali matumizi katika manunuzi ya bidhaa na huduma na kuiepusha na manunuzi ya bidhaa hewa. Kinyume cha hapo tutaendelea kulalamika upandaji wa gharama kwa watoaji wa huduma na manunuzi ya bidhaa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali inakusudia kutumia zaidi katika matumizi ya kawaida (Shs.6.6 trillion) kuliko matumizi ya maendeleo (Shs.2.8 trillion.) zaidi ya hapo katika miaka 12 ya bajeti za nyuma, matumizi halisi ya maendeleo yamekuwa madogo kuliko yalivyoidhinishwa katika bajeti. Hii ni kama tulivyowahi kusema kuwa ukubwa wa Serikali utasababisha matumizi makubwa ya kawaida. Kambi ya Upinzani, inaona kuna kasoro kubwa ya kiuwiano kati ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo, hivyo kucheleweshaji ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini. Fedha nyingi zinatumika katika uendeshaji wa Serikali kuliko katika maendeleo na huduma za jamii na

hivyo kupanda kwa pato la Taifa kutokuwa na manufaa ya moja kwa moja kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Makaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali *(CAG,)* katika Wizara na Idara za Serikali tulizochambua mathalani tumebaini kuna upungufu wa makusanyo ya mapato. Mrahaba usiokusanywa kutoka kampuni ya almasi ya *Williamson Diamond Ltd.* ni shilingi 841,137,251na *Tansort* Tsh.206,662,556.

Aidha, misamaha ya Kodi nayo imekuwa ya kutisha, kwani hadi kufikia mwezi huu wa Juni 2008, kiasi cha Tshs.819.9 bilioni zilikuwa zimesamehewa kama kodi huku misamaha hii mingi ukiondoa ya mashirika ya dini ikiwa haijamnufaisha mwananchi masikini. Hiki ni kiasi kikubwa kwa nchi inayoomba misaada kila kukicha. Kambi ya Upinzani inaona huu ni upungufu mkubwa wa mapato ya wanyonge wa Watanzania kwa kuyatupa bila utaratibu wa wazi na unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kumalizia tathmini yetu kwa kukumbusha kwamba Kambi ya Upinzani mwaka jana ilikataliwa ombi lake la kuunda Kamati ya Bunge kuchunguza *EPA*, *Twin Tower*, *Mwananchi Gold Mine* na Meremeta. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri tena kutoa ufafanuzi, kuhusu mambo yafuatayo:-

Waziri alieleze Bunge lako Tukufu thamani halisi ya gharama za ujenzi wa majengo ya Benki Kuu (*Twin Tower*) ambayo kwa taarifa ya Benki Kuu gharama imeshazidi USD500 million au wastani wa Tshs. 600 bilioni na mjenzi bado hajakabidhi rasmi majengo pamoja na kwamba lilifunguliwa na Rais Mstaafu Mkapa mwaka 2005 kabla ya kustaafu. Aidha, kuna wasiwasi kuwa matumizi haya pia yalisababisha mfumuko wa bei, tunataka maelezo. Pia tunamtaka atupatie taarifa ya uchunguzi iliofanywa na Benki Kuu yenyewe ili tuweza kulinganisha na taarifa tulizo nazo.

Mheshimiwa Spika, Bunge lililopita tuliomba Bunge lako Tukufu lipewe maelezo juu ya uwekezaji wa *BOT* katika *Mwananchi Gold Mine* wa Dola za Marekani 5,512,398.55 hadi tarehe 30 June, 2006, kwamba je, *BOT* iliendelea kuwekeza katika kampuni hiyo binafsi na kiasi gani cha mapato yaliopatikana hadi sasa? Tunataka Serikali itupatie maelezo ya kina ambayo tunatumaini yatakuwa tofauti na ya mwaka jana, yatakuwa si majibu ya kisiasa.

Katika kikao cha bajeti cha 2006/2007, Bunge lilielezwa kuwa ule Mradi ulioasisiwa na Marehemu Baba wa Taifa wa kuwapatia Wanajeshi wetu fedha kwa ajili ya kuendeshea mradi wa Nyumbu, *Meremeta Gold Company* ambayo ilikuwa chini ya uongozi wa *Time Mining* ya *South Africa* na kudhaminiwa na *BOT* kwa USD 100 million, iko katika hatari ya kufilisika, lakini tukaambiwa kuwa *BOT* ilikuwa ikifanya tathmini. Kambi ya Upinzani, inataka kupata taarifa ya kina kuhusu tathmini iliofanywa na *BOT* juu ya mradi huo. Aidha, tunataka kupatiwa taarifa rasmi juu ya umiliki wa mgodi huu sasa. Vinginevyo mgodi huo ukabidhiwe *STAMICO* kwa fursa zile zile au zaidi ya zinazopewa makampuni ya nje ili Watanzania waonje matunda ya rasilimali zao.

(a) Katika Kamati tuliomba kupewa taarifa juu ya *JFC*, Waziri katika majibu yake (mwaka jana 2007/2008) kwa kamati (uk2.) alijibu “wakati uamuzi kuhusu mapendekezo ya Tume unasubiriwa, bajeti ya 2007/2008, imetenga mgao wa Zanzibar kwa utaratibu wa asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti”. Mwaka huu Waziri katika hotuba yake Ukurasa wa 19 amesema “...Serikali zote mbili zimekamilisha uchambuzi wa taarifa za Tume na sasa ziko kwenye taratibu za kupatiwa maamuzi na Serikali hizo” mwisho wa kunukuu.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi lini Serikali itaendelea na kuvunja Katiba? Naomba Waziri atueleze. Kutokutekelezwa kwa hili kumesababisha matatizo mengi katika mgawo wa rasilimali za mapato na matumizi ya Muungano, jambo linalopelekea manung’uniko yasiyokwisha. Kwa mfano, mapato yanayotokana na gesi, mapato ya kodi na pia gharama za kuchangia shughuli za Muungano. Ni vyema Bunge lako Tukufu likasimama kidete, kukataa Katiba kuendelea kuvunjwa.

(c) Kambi ya Upinzani mara hii inataka kupata tarehe ya kuanza mfuko huu, hatuko tayari kuendelea kushiriki kuvunja Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka juzi 2007/2008 (uk.59), Serikali ilikusudia “kuanzisha utaratibu wa kupitisha moja kwa moja *(fast tracking)* bila ukaguzi bidhaa zote zinazoagizwa…”. Utaratibu huu ni mzuri kama upo uadilifu wa kutosha wa walipa kodi na wakusanyaji wa kodi. Serikali ilipoona kuna udhaifu katika utendaji Bandarini, iliamua kukodisha shughuli za bandari kwa makampuni mbali mbali. Kambi ya Upinzani ilitegemea Serikali kuja na tathmini ya utekelezaji wa makampuni hayo ili iwe rahisi kwa Bunge lako Tukufu kuamua, juu ya utaratibu uliopendekezwa na Serikali kama usimamiwe na *TRA* au kampuni binafsi, kwani kuna mashaka kwamba makampuni yaliyoko bandarini yameshindwa kufanya kazi zao kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa “*fast tracking*” unaweza kutumiwa kuficha udhaifu wa makampuni yaliyopewa kutekeleza shughuli za bandari. Aidha, utaratibu huu unaweza kuwa njia moja ya kuipunguzia mapato Serikali. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri atupe tathmini ya mpango huu kwa kungalia makusanyo ya kodi kwa walipa kodi hao hao wakati walipokuwa wakikaguliwa na sasa ambapo hawakaguliwi Bandarini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2009/2010. Kama nilivyoeleza wakati ninachambua matumizi ya Serikali ya mwaka wa bajeti 2007/2008, matumizi halisi yaliyoainishwa katika hali ya Uchumi wa Taifa na bajeti iliyopitishwa na Bunge ni vitu viwili tofauti. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi hakufanya uchambuzi wa matumizi halisi kisekta au kwa kila fungu. Hatuna sababu ya kuamini kwamba katika bajeti hii matumizi yatafuata makadirio yatakayopitishwa na Bunge hasa ukizingatia kuwa Serikali bado inasisitiza kuendelea na utaratibu wa *cash budget* wa kutumia tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia umaskini wa Tanzania, umuhimu wa elimu na afya katika maendeleo na ujenzi wa nguvu kazi iliyo na tija, nafasi ya mapinduzi ya kilimo katika kuchochea kukua kwa uchumi, kuondokana na baa la njaa na kuutokomeza

umaskini na ulazima wa miundombinu hasa barabara na nishati katika kuiwezesha sekta binafsi kuwekeza na kuzalisha bidhaa na huduma, mfumo wa bajeti utakaokidhi mahitaji ya maendeleo ni kuitengea Elimu asilimia 22, Afya asilimia 12, Kilimo asilimia 12, Miundombinu asilimia 20, Maji 10, Nishati asilimia 9, Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia 5%, Matumizi mengineyo asilimia 10% ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani bajeti ya Serikali itumie asilimia 25 ya pato la Taifa. Asilimia 20 ya pato la Taifa likusanywe kama kodi na mapato mengine ya ndani ya Serikali na asilimia 5 ya pato la Taifa itokane na misaada. Kwa kuanzia ikiwa misaada toka nje itakuwa mikubwa bajeti ya miundombinu iongezwe ili kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi. Uchumi unavyokua mapato ya Serikali yataongezeka na kutegemea misaada ya nje kutapungua. Matumizi ya Serikali hayafuati mwongozo huu.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Uchumi kaeleza kuwa "mapato ya ndani yamelengwa kufikia shilingi bilioni 4, 728.595 (trilioni 4.728) sawa na asilimia 18.5 ya Pato la Taifa (kwa takwimu za sasa). Hili ni ongezeko la asilimia 31 kutoka mapato yaliyotegemewa kukusanywa mwaka 2007/2008." Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 39 ukilinganisha na makadirio ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, Waziri hakufafanua maeneo yatakayoongeza mapato hayo. Ni vyema angalau Waziri akatueleza vianzio vya mapato haidhuru kwa mafungu makubwa kama vile Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Kodi ya Ushuru wa Forodha, Kodi ya Mauzo na *Excise Duty,* kodi na tozo ya mafuta, kodi ya mapato na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wa Kambi ya Upinzani juu ya vipaumbele vya bajeti; kupunguza bajeti tegemezi kutoka 34%-31.8%. Katika jambo hili, Kambi ya Upinzani haina budi kuikumbusha Serikali kile ambacho tulikisema kwenye bajeti ya mwaka 2007/2008 kuwa tuliweza kupunguza utegemezi wa bajeti hadi kufikia asilimia 31.8%, tunashukuru Serikali kwa kufanyia kazi mapendekezo yetu japo haikuweza kufikia lengo tulilokuwa tumeliweka mwaka jana kwani Serikali imeweza kupunguza utegemezi hadi kufikia asilimia 34 tu kwa makadirio ya bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano uliopita wa Bajeti tulisema sana juu ya jambo hili la kutegemea wafadhili katika maendeleo yetu. Kambi ya Upinzani inaipongeza *TRA* kwa kukusanya mapato kwa kiwango marudufu ukilinganisha na miaka iliyopita. Lakini pia tulisema kuwa uwezo wa Serikali kukusanya mapato ni mkubwa zaidi, ila kuna uzembe mkubwa na kutojali (*laxity*), ubadhirifu na ufisadi kama inavyodhihirishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka hadi mwaka. Madhara ya Bajeti ya namna hii ni kwamba tunapopata matatizo inabidi kupitapita na kupunguza matumizi kadhaa (*realocation*) ili tu kuweka hali sawa ya madhara yaliyotokea. Hii ni hatari kwa Maendeleo ya Watanzania kwa kiasi kikubwa kwani hata bajeti ya mwaka huu baadhi ya Wizara zilipunguziwa fedha bila mpangilio.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya mapato. Kambi ya Upinzani katika kuinua uchumi wa nchi na mwananchi, imeibua vyanzo vipya vya mapato na vile

ambavyo mwaka jana tulivisema na baadhi kufanyiwa kazi na Serikali kwenye bajeti yake ya mwaka 2008/2009 ingawa vingine imeshindwa kuvifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo kama Serikali ingekuwa makini na kuchukua maamuzi tunayopendekeza, mapato ya Serikali yangeongezeka marudufu. Meneo yenyewe ni kama yafuatayo:-

i. Kuongeza ada ya leseni kwa meli za nje zinazovua katika bahari kuu hadi kufikia USD 50, 000 kutoka inayotozwa sasa ambayo ni USD18, 000 kwa mwaka. Kulingana na takwimu zilizopo ni kuwa kuna meli 140 (japo Kumbukumbu za Bunge-Kikao Cha tatu 5th.Feb.2004 Serikali ilisema kuwa imetoa leseni 193 za Meli za Uvuvi) za nje zilizopatiwa leseni za uvuvi katika bahari kuu ya Tanzania. Kwa maoni haya, mapato ya yatakuwa Tshs 9.5bn ambayo sasa hayakusanywi. Pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kusema meli zinazovua kinyume cha sheria ni 200, kwa ajili ya kuwa na uhakika wa mapato bado tunabaki na takwimu za mwaka 2007/2008;

ii. Kuongeza tozo la mrahaba wa mauzo la asilimia 10 katika bidhaa za samaki zinazovuliwa katika Bahari Kuu. Kila meli kwa mwaka inavua wastani wa tani 200 za samaki, kwa makisio ya chini sana, watavua Tani 2000 kwa mwaka. Bei ya soko kwa kilo ya samaki ni USD2.5. Kwa wanaojua biashara ya sekta hii, kiwango cha uvuvi ni kikubwa zaidi. Kwa maoni haya, mapato yatakuwa Shs.130bn. ambayo sasa hayakusanywi na Serikali;

iii. Katika kuhakikisha kuwa sekta hii ya uvuvi inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla Bandari ya Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar inashauriwa zitenge maeneo ya bandari za samaki *(Fish Ports and Fish Processing Plants)* ili meli zote za uvuvi wa bahari kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula wanapokuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato. (Vyombo vyetu vya ulinzi, vikishirikiana na *TRA* na Mamlaka ya Uvuvi kudhibiti mapato haya). Kwa uamuzi huu, mapato yatakuwa Tshs.3bn. ambayo nayo sasa hayakusanywi na Serikali; na

iv. Uvuvi katika maziwa ya Lake Victoria na Tanganyika, haujadhibitiwa vizuri. Hivi sasa kuna uvunaji haramu wa wastani wa Tani 36,000 kwa mwaka, kama uvunaji huu haramu ukidhibitiwa, Serikali inaweza kujipatia kiasi cha shilingi 45bn kwa mwaka. Uganda baada ya *breeding stock* kupungua mauzo pia yalipungua kwa wastani wa US$30million. Pia uvunaji huu haramu katika maziwa hayo matokeo yake viwanda vyetu vinakosa mali ghafi. Tunataka hatua ya dharura kuikabili hali hii kwa kutumia vyombo vya ulinzi na *TRA* ili kuongeza mapato na ajira. Zoezi hili litaongeza wingi wa samaki hivyo viwanda vya samaki vitaongeza uzalishaji na kodi itaongezeka. Serikali imeshindwa kushughulikia jambo hili hadi leo.

Mheshimiwa Spika, maoni haya Kambi ya Upinzani, sio tu yamepanua wigo wa kodi, lakini pia kwa hatua hizo tutakuwa tumedhibiti uvunaji wa rasilimali zetu ambapo sasa hazivunwi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayotokana na misitu, ni chanzo kingine kikubwa ambacho vile vile mapato yake sasa hayakusanywi na Serikali katika sekta ya maliasili na hasa bidhaa za magogo na mbao. Kutokana na ripoti za kiutafiti kutoka kwa kundi la wahisani na pia asasi kadhaa zisizo za kiserikali, (Kama *TRAFFIC*) (2005/2006), Serikali ilikusanya asilimia 4 tu ya mapato kwa mwaka 2004 yaliyopaswa kukusanywa kutoka katika bidhaa za magogo na mbao. Wanunuzi wakubwa ni China, India na Japan. Katika utafiti huo, katika kipindi cha mwaka 2001/2005, China peke yake ilinunua Cu.mita 18,316 x $150 kwa rekodi za Maliasili Tanzania kwa bei ya wastani wa USD2.7m. sawa na Tshs. 3.5bl. na Cu.mita 108,605 kwa rekodi za Forodha za China, kwa maana hiyo ama kwa ufisadi au vinginevyo Serikali imekosa mapato ya Cu.mita 90,289 x $450 = $40.6m sawa na Tshs.*52.8bn.* utafiti huu ulihusu magogo na mbao zinazotoka Mikoa ya Kusini tu. Taarifa hii inathibitisha Taifa lilikoseshwa fedha kwa kuuza kwa Dola 150 tu wakati bei halisi China ilikuwa Dola 450. Pia kiwango kilichouzwa kimefichwa, huu ni ufisadi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka majibu ya timu ya aliyekuwa Waziri wa Utalii na Maliasili aliposema kuwa ataituma China kwenda kuchunguza jambo hili ndani ya wiki mbili kwani hadi leo hatuna majibu ya timu hiyo. Pia bajeti ya Waziri haionyeshi kama kuna mapato yoyote yatakayopatikana kutokana na chanzo hiki.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri hatua zifuatazo zichukuliwe:-

i. Halmashauri za Wilaya zilizo katika maeneo ambayo bidhaa hizi zinapatikana ziwe mawakala wa kukusanya mapato kutokana na bidhaa za maliasili. Uamuzi huu utapunguza kwa kiasi kikubwa ufisadi uliopo sasa katika Wizara ya Maliasili. Kila Halmashauri inayokusanya kodi ipatiwe gawio kutoka sehemu ya makusanyo;

ii. Mapato yote yakusanywe na *TRA* kwa kutumia stakabadhi za *TRA* kupitia Halmashauri za Wilaya kama ilivyoelezwa hapo juu;

iii. Mtu yeyote atakayekamatwa kwa kutorosha maliasili afilisiwe kwa mujibu wa sheria kama haipo itungwe; na

iv. *TRA* mbali na kukusanya mapato ishirikiane na Bodi ya Mauzo ya Nje kuhakiki bei za bidhaa zetu zinazouzwa nje ili kupata mapato halali ya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hizi mapato ya maliasili misitu yataongezeka kwa asilimia 90 ya mapato ya sasa, makusanyo halisi yatakuwa Tshs 100bn ambazo hazikusanywi sasa.

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na utalii. Serikali inaona kuwa inakusanya mapato kwa wingi hadi kufikia asilimia 16.8% ya pato la Taifa katika Sekta hii. Hata hivyo, Serikali imeshindwa kufikia malengo ya watalii milioni moja kwa mwaka kama ilivyokuwa imepanga. Idadi ya watalii wanaokuja nchini ni wastani wa laki saba (719,031). Isitoshe, Serikali imekuwa ikipoteza mapato kutokana na watalii kulipia

gharama za safari zao na baadhi ya huduma kwa *Tour Operator* huko huko kwao kwa wastani wa USD200-300 kwa mtu mmoja kwa siku. Mtalii anapofika Tanzania, huwa analipa wastani wa USD80-150 tu. Hivyo kuzipunguzia mapato hoteli zetu na kwa maana hiyo na Serikali. Kama watalii hawa wangekuwa wanakuja katika *"Package Tour"* na kuwa tunakusanya wastani wa USD100 kwa siku kwa kila mmoja kwa muda wa siku 7, ukiacha mapato yasiyo ya moja kwa moja, katika eneo hili Serikali ingekusanya kama kodi ya mapato 25% sawa na Tshs 64.5bn ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na uwindaji: Kwa mujibu wa takwimu za Maliasili, kuna vitalu 152. Kwa wakati huu, Serikali inakodisha kwa wastani wa USD7500 kwa mwaka (mara nyingi wamiliki nao hukodisha kwa wenye fedha kwa wastani wa USD100,000 kwa mwaka) Ili kuongeza mapato ya Serikali, Kambi ya Upinzani, inataka hatua zifuatazo zichukuliwe ili kuongeza mapato kama ifuatavyo:-

- Kuwajasirimisha Watanzania vitalu vyote vya uwindaji;

- Ili kupata thamani halisi washauriwe kuingiza Vitalu hivyo katika soko la mitaji kwa kutumia *"eletronic commerce";*

- Kupandisha viwango vya kodi ya Uwindaji; na

- Kutoza asilimia 25% ya mapato yatokanayo na Mtanzania atakayekodisha kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa hatua hizi zinawezekana kwani Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa wanyama wengi zaidi kuliko nchi nyingine za Bara la Afrika, wanyama wanene zaidi na ambao wanaishi kwenye mazingira halisia na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipekee na hivyo kuwavutia wawindaji kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu kutaka kuja na kuwekeza kwenye sekta ya uwindaji. Kwa hatua hii, Watanzania watakuwa wamewezeshwa kumiliki rasilimali zao wenyewe na pia kwa kuongeza viwango vya kodi ya uwindaji makusanyo yanakisiwa kuwa Tshs. 81bn ambayo hayakusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mapato katika Sekta ya Madini. Katika sekta ya madini, kulingana na ukaguzi uliofanywa na Kampuni ya *Alex Stuart*, kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali imepoteza shillingi 1.3 trilioni na hii imetokana na Serikali kutokuwa makini katika kufuatilia nyaraka halali zinazotumiwa na makampuni ya kuchimba madini. Ili kuifanya sekta hii ya madini kuwa na manufaa kwa Taifa na Watanzania wote, hatua zifuatazo zikichukuliwa sekta hii itachangia zaidi:-

i. Kufanya mapitio ya Sheria ya Madini na kupandisha asilimia ya mrahaba toka 3% hadi 5% kwa kuanzia;

*ii.* *TRA* kuimarishwa kiutendaji na kukusanya kodi zote katika sekta ya madini;

iii. Katika mpango wa maendeleo wa kampuni husika, maendeleo ya jamii zinazozunguka migodi yaonekane wazi wazi na kuingizwa katika mpango wa mwekezaji;

iv. Kati ya asilimia 5% za mrahaba utakaotozwa asilimia 2% ibaki katika Halmashauri ya Wilaya/Mji ambamo mgodi upo;

v. Katika masharti ya kuwekeza kwa wageni, ni lazima waingie ubia na Mtanzania au Halmshauri angalau kwa asilimia 10% ikiwa ni pamoja na thamani ya ardhi;

vi. Kuweka sharti ndani ya mikataba na kubadilisha sheria kwamba atakayekiuka mkataba au kusafirisha mali itokanayo na rasilimali za nchi kampuni husika itafilisiwa; na

vii. Kuhakiki madeni waliyokopa wawekezaji ili kupata kiasi halisi walichokopa, ikiwa ni pamoja na *Tax Holiday* kwa lengo la kufuatilia muda wa kusamehewa kodi.

Mheshimiwa Spika, Rais Kikwete aliunda Kamati ya kupitia Mikataba ya Madini mwezi Novemba mwaka 2007 kufuatia Hoja Binafsi ya Buzwagi. Kamati imetoa mapendekezo. Swali la kujiuliza ni je, mapendekezo ya Kamati yamezingatiwa vipi kwenye bajeti hii ya mwaka 2009/2010? Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuiwasilisha ripoti hiyo ndani ya Bunge mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa Serikali imepoteza zaidi ya shilingi 883 bilioni katika kipindi cha miaka 10, kutokana na sheria mbaya ya kodi ya Mapato katika sekta ya madini iliyotungwa na Bunge mwaka 1997. Kupitia *Financial Laws (Miscellenous Ammendments) Act, 1997*, nafuu ya ziada ya uwekezaji asilimia 15 iliwekwa na kuleta upotevu huo wa mabilioni ya fedha za kodi. Sheria hii bado ipo katika sheria za nchi kwa kampuni zote zenye mikataba (*MDA)* kabla ya mwaka 2001. Kambi ya Upinzani Bungeni ilitarajia kuwa Serikali ingefuta sheria hii na kuangalia uwezekano wa Makampuni ya Madini kulipa fedha hizi kwani nafuu haikuwa na ulazima wowote na haimo katika kanuni za kodi. Kambi ya Upinzani inategemea kukusanya mapato haya kwa kiasi cha shilingi 88.3bn.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inapendekeza kuwa msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta kwa Kampuni za Madini ufutwe. Mwaka 2007/2008, Serikali kupitia msamaha huu, haikukusanya shilingi 59 bilioni kutoka kampuni sita za madini. Waziri wa fedha amesema kuwa wale ambao hawatasamehewa, ni wale ambao watawekeza kuanzia mwaka 2009 July, hivyo ni wazi kuwa wale wa zamani hawatolipa hata sentí moja, hivyo kulikosesha mapato Taifa na kupunguza faida ya ukuaji wa sekta ya madini katika uchumi. Kambi ya Upinzani, inataka kuwa msamaha wa kodi ya Ushuru wa Mafuta kwa kampuni za madini ufutwe mara moja. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iondoe misamaha ya kodi kwa mafuta wanayotumia wazalishaji wa makampuni ya madini katika migodi mikubwa na ya kati na kuanzisha mfuko maalumu wa kufidia punguzo la mafuta yanayopelekwa vijijini.

Aidha, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla juu ya hali ya uchimbaji wa madini mbalimbali katika machimbo ya Kabanga Nikel yaliyoko Mkoani Kagera, Wilaya ya Ngara na uhalali wa wachimbaji walioko kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni, inaona kuwa Serikali inafanya mzaha na umuhimu wa sekta ya madini katika mapato ya Serikali na kwamba kitendo cha Waziri kutokuzungumzia chochote juu ya Mapendekezo ya Kamati ya Rais na utekelezaji wake, ni dalili tosha kuwa Serikali inatilia maanani zaidi maslahi ya wawekezaji kuliko ya Watanzania. Serikali ituambie kwa nini wawekezaji wa madini wanaogopwa?

Mheshimiwa Spika, mapato kutoka madini ya vito. Taarifa mbalimbali za kitafiti zinaonesha kuwa Tanzania inapoteza mapato mengi sana katika madini ya vito kwa sababu ya uzembe na ufisadi.  Kwa mfano, katika soko la dunia, mauzo ya Tanzanite mwaka 2005 yalikuwa na thamani ya Dola za kimarekani 400m. Hata hivyo, rekodi ya Tanzania ni Dola 16m tu. Tuna taarifa kuwa Kenya ilipata tuzo kwa kusafirisha Tanzanite nyingi duniani wakati hawana Tanzanite. Kwa kutumia vito vyetu vya aina mablimbali kama vile Tanzanite, Alexadrite, Safaya, Ruby za aina nyingine zote, Serikali ingeweka usimamizi madhubuti tungeweza kulipatia taifa fedha kwa ajili ya kuendesha uchumi na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi kuliko hali ilivyo hivi sasa kuwa wananufaika zaidi wawekezaji wakubwa tu huku wananchi wa maeneo yenye vito hivyo wakibakia kwenye lindi la umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ingekubaliana na ushari wa Kambi ya Upinzani, Serikali ingepitia upya kabisa mwenendo mzima wa biashara ya madini haya ili kuwa na chanzo kimoja tu cha mauzo. Udhibiti huu ungeipatia Serikali mapato ya jumla ya Tshs. 150bn. ambayo hayakusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Mapato katika Kodi nyinginezo. Misamaha ya Kodi, eneo lingine ambalo tumekuwa tukipoteza fedhanyingi sana ni hili. Kama ilivyo katika taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, inakadiriwa kuwa takribani shilingi 819.9 bilioni zilitolewa kama misamaha ya kodi katika mwaka wa fedha unaomalizika. Aidha, hali ya misamaha ya kodi kwa upande wa Zanzibar ilikuwa ni ya kutisha kwani mwaka 2008/2009, *TRA* ilikusanya kiasi cha shilingi 28.1 bilioni huku misamaha ya kodi mbalimbali ikifikia shilingi 18.3 bilioni, hili ni jambo la ajabu sana kwani misamaha hii ukiondoa ile inayolenga mashirika na madhehebu ya kidini, haiwanufaishi wananchi masikini wa taifa hili. Ili kuongeza mapato yetu ya ndani, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ipunguze misamaha ya kodi kwa asilimia 50%. Uamuzi huu utaweza kuongeza mapato na kuwa Tsh. 409.95bilioni ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kodi katika *Posho "Allowances'*. Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria Na.11 ya mwaka 2004, Kifungu cha 7(1) na (2), kila atakachokitoa mwajiri itabidi kikatwe kodi isipokuwa kama mfanyakazi atatumia fedha zake na mwajiri akamrudishia. Kwa mujibu wa sheria hii, posho zote za warsha, semina,

makongamano, mikutano na vikao zinapaswa kukatwa kodi ya mapato. Hii pia inajumuisha posho wanazopata Waheshimiwa Wabunge kutokana na vikao hapa Dodoma na Dar es Salaam. Sheria ya Kodi ikirekebishwa ili kutoza kodi mapato haya kwa kiwango cha *VAT* yaani 18%., hatua hii pia ingelenga kupata manufaa yafuatayo:-

(a) Mifuko ya Pensheni itapata wanachama zaidi; na

(b) Kodi ya Serikali ambayo ni ya uhakika (*P.A.Y.E.* itapanda maradufu kwani *Employment Allowance* haitozwi kodi).

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu Serikali ingepata mapato ya Tshs.6.07bn ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya hisa za Serikali. Bado kuna makampuni ambayo Serikali ina hisa ambayo sasa ingefaa hisa hizo kuuzwa kwa wananchi lakini Serikali ipo kimya katika hili. Kwa mfano, ni kwa nini Serikali haiuzi hisa zake za kampuni ya simu ya *CELTEL, NBC, BP*, Kilombero Sugar n.k katika soko la hisa? Kwa nini haiuzi hisa zake ili kupata mapato ya kuendesha uchumi? Iwapo Serikali ingeuza hisa zake ingeweza kupata fedha kulipia na kutekeleza mipango mingine ya maendeleo. Soko la Hisa la Dar es Salaama lapaswa kuboreshwa kwa kuingiza kampuni nyingi zaidi ili kumilikisha wananchi hisa za makapuni na kufanya biashara ya hisa kuwa nzuri na yenye kuweza kutabirika. Kwa kuuza hisa za makampuni hayo kama tulivyoainisha mwanzo tungekusanya Tshs.475 bilioni.

Mheshimiwa Spika, mapato kutokana na Bandari ya Mtwara na Tanga. Eneo lingine ambalo bado halijatumiwa vizuri ni la kuuza mauzo nje ya nchi na hasa nchi jirani *(Bonded Goods).* Kama bandari ya Mtwara ingejengewa maghala ya kuhifadhia mazao na bidhaa kwa kufanya mauzo ya bidhaa zetu za viwandani kama vile cement na mifugo, mchele na bidhaa nyingine, ingesaidia. Nchi ya Comoro, ambayo matumizi yao ni saruji tani 70,000, mchele tani 40,000 kwa mwaka na ng'ombe ni 4,000 kwa wiki, inaitegemea sana Tanzania katika vyakula na vifaa vya ujenzi. Aidha tutasukuma uuzaji wa bidhaa zetu nje kama Muhogo, korosho, ufuta na samaki. Uimarishaji huu utaweza kutuingizia kiasi cha shilingi 4 bilioni kutokana na kodi peke yake ambayo sasa haikusanywi.

Mheshimiwa Spika, kodi itakayotokana na Leseni za Madereva. Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa mfumo wa Leseni za Madereva uboreshwe kwa kutoa leseni mpya kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya komputa. Leseni hizi zitakuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa zote muhimu za madereva. Hii itasaidia kupunguza uhalifu na hasa ajali za barabarani na pia itakuwa ni sehemu ya kitambulisho. Mradi huu uendeshwe kwa utaratibu wa *PPP*. Kwa makisio ya chini, Madereva laki mbili na nusu mwaka huu wa fedha na ada ya leseni kuwa Shs.50,000, tutakusanya jumla ya shilingi 6.25bn ambazo sasa hazikusanywi.

Mheshimiwa Spika, mapato kutokana na kuuza ndege ya Rais. Kutokana na dhamira yetu toka mwaka 2003 kwamba ununuzi wa ndege ya Rais ni anasa na gharama zisizo na msingi. Kwa sasa Serikali inatumia Shs.6 milioni kwa saa ya kuruka ndege hii.

Kambi ya Upinzani bado inaendelea na ushauri wake kwamba ndege hii kama alivyofanya Rais wa Ghana Bw. John Kufouri iuzwe kwa mnada. Kwa uamuzi huu Serikali itapata mapato ya Tshs 30 bilioni. Pia hatua hii itaiwezesha Serikali kupata fedha za kutengenezea ndege zake.

Mheshimiwa Spika, kuwarahisishia Watanzania kwa kuifanya Mamlaka ya Manunuzi nchini ijitegemee kwa kutumia utaratibu wa manunuzi wa mtandao *(e-Procurement)* kwa ajili ya kusajili makampuni katika ngazi za Wilaya, Mkoa hadi Taifa na nje zinazotoa huduma kwa Serikali. Kuiboresha mamlaka hii ili isaidie kupunguza rushwa katika manunuzi na kuipunguzia Serikali bei ya manunuzi kwa wastani wa si chini ya 15% ya manunuzi yake yote. Njia hii itatuingizia mapato kiasi cha shilingi 250bn .

Mheshimiwa Spika, ushauri huu uliotolewa na Kambi ya Upinzani, kama Serikali ingekubali kuufanyia kazi kuhusu sera ya mapato, yangeipatia Serikali jumla ya mapato ya ziada ya Tsh. 1,847.07bn. Ushauri wa Mapato haya yote ni kutokana na kuboresha vianzio vilivyopo na kubuni vipya ambayo Serikali haikuviona.

MheshimiwaSpika, muhtasari, wa ushauri wetu juu ya vyanzo vipya vya mapato ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

**VYANZO VYA MAPATO**

| | Maelezo | Makusanyo(Tshs. Billioni) |
|---|---|---|
| 1 | Hisa za Serikali | 45.00 |
| 2 | Ada ya Leseni-Uvuvi bahari Kuu | 9.50 |
| 3 | Tozo la Mrahaba-Uvuvi Bahari Kuu | 130.00 |
| 4 | Fish port and Processing | 3.00 |
| 5 | Bidhaa za misitu | 100.00 |
| 6 | Vitalu vya uwindaji | 81.00 |
| 7 | Kodi isiyokusanywa katika madini | 88.30 |
| 8 | Ushuru wa mafuta makampuni 6 madini | 59.00 |
| 9 | Mapato ya madini ya Vito | 150.00 |
| 10 | Misamaha ya kodi ya mapato | 409.95 |
| 11 | Kodi katika posho | 6.07 |
| 12 | Mauzo ya hisa za Serikali | 475.00 |
| 13 | Bandari ya Tanga na Mtwara | 4.00 |
| 14 | Leseni za Madereva | 6.25 |
| 15 | Mauzo ya Ndege ya Rais | 30.00 |
| 16 | Electronic Procurement | 250.00 |
| | JUMLA | 1,847.07 |

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri na mapendekezo yetu ya mapato, tungeweza kukusanya jumla ya Tshs. 7,091.138bn au (7.091 trilioni) kama mapato ya ndani. Makusanyo haya yangekuwa ni ziada ya makusanyo ambayo Serikali imepanga

kuyakusanya kwa kiasi cha Shs. 5,234.068bn au (5.234 trillion) tofauti ya zaidi ya Shs.1,857.07bn au (1.857 trilioni) na bila kumuumiza mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia kuwa nchi yetu itapata misaada na mikopo kutoka nje kama jinsi ambavyo imeainishwa katika Makadirio ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010, Makadirio ya Mapato ya Bajeti hii, yangefikia jumla ya Tshs.10,273.086bn au (10.27trillion).

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu kodi mbalimbali. Baada ya Kambi ya Upinzani kuainisha vyanzo vipya mbalimbali vya kodi ambavyo havimuumizi mwananchi wa kawaida na pia baada ya mapato ya Serikali kuongezeka kutokana na vyanzo hivyo, hivyo basi tunaitaka Serikali ichukue hatua zifuatazo ili kuweza kuinua uchumi na kukuza ukuaji wa pato la Taifa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mishahara kwa watumishi wa Serikali. Kutokana na kuongezeka kwa mapato ya ndani, Kambi ya Upinzani inashauri kiwango cha chini cha mshahara wa wafanyakazi wa Umma kiwe Tshs 315,000 kwa mwezi, kwa ngazi nyingine mshahara ungepanda kwa asilimia ambayo italeta uwiano baina ya kipato cha chini na cha juu. Ufafanuzi wa kina utatolewa na Waziri Kivuli wa Utumishi wa Umma. Kiwango hiki hakitatozwa kodi ili kuweza kumfanya mtumishi wa ngazi ya chini aweze kumudu gharama za maisha, japo hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, Kilimo na Nishati ni vipaumbele vyetu vikuu katika mpango mzima wa kuinua uchumi na kuongeza kipato kwa Watanzania walio wengi. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, ni kuwa Serikali imejikita zaidi katika hatua ya awali kuwa na shule nyingi, idadi kubwa ya wanafunzi, jambo ambalo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Kutokana na kazi kubwa iliofanywa na Kambi ya Upinzani ya kutafuta mapato zaidi, muono wetu ni kuimarisha hatua iliyofikiwa kwa kuelekeza matumizi yetu katika kuboresha viwango vya elimu ili kuwa na elimu bora. Hivyo, tunashauri kuwa tuhakikishe mkazo mkubwa unawekwa katika kuwaelimisha Walimu katika ule mtindo wa zamani. Pia Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vyote vya elimu kama vitabu, madaftari, kalamu n.k. Hatua hii itawawezesha wananchi kuweza kumudu gharama za kusomesha watoto wao na kuliendeleza Taifa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani Juu ya Utaratibu wa Mgao wa Kutumia Fedha. Kama tulivyoshauri katika hatua mbalimbali za maoni yetu, katika kutekeleza mipango ya Serikali na kuwafanya watekelezaji wa mipango hiyo waweze kutekeleza vyema, utaratibu wa “*cash budget*” haufai. Utaratibu uliokuwa unatumika zamani wa “*Warrant system*”urudiwe. Aidha, fedha badala ya kutolewa kwa mtindo wa kila mwezi, utaratibu wa kutoa fedha kwa kipindi cha miezi minne minne utumike.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vipaumbele tulivyo shauri, tumegawa mapato ya bajeti hii mbadala kama ifuatavyo:-

Tshs.

Billion

| | | |
|---|---|---|
| Kilimo | 12% | 1232.7703 |
| Nishati | 9% | 924.5777 |
| Elimu | 22% | 2260.0789 |
| Miundombinu | 20% | 2054.6172 |
| Afya | 12% T. | 1232.7703 |
| Maji | 10 %. | 1027.3086 |
| Mawasiliano, sayansi na teknolojia | 5%. | 513.654 |
| Matumizi mengineyo | 10% | 1027.3086 |

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani juu ya sura ya bajeti

| Mapato: | shilingi bilioni |
|---|---|
| Mapato ya Ndani | 7,091.138 |
| Mikopo na Misaada ya Nje Ikijumuisha HIPC/MDRI | 3,181.948 |
| JUMLA YA MAPATO YOTE | 10,273.086 |
| Matumizi | |
| Matumizi ya Kawaida | 5,650.1973 |
| Deni la Taifa | 1,523.024 |
| Wizara | 2,542.588 |
| Mikoa | 101.7035 |
| Halmashauri | 1,412.549 |
| Matumizi mengine | 71.197 |
| Matumizi ya Maendeleo | 4,623.086 |
| Fedha za Ndani | 1,441.138 |
| Fedha za Nje | 3,181.948 |
| JUMLA YA MATUMIZI YOTE | 10,273.086 |

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchanganuo huo, tofauti za kimsingi za hoja ya Waziri wa Fedha na Ushauri wa Kambi ya Upinzani ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli utaiwezesha Serikali kutumia fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo kwa asilimia 31.17%. Hivi sasa bajeti ya maendeleo ya Serikali inategemea wafadhili kwa asilimia 100%.

(b) Ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli utaiwezesha Serikali kupunguza Bajeti tegemezi. Mikopo na misaada toka kwa wahisani ni asilimia 30.97% ya bajeti nzima kivuli badala ya utegemezi wa asilimia 33.45% uliowasilishwa katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mlinganisho wa kati ya Ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti yake kivuli na Sura ya Bajeti ya Serikali ni kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho I.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli niliyowasilisha, ni kuchochea ukuaji wa uchumi, kuondokana na bajeti tegemezi kama Taifa na kuwa na Taifa lililoelimika lenye utawala unaoheshimika. Katika hotuba yetu, nimeonyesha wazi wazi kuwa tunazo fursa kubwa za kupata mapato ya ndani. Tatizo ni mtazamo wa kifikra "*Mind Set*". Changamoto kubwa tuliyonayo kama Taifa ni kwa viongozi kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wengine bila kujali itikadi za kisiasa, ili kwa pamoja tuwaondolee umasikini Watanzania waliokalia rasilimali zinazozidi mahitaji yao. Lazima sote tujiulize kwa nini wageni na wajanja wanatajirika lakini wakulima na wafanyakazi wetu ni masikini? Taifa hili ni letu, tusemezane, tujadiliane hatimae tusonge mbele.

Mheshimiwa Spika, tuliyosema yanawezekana, yanahitaji viongozi na watumishi kuweka maslahi ya Taifa mbele. Raslimali tulizonazo zinatosheleza kama zitasimamiwa na kutumika kwa maslahi ya watu wetu. "TUNAHITAJI KUZINDUKA".

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, pamoja na shukrani zake, inapenda kutoa masikitiko yake kuwa imelazimika kutoa hotuba hii kwa dakika 40 tu. Mheshimiwa Waziri alitumia saa nne kutoa hotuba zake. Hali hii imewanyima Watanzania kufaidi bajeti mbadala kama ilivyo kwenye Hotuba hii kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kukushukuru na kuwashukuru waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa kunisikiliza. Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa masuala ya Fedha. Napenda kuwahakikishieni kwamba hotuba yenye maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi na Hotuba ya Kambi ya Upinzani zote zitatoka zilivyo ndani ya *Hansard* ya Bunge. Kwa hiyo, kwa ajili ya rejea hakuna matatizo. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, ninaorodha hapa ya wachangiaji 55 na niseme tu, si vema kuendelea kuleta majina kwa sababu tunazo siku tatu na nusu ili tuweze kuhitimisha kwa kura za *rollcall*, ndivyo itakavyokua. Nitawataja watano wa mwanzo ili wajiandae; kwanza Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, atafuatiwa Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lucas Selelii na baada ya hapo ni Mheshimiwa John Cheyo. Kwa sasa, namwita Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa ajiandae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niwe mchangiaji wa kwanza kwenye hoja iliyombele yetu.

Kwa niaba ya wananchi wa Chunya, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake ya tarehe 10 ya kunusuru uchumi wa nchi yetu. Vilevile napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote kwa maandalizi mazuri kwa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inaonyesha kwamba trilioni 6.7 ni matumizi ya kawaida na trilioni 2.9 ni matumizi ya maendeleo. Sasa katika hiyo 6.7 asilimia 70 inaenda kwenye manunuzi, trilioni 2.9 asilimia 100 inaenda kwenye manunuzi. Sasa inaonekana kwa wastani katika ile trilioni 9.5 asilimia 80 ya fedha hizo zinakwenda kwenye manunuzi. Ni bahati mbaya huyu mdudu anaitwa manunuzi hajadhibitiwa vyema kwa kipindi kirefu sana. Tulipokuwa na *Central Tender Board*, tukabadilisha Bunge likatunga Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2001 baadaye likatunga Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 lakini muda wote huo Wizara ilikua inahusika na manunuzi hapakua na Kitengo cha Sera.

Vilevile ilikua imegawanyika *PPRA* inayodhibiti manunuzi iko Wizara ya Fedha lakini manunuzi yalikua Wizara ya Miundombinu. Bahati nzuri mwaka jana Serikali imeamua kutoa Kitengo cha Manunuzi kukiweka Wizara ya Fedha na safari hii kwenye Bajeti hii Wizara ya Fedha imeunda Kitengo cha Sera kwenye Wizara ya Fedha. Huo ni mwenendo mzuri sana na naipongeza sana Wizara. Sasa Wizara ikamilishe kujipanga vizuri katika kudhibiti maununuzi ya umma, ichukue na Kitengo cha *Government Stores* kirudi Wizarani na pia *National Board for Materials Managament* nayo irudi Wizarani ili Wizara iweze kudhibiti hii asilimia 80 ya matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kitengo cha Sera kuwa Wizarani, pia mwaka 2006 Wizara iliajiri Wataalam wa Fedha na ikawafundisha vizuri na ikawapeleka kwenye Halmashauri ili kuweza kudhibiti matumizi ya fedha huko kwenye Halmashauri na mwenendo wa matumizi kwenye Halmashauri inaonekana miundo ni mizuri na Halmashauri nyingi zinapata hati safi. Sasa naiomba Wizara vilevile iajiri wataalam wa manunuzi, iwape mafunzo na iwapeleke kwenye Halmashauri huko kwenda kudhibiti matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kidogo kuhusu makampuni ya madini ambayo mengine yamefutiwa msamaha wa kodi ya mafuta na mengine yanasema Serikali itaanza kujadiliana nayo ili kutoa kipengele hicho kwenye mikataba. Kwa kumbukumbu yangu, ni kwamba msamaha wa kodi kwenye mafuta kwa makampuni ya madini ulikuja baada ya mikataba. Ulikuja kwa tangazo la Serikali, kwa hiyo naiomba Serikali itoe tangazo la kufuta misahama hiyo kwani makampuni haya yameshafaidi fedha hizi kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali imetoa fedha kuweza kuiokoa Kampuni ya *Artmus* ambayo imefilisika ili iweze kuendeleza kuleta umeme kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, imetoa kiasi cha shilingi bilioni 7.0. Hili ni wazo zuri sana na naipongeza sana, ila naiomba Serikali isiikopeshe *Artmus* maana kuja kulipa mkopo watakuwa wanasema hatujapata faida mwaka huu, hatujapata faida mwaka huu kwa hiyo hawarudishi mkopo huo. Kwa hiyo,

naomba Serikali inunue hisa kwa *Artmus* na akabidhiwe *TPDC,* hilo litakuwa ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niipongeze Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi bilioni 12.5 kwa ajili ya barabara ya kutoka Mbeya kwenda Chunya hadi Makongorosi, mwaka jana Serikali ilitenga shilingi bilioni sita, mwaka huu imetenga shilingi bilioni 12.5, naipongeza Serikali. Lakini nina masikitiko, barabara hii iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi na Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la uzinduzi mwaka jana mpaka leo hakuna hata kilometa moja ya lami iliyowekwa pamoja na hela zote hizi kutengwa. Mwezi wa nne Kampuni ambayo ilikuwa inapewa barabara hii imejiondoa kwenye barabara hiyo na Serikali nayo ikavunja mkataba, sasa kwa kuwa unapovunja mkataba hauendi kwenye *competitive* tena, naiomba Serikali itutangazie mkandarasi atakuwa nani. Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu atakapokuwa anatoa makadirio yake tarehe moja au mbili atuambie ni nani mkandarasi wa kuanza ujenzi wa barabara hiyo ya kutoka Mbeya kwenda Chunya hadi Makongorosi, wananchi wana hamu sana na barabara hiyo na wameisubiri kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niongelee umeme kutoka Makongorosi hadi Lupa na napenda kuishukuru sana Serikali na kuipongeza sana kwa kutenga kiasi cha fedha cha kutoa umeme kutoka Makongorosi kwenda Lupa na fedha hizo zimetolewa tayari ziko *TANESCO*, naiomba sana *TANESCO* itangaze haraka mkandarasi atakayetoa umeme kutoka Makongorosi kwenda Lupa ili wananchi wa Vijiji vya Mkola, Upendo, Mtande, Mamba, Kisalase na Lupa yenyewe wajiweke tayari kupokea umeme huo kutoka Makangorosi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba ninukuu, ukurasa wa 28 anasema hivi:-

*"Kuimarisha udhibiti wa bidhaa za mafuta ya petroli ikiwemo kuhakikisha kuwa mita za kupitishia bidhaa hizo zinafanya kazi vizuri wakati wote, kushirikiana na Mamlaka husika katika kudhibiti uchanganyaji wa dizeli na mafuta ya taa na kuhakikisha kuwa mafuta yanayopitishwa hapa nchini kwenda nchi jirani hayauzwi katika soko la ndani."*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu suala hili, tatizo kubwa ni kwamba Serikali kwa nia njema kabisa imepunguza ushuru wa mafuta ya taa kwa lita moja, ambapo ni shilingi 52, wakati mafuta ya dizeli kwa lita moja ni shilingi 314, mafuta ya petroli kwa lita ushuru wake ni shilingi 339. Hapa ndipo kuna tatizo na wanaohusika ni makundi mawili. Kundi la kwanza ni makampuni ya mafuta yote labda kasoro moja au mawili. Ukiangalia wanavyoagiza mafuta huko nje wanajaza matanki na matanki ya mafuta ya taa ili vituo vyao vilivyosambaa nchi kote viweze kuchanganya mafuta ya taa na dizeli au mafuta ya taa na petroli. Nimesema, hapo msafi labda mmoja au wawili. Lakini wengine wote wanahusika na biashara hii ya kuchanganya mafuta ya taa pamoja na dizeli au petroli.

Mheshimiwa Spika, kundi la pili ni wamiliki wa vituo vya mafuta. Ukiendesha gari kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kutoka Kibaha mpaka Mlandizi urefu wake ni km 20, lakini vituo vya mafuta pale viko 27 na vituo vyote hivi vimejengwa kuwa na kituo mbele lakini nyuma huko kuna boma kubwa linamaukuta marefu kuliko *Fort Jesus* na lina geti limefungwa mchana kutwa sasa huko ndiko kuna pamp za kuchanganya mafuta. Huko ndiko wanakochanganya kama ni dizeli asilimia 70 ya dizeli na asilimia 30 ya mafuta ya taa, kama ni petroli asilimia 70 na asilimia 30 ya mafuta ya taa. Mimi nawaomba *EWURA*, hawa watu wameomba leseni ya kuuza mafuta, hili boma la huko nyuma la nini? Vinginevyo wanyang'anywe leseni ili wawanusuru Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kitendo hiki cha kuchanganya mafuta kina mambo matatu, la kwanza wanaikosesha Serikali mapato yake kwa kiasi kikubwa sana na wanatengeneza faida kubwa sana. Hivyo, kwa kuikosesha mapato yake wanamkosesha mwananchi wa Tanzania huduma za jamii kama barabara, maji na afya wao wakipata faida haramu. Lakini vilevile kwa kuchanganya mafuta hayo wanawaharibia Watanzania magari yao. Watanzania hawa wengi magari yao ni ya mkopo gari ambalo anategemea limsaidie miaka mitano, sita au kumi, unakwenda kumwekea mafuta ambayo yameshanganywa na mafuta ya taa!

Mheshimiwa Spika, injini iliyotengenezwa kwa kutumia petroli itadumu kwa kutumia petroli. Injini za ndege ambazo zimeundwa kwa kutumia mafuta ya taa, zitadumu kwa mafuta ya taa. Sasa unapochukua mafuta ya taa na kuweka kwenye injini ya kutumia petroli, unaua gari la Mtanzania huyu, maskini linatumika miaka miwili limekufa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba, hawa wanaotengeneza faida kubwa sana kwa kuchanganya mafuta ya taa na petroli na dizeli, wamuogope Mtanzania ambaye wanamfanyia dhuruma hii. Kama hawawezi kumwogopa Mtanzania huyu basi naomba wamwogope Mwenyezi Mungu. Huu ni ufisadi, wamwogope Mungu na kama wanalewa na faida kubwa wanayopata hata Mungu hawataki kumwogopa, naomba Serikali iweke rangi kwenye mafuta ya taa ili mtu yeyote anatakayechanganya mafuta aweze kuonekana na tuweze kuwanusuru Watanzania katika janga hili la uchanganyaji wa mafuta ya taa na petroli na dizeli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na kwa niaba ya wananchi wa Lupa na Wilaya ya Chunya, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na wakati huo huo nitoe masikitiko yangu, kwa bahati mbaya vitabu ulivyovieleza mpaka sasa havipo. Nimetoka hapa, nimekwenda kwenye *pegion hall,* sijavikuta. Kwa hiyo, nitaongea kwa takwimu za vitabu vilivyopita. Lakini hii ni dhahiri kabisa kwamba kwa namna hii Bunge lako litashindwa kuchambua vitabu vizuri, kwa hiyo, wakati ujao tunaomba wawe makini zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwanza sitaunga mkono hoja hii na nitaeleza sababu ambazo zinanifanya nisiunge mkono. Kwanza kabisa, nianze na Kitabu cha Hali ya Uchumi, ukurasa wa 76 na naomba uniruhusu ninukuu na nitaomba maelezo ya kina kwa Mheshimiwa Waziri siku ya kujibu. Sitasoma yote nitasoma sehemu kwa sababu ni ndefu kidogo. Mheshimiwa Waziri anazungumzia deni la ndani na anasema:-

*"…Kati ya deni hilo, asilimia 99.6 ni dhamana za Serikali wakati asilimia 0.4 ni madeni mengine ya Serikali. Ongezeko hilo lilitokana (na hapa ndipo nataka kukazia), kujumuishwa kwa madeni ya akaunti ya kulipia malimbikizo ya madeni ya nje (EPA) na Hatifungani maalum za Serikali".*

Mheshimiwa Spika, nitataka Waziri anieleze kwa kina haya malipo yaliyojumuishwa, ya *EPA* ni yapi na yachambuliwe kabisa kwa kina kwa majina ya watu waliolipwa kwa sababu kwa taarifa ya *Arnest and Young* taarifa ya Aquarly, taarifa ya Lansard; taarifa zote zilionyesha kwamba madeni haya, akaunti zake waliohusika hawapo. Tunajua Kamati ya Serikali iliyokuwa inafanya uchunguzi nje haijamaliza kazi na kama imemaliza Waziri atoe taarifa Bungeni vinginevyo hapa kuna kiini macho kizito na tutataka majibu ya kina vinginevyo Bunge lako litakuwa linachezewa vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ninataka nilizungumzie ni suala linalohusu kuondolewa kwa misamaha ya kodi kwa *NGO's* na Madhehebu ya Dini. Katika hili, naomba nitangaze kwanza maslahi yangu, wewe mwenyewe unafahamu kwamba nahusika na *NGO's* kadhaa, ile unayoijua ya *CCBRT* ni moja tu lakini nipo kwenye *NGO's* nyingi lakini nimefanya kazi katika Baraza la Maaskofu kama Katibu Mkuu, nyingi za Hospitali hizi nilizijenga mwenyewe. Kwa hiyo, ninapozungumza, ninazungumza kitu ninachokifahamu, sina maslahi binafasi ya fedha kama inavyotakiwa na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ningependa kabisa Waziri anihakikishie kile ambacho amejaribu kukifafanua kwenye *press conference*, jana au juzi akieleza misamaha iliyoondolewa kwamba haihusiani na huduma za jamii kwa maana ya hospitali, shule na miradi mingine ya jamii. Sasa kifungu alichokifuta ni kifungu cha kumi ambacho naomba nikinukuu, kwenye *Finance Bill* ni Kifungu cha 28, ninaharakisha kwa sababu iko kwenye hotuba yake na sina namna ya kufanya bila kurejea kwenye *Finance bill*, anasema:-

*"By deleting item 10 and substituting for it the following (akasoma kifungu cha kumi), the importation of local purchase by registered religious organisations of goods and solely for worship."*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maana nyingine amefuta zile *exemption* zote zilizowekwa na kwa bahati mbaya nilishiriki sana katika Sheria ya awali ambayo huduma zote za jamii zilipewa *zero rating* katika *VAT* pamoja na ushuru wote unaohusika. Sasa unapofuta hizi maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, nimefanya kazi kwa *weekend* nzima kutafuta *list* ya hospitali zote zilizoko vijijini kama mfano tu wa huduma za jamii. Ninatoa mfano mdogo tu wa hospitali hizi nikianza kwa mfano Jimboni kwangu Hospitali Bugerik Karatu, Kansei, Endara, Kilimamoja, Mbulumbulu, Endeshaek na nyinginezo. Nikienda Iringa, Ihimbo, Ipalamwa, Idete, niende Mkoa wowote ule ambao utaniambia niende, Tanga Mlalo *Dispensary*, Kiberashi, niende Kagera Nyabugere *Dispensary* iko Biharamulo na Mikoa mingine; hospitali hizi ziko vijijini na hakuna hospitali yoyote ya Serikali kwenye maeneo haya, tunapofuta, hao Watanzania ambao sasa wanapata huduma hizi, tutawapelekea nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe kwenye Bodi moja inaitwa CBM, tunakodisha ndege kupeleka huduma za hospitali kwenye maeneo ambayo Serikali haifiki kabisa. Hospitali moja iko hapa jirani, Berege, pale tunatoa huduma ya macho lakini tunafanya maeneo karibu yote na tunakwenda mpaka Ilembula kule Iringa. Tunapofanya hivi hatupati wala hatutozi hata senti moja, huduma zinatolewa bure, ndege tumelipia. Sasa tunajiuliza, unapoondoa misamaha hii maana yake mfadhili wa nje anayetupa misaada tunataka sasa ailipe Serikali ya Tanzania kodi. Ni kwa nini mlipa kodi wa Ulaya ambaye anawasaidia Watanzania wetu bure tunaendelea kumtoza kodi hapa? Hilo, napenda Waziri atupe ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshtuka na taarifa ya jana ya ufafanuzi ya Waziri akisema kwamba wako ambao wametumia vibaya, akatoa mfano kuna aliyenunua magari akaenda kufanyia biashara, kuna aliyenunua *cement* kujenga kanisa akaenda kufanya kitu kingine. Nataka kumuuliza Waziri alieleze Bunge hili, kama ana watu hawa, hata kama ni Askofu, kitu gani kimemzuia asimkamate Askofu ambaye anavunja sheria ya nchi hii? Kama ni kweli wametumia vibaya misamaha hii, ni kwa nini hawa walioharibu hiyo misamaha wasishughulikiwe badala ya kuumiza Mashirika yote ambayo yanalisaidia Taifa hili kwa hisani mahali ambapo Serikali yetu imeshatangaza kila wakati kwamba Madhehebu ya Dini ni wadau wakubwa wa huduma katika kuimarisha huduma bora kwa kila Mtanzania. Je, leo tunatangaza kwamba ushirikiano wetu huu, agizo na maelekezo ya Serikali na kauli za Serikali za kushirikiana na wadau mbalimbali zimefutwa au zimefanywa nini?

Mheshimiwa Spika, kama ni kweli wameingiza Serikali hasara, kwa sababu hakuna msamaha ambao unaofanyika bila kwanza barua ya DC kupatikana, bila *TRA* kutoa kibali chao na misamaha yote iko *recorded* Serikalini, ni kwa nini hawa watu wa Serikali wasichukuliwe nao hatua? Waziri kabla hajafuta, atuambie ni wangapi wamekamatwa kwa kuiingizia hasara Serikali kwa watu walioko kwenye Serikali yake kabla hajaondoa misamaha katika kodi. Mimi nitapenda ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, Waziri pia atuambie anapofuta, ni kiasi gani kwanza Madhehebu ya dini wanatoa katika eneo la huduma, naachia eneo la ujenzi wa Makanisa na Mambo ya ndani ya Kanisa, ni kiasi gani cha fedha zinaingizwa kwa mwaka nchini kusaidia Taifa hili ili kulinganisha ni kiasi ambacho sasa anafuta, kama ni kidogo, basi kinaweza kufutwa, lakini kama ni kikubwa, hasara hiyo tutaifanyaje? Vile vile atuambie, anajadiliana na makampuni ya madini lakini wadau wa Madhehebu ya Dini na NGO's

hakuwaita kujadiliana nao kabla hajafuta. Bila kupata maelezo ya suala hilo, mimi siwezi kukubaliana kabisa na bajeti hii na sitaiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nigusie eneo lingine ambalo kidogo limenitisha. Tunazungumzia sana “Kilimo Kwanza” kama ni kitu kipya lakini mimi nashtushwa kwa sababu ninaliona eneo hili linafanywa kisiasa. Kilichoko ni maneno ya kisiasa zaidi kuliko ya bajeti. Bajeti si maneno wala ya Mheshimiwa Waziri wala ya Rais, bajeti ni takwimu zilizopo katika vitabu. Sasa kwa kuwa siioni kwenye vitabu, nataka Waziri anihakikishie baadaye, hizi takwimu za kukifanya kilimo kiwe kwanza, kisiwe pili, tatu na nne, ni zipi? Nikichukua mfano; mwaka jana tulikuwa na bilioni 513 kwa ajili ya kilimo, mwaka huu tuna bilioni 667. Sasa, ni kweli kimahesabu imeongezeka, lakini ukienda kwenye *percent* mwaka jana tulikuwa na asilimia 7.1 na mwaka huu ni 7.0, maana yake tumepungua. Je, tumekwenda kwanza au tumerudi chini. Sasa hilo “kwanza” maana yake nini? Nilitegemea “kwanza” ningeiona kwenye maandishi.

Mheshimiwa Spika, najua kuna *ASDP* na kadhalika lakini hapo hapo, natoa *comment* ya *ASDP* yenyewe. *ASDP* bajeti ya mwaka 2006 – 2013, tulilenga kutumia trilioni 2.7, leo ni mwaka wa tatu, katika miaka mitatu ya trilioni 2.7, tumetumia bilioni 578.6 tu ni sawa na asilimia 21.4 ya fedha tulizopaswa kutumia katika miaka mitatu. Lakini kwa takwimu za Serikali kwa vitabu vilivyoko, sina hakika vitabu vipya, tulichotumia ni asilimia 7.3. Sasa kama kwa miaka mitatu tumetumia 7.3, leo unakuja na kitu kipya, *ASDP* bado iko pale, matunda hatujaona, hela hatujamaliza, mimi naona hapa ni kauli ambazo zitatuchanganya, tutaiunga mkono, lakini hakuna kitu chochote. Kama kutakuwa na maelezo ya kina nitaweza kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwenye *stimulus package*, kikubwa ambacho amegusia Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, lakini naomba kusisitiza, tunasikitishwa sana kwamba *package* iliyotajwa kwenye vitabu vyenyewe hatuioni iko wapi, labda hivyo vipya. Lakini hata ingelikuwepo, mipango mikubwa namna hii na hasa kwa uzoefu wa *EPA* huko nyuma, hatutegemei kama itapangwa tu kule Serikalini bila Bunge kupata nafasi ya kujadili na ndio maana tumetoa *package* huko nyuma ya mifano ya nchi zote ambazo zimetengeneza *stimulus* ya namna hiyo ikiwemo na Marekani ambapo Bunge limejadili, makampuni yameainishwa na kimsingi kampuni ambayo inapaswa kulipwa ni lazima inakuwa *declared bankrupt* kabla haijaenda kulipwa. Hakuna kampuni yoyote kwa mujibu wa sheria ya Tanzania iliyokuwa *declared bankrupt* katika kipindi kati ya mwaka jana katikati na sasa ambapo uchumi wa Dunia unasemekana kwamba umeathirika sana kwa ajili ya *Global Financial Crisis*. Sasa kama hatujaathirika, ni sababu zipi tunaenda kulipa na kwa misingi ipi? Sasa sisi tunasisitiza, ni lazima watakaolipwa, wafanyiwe *audit* maalum, majina yao yatangazwe na taarifa hiyo kwa kuwa Bunge halitakutana mara nyingi, ipelekwe kwenye Kamati ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia kusema kwamba sitaiunga mkono bajeti hii mpaka nipate maelezo ya kuridhisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Slaa, ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Mgana Msindai wakati huo huo Mheshimiwa Lucas Selelii ajiandaye.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie bajeti ya Serikali kwa mwaka unaokuja. Nimpongeze Mheshimiwa Mkulo, niipongeze Serikali kwa ujumla, kwa kweli bajeti wamejitahidi kuitengeneza, ule upungufu mchache ndio tutauonyesha ili waweze kwenda vizuri zaidi. Lakini, ningeomba kwa kuanza, Serikali iwaonyeshe Watanzania kwamba hii bajeti siyo ya maneno matupu, ni bajeti ya utekelezaji. Hilo naomba na nina imani kabisa Serikali imedhamiria kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi mazuri ambayo nitayagusia kwenye bajeti hii, yamepitishwa na tunaomba utekelezaji wake uanze haraka hasa kwa fedha za ndani. Kwa sababu keshokutwa tutapitisha Sheria ya Fedha, maana yake kwa mara ya kwanza fedha zitaanza kutoka kwa wakati uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na miundombinu, maeneo mengi Serikali imetenga fedha, tunaomba utekelezaji uende haraka kwa sababu bila miundombinu, wananchi wetu watazidi kuumia. Nikianza na daraja la Mto Sibiti, baada ya kelele ya muda mrefu, mwaka huu zimetengwa fedha. Ninaloomba tu, daraja la Mto Sibiti liko mahali ambapo mafuriko huanza mwezi Novemba mpaka mwezi wa Tano. Maana yake yakianza Novemba mwaka huu ni mpaka mwezi wa Tano mwaka unaokuja. Tunaomba bajeti ikishapita, watangaze mapema tenda ili kuhudumia hilo daraja muhimu na barabara yake kilomita 25 walizozitengea fedha.

Mheshimiwa Spika, hii barabara ni muhimu sana, inaunganisha Mikoa yote ya Ziwa, Shinyanga na nchi jirani. Inapita Iramba Mashariki, inaunganisha Dodoma – Arusha na Mikoa mingine. Kiangazi, ndio barabara kuu ambayo huwa inatumika. Kwa kweli nirudie kuipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ambazo tuliomba zipandishwe hadhi kwa sababu Halmashauri haiwezi kuzihudumia na barabara moja ambayo imepandishwa hadhi ni ile inayotoka barabara kuu ya Singida kwenda Nzega, unaingia Kiomboi, unakwenda Kisiriri, unakwenda Kidalu, unakwenda Ibaga, unakwenda Kidarafa, hatimaye unaunganisha na Mkoa wa Manyara. Naipongeza sana Serikali kwa kuipandisha hadhi hiyo barabara. Sasa tunaomba watu wa TAMISEMI na Serikali Kuu wasaidie kwa sababu watakuwa wamefungua milango kuwaendeleza wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, barabara zote za nchi hii ni za kwetu, kuna barabara ya Manyoni – Itigi kwenda Kigoma, nayo ni muhimu sana. Nayo nina imani imetengewa fedha na ianze mapema. Lakini kuna barabara ambayo sisi tunaungana na watu wa Mkoa wa Singida. Sasa hivi kwenda Mwanza hakuna tatizo, kuja Dodoma, tatizo bado dogo na linashughulikiwa. Barabara ya Nzega kwenda Tabora ni kero kubwa kwa sababu hiyo ni sehemu ya barabara kubwa ambayo hatimaye itaunganisha Nzega – Tabora kwenda

Rungwa na kwenda Mbeya kama msemaji wa Mkoa wa Mbeya alivyosema hivi karibuni. Kwa hiyo, mimi naomba sana Serikali itilie mkazo mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye kilimo, tumesema kilimo kwanza na kwa kweli bila kilimo, tutaendelea kulia kila mwaka. Tunaomba huduma zote zinazohusiana na kilimo, hizi fedha zilizotengwa, kuna fedha ambazo zitapitia *TIB* na nina imani hiyo benki itasaidia sana wakulima wetu kuwawezesha ili tuweze kupata maendeleo. Tunaomba isiwe ya kukopesha wakubwa tu, tunaomba na wakulima wadogo wadogo wapate nafasi ya kukopeshwa hiyo fedha.

Hapo hapo niingie kwenye kitu ambacho Watanzania wote wamesikitika sana. Serikali kufuta asilimia 10 ya kodi ya mafuta ya kula kutoka nje. Kila mwaka huwa ni lazima tupigizane kelele na Serikali, inarudisha hiyo kodi. Jamani, sasa hivi kila kona ya Tanzania wanalima alizeti, wanalima michikichi, wanavuna karanga, ufuta, mazao yote yanayotoa mafuta yanalimwa hapa nchini, hakuna pembe yoyote ya Tanzania yenye shida ya mafuta siku hizi. Mheshimiwa Waziri alisema wamekubaliana *East Africa* hiyo kodi ifutwe, sisi hatuendi na *East Africa*. Mambo ambayo yanatufaa Tanzania, tunabaki nayo. Nitawapa mfano, sasa hivi tumekataa ardhi yetu isiingie kwenye mchakato huu, kwa nini isiwe mafuta? Sasa hivi wananchi wetu hawana tatizo, hawapigi kelele. Nenda zungukia Mkoa wa Singida, Mkoa wa Tabora, Shinyanga, Ruvuma, Iringa, Mikoa yote alizeti imestawi na hatujui tutauza wapi. Sasa kwa nini tuletewe mafuta kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninashauri Serikali, kwa nini mgombane na wananchi wenu? Mimi ningeomba hiyo kodi irudishwe mara moja. Kwa kweli tutakuwa hatuendelei, lakini wananchi tutakuwa tunarudi nyuma. Hiyo kodi ikifutwa, kesho, Kimbo, sijui mafuta gani yatajaa hapa nchini hata wananchi wetu watashindwa mahala pa kuuza mafuta yao. Tunaomba sana kwa hapo Serikali iangalie, hilo linawauma Watanzania wote. Sasa mimi sidhani kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakubali kugombana na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, nimesoma kwenye bajeti humu misamaha ya kodi kwa majerikeni ya kuwekea maziwa. Hapa kwetu tuna maziwa mengi sana, hatuna viwanda. Sasa, haya majerikeni yaliyosamehewa kodi, tutawekea maziwa tupeleke kwenye viwanda gani? Ndiyo! Sisi ni wa tatu katika ufugaji wa ng'ombe, nafikiri duniani na maziwa yapo! Lakini leo, tunaletewa maziwa ya unga, tunaletewa maziwa ambayo hatuyafahamu. Kuna mfano mdogo, sisi tuko kwenye soko la Afrika Mashariki, kuna kiwanda kimoja kiko Musoma, kinatoa maziwa mazuri sana, lakini wanawekewa mizengwe, hawawezi kuuza kwa jirani zetu, leo sisi tunataka tuwaruhusu. Mimi ninashauri tufikirie upya, haya majerikeni yaendane na kufufua viwanda vyetu vya maziwa vya Arusha, Dar es salaam na vingine vijengwe hata Singida, maziwa tunayo mengi na karibu na Msumbiji huko Ruvuma ng'ombe wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimsemee mkulima wa kawaida, tuna Wizara ya Maji na Kilimo, nashukuru wanatusaidia na sasa hivi tunataka wananchi wetu walime. Mwaka jana na mwaka juzi niliwaambia mkitaka mfano mzuri wa mabwawa madogo madogo

nendeni Soronera pale. Mto Soronera hauna zaidi ya kilomita 40, una mabwawa madogo zaidi ya 20, ambapo hata sisi makorongo yetu yanayomwaga maji bila mpango, yakijengwa mabwawa madogo madogo yatawasaidia sana wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kuna skimu zimekufa; kuna skimu ya Mwangeza toka mwaka juzi Serikali inasema itatoa fedha. Hebu wakati Wizara hiyo ikifika iniambie; kuna Mwangeza, kuna Msingi, kuna Masagi na nyingine nyingi tu. Tulikwenda Rukwa, zipo! Kila kona tulikokwenda zipo! Kwa hiyo, sisi wananchi wetu kuwawezesha hata tukiwapa pesa kwa hizi mvua tunazotegemea, hawatafanikiwa, tuwasaidie tuanzishe kilimo cha umwagiliaji, hicho ndio kitakachotukomboa. Hilo, naliomba sana Serikali kutilia maanani suala hilo.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye umeme; tumeambiwa kuna umeme vijijini, mpaka leo hatujaona mchanganuo, hatujaona wataanza lini. Bado wanapita kufanya mikakati, upembuzi yakinifu, sijui tutakuja kumaliza lini! Mimi naomba Waziri wa Nishati aniambie kwanza mradi wa umeme ambao ulianza miaka minne iliyopita wa kutoa umeme Mtinko – Ikungi – Iyambi – Nduguti na Nkalakala umefikia wapi? Serikali iliahidi kutoa umeme Kinampanda uende Chuo cha Msingi, mpaka leo hakuna kitu. Ahadi hizi ziko kote, hata kwa Mheshimiwa Spika, ziko, ukienda Peramiho zipo. Kwa hiyo, sisi tunaomba huu umeme vijijini tuelezwe, upo au haupo? Kama upo, umeanza kutumika wapi? Tunawashauri na huu umeme wa upepo hebu nao uanze mapema.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu sasa wanajiletea maendeleo kwa kujenga shule, kujenga nyumba zao za kisasa, lakini mpaka leo bado tunaumia bei ya vifaa vya ujenzi. Mimi sijaona Serikali inasemaje katika eneo hili. Wananchi wetu wanachotaka ni mabati, sementi, tupate bei ambayo ni nafuu, kama tunaweza kufidia kwingine, kwa nini tusifidie kwenye haya? Mimi naomba sana Serikali ilishughulikie suala hilo. Kuna miradi ambayo imepitishwa, tunaomba hasa kwa fedha za ndani, zisimamiwe mapema.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu, Waziri alijibu hapa hapa wa TAMISEMI, akasema zile fedha zinazopelekwa kwa ajili ya kujenga uwezo, tutajitahidi kuimarisha Chuo chetu cha Hombolo ili kozi zote za kuwapa uwezo watu wetu, Wakurugenzi, Maafisa Mipango, Waweka Hazina, Madiwani na wengine wote, zifanyike Hombolo. Sasa tunaomba Waziri anayehusika asisahau suala hilo. Zamani tulikuwa na Chuo cha Mzumbe, kikachukuliwa sasa hivi ni Chuo Kikuu Mzumbe. Kimeanza Chuo cha Hombolo, hebu tuwasaidie hicho Chuo kiendelee kwa ajili ya faida ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, lingine, ninashauri Wizara ya Elimu, tumejenga shule nyingi sana, nyingi hazijakamilika na Walimu hakuna. Uwekwe mpango wa makusudi kupata Walimu wa kutosha na uwekwe mpango wa makusudi kumaliza majengo ambayo wananchi walishamaliza zamu yao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msindai, kengele ya pili, nakushukuru sana.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Selelii na nadhani baada ya hapo atafuatiwa na Mheshimiwa John M. Cheyo na pengine ndiye atakuwa wa mwisho kwa asubuhi hii.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi leo ili niweze kuzungumza katika bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze na utangulizi, kuishukuru Serikali kwa fedha ambazo wametenga za umeme kwenda Ndala, hizo pesa ziko *TANESCO* tayari. Ambacho ningeomba tu Wizara ya Nishati na Madini iwaagize watu wa *TANESCO* watangaze haraka hiyo tenda ili *Christimas* hii watu wa Ndala, Puge, Kiliziwa waweze kupata umeme. Ahsante sana Serikali kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya juzi tarehe 10 ambayo ilielekeza namna ya kupambana na mtikisiko wa uchumiwa Dunia na hasa alipokuwa amesema juu ya kuzingatia kilimo. Mimi katika hili, nipende kuleta kilio cha wananchi wa Mkoa wa Tabora ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakinyonywa na makampuni ya Tumbaku katika suala la mbolea.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa Mkoa wa Tabora nao ni wakulima kama wakulima wengine wa Mikoa mingine walivyo. Hivi kuna tabu gani Serikali hii nzuri kuwakopesha na kuwapatia mbolea ya ruzuku? Ninaiomba Serikali kwa kuzingatia jambo hili muhimu la kilimo kwanza, iweze kuwapatia ruzuku ya mbolea kama inavyofanya katika Mikoa mingine na kama ilivyoanza kufanya katika Wilaya ile ya Sikonge. Sambamba na hilo, vile vile niweze kuungana mkono na Mheshimiwa Rais katika azma yake ya kuimarisha miundombinu hasa ujenzi wa barabara na nitumie fursa hii kuishukuru Serikali katika kuzingatia barabara yetu ya Nzega – Tabora kuitengea ingawa kwa uchache sana shilingi bilioni tano mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuchangia ifuatavyo. Tanzania ni nchi ambayo imebarikiwa kuzungukwa na nchi ambazo hazina bandari. Ni bahati ambayo imepewa na Mwenyezi Mungu, hatujagombea wala hatujaomba, Mwenyezi Mungu akatujalia, tukazungukwa na nchi za Burundi, Kongo, Uganda, Zambia ambazo zimefungwa, haziwezi kwenda popote zaidi ya kutumia bandari yetu. Lakini kwa bahati mbaya sana, fursa hii hatujaitumia sawa. Fursa hii ambayo Mwenyezi Mungu ametupa bure, fursa hii ambayo tumepewa kwa kudra ya Mwenyezi Mungu hatujaitumia kwa akili ya kufanya biashara. Tungekuwa na fursa ya kutumia vizuri, nchi yetu katika bajeti hizi wala isingehangaika.

Mheshimiwa Spika, ninashauri wachumi wetu walioko pale, walione hili. Wabunge wamekuwa wakisema mara nyingi, Wabunge wamekuwa wakishauri mara

nyingi, walione hili na kulitilia maanani, kutumia nafasi hii ya nchi hizi ambazo hazina bandari, kutumia fursa hii ili nchi yetu iweze kupata fedha nyingi kwa kutumia bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo ninapendekeza, kwanza pale bandarini pale tuondoe ukiritimba wa *TICTS*, tuondoe ukiritimba. Kwa nini *TICTS* mnaing'ang'ania? Wekeni watu wengine washindane na huyu *TICTS*. Tumempa sijui miaka 20, 25 kwa nini? Yote haya yanakuja kwa sababu ya ufisadi. Tuondoe ukiritimba wa *TICTS* ili nchi iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kuhusu reli. Reli ni mbovu na tuliowapa kuendesha reli ni wabovu. Tumewapa Wahindi wale maskini kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitakupa ushahidi, wakati reli inaendeshwa na Watanzania na inaendeshwa na Serikali ya Tanzania tulikua tunafanya biashara vizuri sana, ilikuwa inafikisha mpaka tani milioni mbili na nusu mwaka 2002, 2003, 2004. Angalia rekodi katika hali ya uchumi mwaka huu, imesafirisha tani 400, hawa Wahindi hawafai, wafukuzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana hawa watu wamepata kwa njia za pembeni, wewe utampaje mkandarasi ambaye hana uwezo! Hawezi kukopa, hakopesheki, leo ndio unampa aendeshe Shirika kubwa namna hii katika nchi yetu! Nchi yetu imefanywa sijui kichaka cha namna gani na watu tunawashangilia tu, tunawabeba, haiwezekani, wafukuzwe hawa Wahindi, hawafai kabisa! Tungeweza kuimarisha reli yetu hii, mzigo ulioko DRC – CONGO peke yake ni tani milioni tano. Mzigo ulioko Congo, ukaunganisha na mzigo ulioko Burundi, Uganda na Rwanda, unaweza kupata tani milioni 10. Lakini kwa sababu mipango yetu hatuipangi vizuri, hatusikilizi ushauri, unawapa Wahindi. Tani 400 ndio unafanya kazi gani? Ndio maana nchi zote hizi wameacha kusafirisha kwenye bandari yetu, kuna ukiritimba wa *TICTS*, kuna ukiritimba tena kwenye reli, badala yake wanakwenda Mombasa. Tutaendelea kulia umaskini, tutaendelea kusingizia mtikisiko wa Dunia, kumbe sisi wenyewe tungetumia njia zetu za kuimarisha uchumi hapa, wala tusingebabaika lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakatizwa hata kupunguza siku za Bunge kwa sababu ya mambo ya namna hii. Hawafai hawa watalaam wetu hawa! Wanapenda kusingizia tu wakipata kitu, wanazingizia mtikisiko. Hawajafanya kazi barabara ya kuumiza vichwa vyao namna gani ya kuepusha suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais kasema kwamba ili tuinue uchumi, tujenge miundombinu, tujenge barabara. Nimeomba kuhusu mwongozo wako, barabara ile ya Chalinze kwenda Tanga pamoja na kuidhinishwa na kufanya inavyofanywa, lakini kama kweli wachumi hawa wangekuwa wanazingatia mambo ya kiuchumi, wangeanzia kujenga Chalinze kwenda Kibaha, kwenda Dar es salaam. *Traffic* kubwa iliyoko pale, inabeba kutoka Mbeya, wanafika Chalinze, kutoka Mwanza wanafika Chalinze, kutoka Congo, kutoka Burundi, kutoka Rwanda wanafika Chalinze. Sasa badala yake unajenga huku njia mbili mbili kutoka Chalinze kwenda Tanga unakuja kwenye njia moja, hiyo

akili ya wapi! Ndio maana nasema wangekuja tuwashauri, wangekuja tuwaeleze kwamba *the best practice* mgejenga kutoka Chalinze kupunguza hata msongamano wa Dar es Salaam, kupunguza msongamano wa pale Kibaha! Lakini wanakwenda tu, wanafanya tu. Inauma kweli, inatuumiza sana sisi tunaotoka Mikoa ya Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana hapa tukasema kwamba hebu tuunganishe Mikoa, hebu barabara zetu zijengwe za Mikoa, hebu barabara zetu zijengwe za kiuchumi kama hivi tunavyokwenda Kigoma. Nimesema DRC – Congo kuna mzigo pale, ukijenga barabara ukafikisha Kigoma, ukaimarisha bandari ya Dar es salaam, ukaimarisha bandari ya Kigoma na bandari ya Mwanza, una pesa tayari. Lakini wenzetu hawa hasa wanaokaa huku mbele, hasa Mawaziri, wana hiyana, wana roho mbaya na *Wallah*, Mungu atawalaani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unaacha barabara ya muhimu kutoka Dodoma, amesema leo Waziri bilioni 110 Serikali imekula hasara.

Kwa taarifa nilizonazo, Serikali imepelekwa Mahakamani, ujue pale kuna bilioni nyingine Serikali inalipa. Wapo humu humu na ukiwauliza majibu yao watakwambia; ooh Serikali ni sikivu tumekusikia, subiri bejeti ijayo, tumepanga mpango kabambe, kasungura kenyewe kadogo. Kasungura kidogo! Wao wanapeleka barabara za Wilaya, wao wanafanya barabara ambazo zipo zinaendelea, sisi wanatunyima. Lazima tuseme na mimi naomba ninyi mlioko mstari wa mbele lazima muone aibu; angalieni makaburi, yameandikwa hivi: “Sisi tuliolala hapa tulikuwa kama wewe.” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi sivutii barabara ya kutoka Manyoni kwenda Itigi, Tabora na Kigoma hapana, lakini angalia hata Dodoma yenyewe; Makao Makuu ya nchi kuna barabara kuu inaitwa *The Great North Road* inatoka Cairo mpaka Minjingu, inatoka Johannesburg mpaka Iringa, miaka hamsini ya uhuru leo tumeshindwa kuunganisha. Leo wanakwambia tunaunganisha kutoka kwa Mustafa pale, kutoka Korogwe sijui barabara ya Wilayani kwenda Dumila, kwenda Kongwa aah! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimekwambia hapa; hao watu wana hila mbaya na CCM hawana jambo la maana la kuliweka ndani ya CCM ieleweke. Nenda Nzega kwenye jimbo lako, wale wote wanaweza kupita Nzega; barabara kutoka Nzega kwenda Tabora ni kama vile unaenda jahanamu.

Mheshimiwa Spika, pale Tabora ni *center* kama *hub*, ukienda Magharibi utakwenda Kigoma; ukienda Kusini utakwenda Mbeya mpaka Mpanda; ukienda Mashariki utakwenda Itigi mpaka Manyoni; ukienda Kaskazini unakwenda Nzega mpaka Mwanza; Tabora imeachwa hivyo hivyo; miaka hamsini ya Uhuru, leo wanakwambia mipango iko mbioni na wewe ni Diwani kazungumze kwenye Halmashauri; ukazungumze *Trunk Road* kwenye Halmashauri!

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa uchungu sana. Ninasikitika sana inapotokezea vitu vya namna hii kufanywa na Serikali ambayo tunaiamini hasa ya Chama cha Mapinduzi! Ninaamini hawa watu wana nia mbaya na sisi Wabunge ambao

tunatokana na Chama cha Mapinduzi, wangekuwa na nia nzuri wangetupa mipango ambayo inaeleweka ya kusemekana vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika Kitabu cha Nne ambacho wanasema wameleta kingine, barabara zote zilizotengewa fedha hazina makisio. Zimetengewa pesa bila kuwekewa makisio; hivi uliona kitabu gani cha bajeti kinakosa makisio ya barabara? Barabara inatengewa fedha hujui itaisha lini, ndio yale ya barabara kukaa miaka mitano au sita.

Siku zote fedha ambazo zinatengwa huwa tunaambiwa kwamba, tutatengewa kwa mtindo ule wa *MTEF;* kwamba, baada ya miaka mitatu utapitisha bajeti hii na kila mwaka labda utapitisha shilingi bilioni arobaini, mwaka kesho shilingi bilioni thelathini mpaka barabara itakapokamilika. Angalia kurasa zote zile hazina makadirio!

Mheshimiwa Spika, labda hivi vitabu ambavyo vimekuja watatuambia, lakini hata hivyo naomba virekebishwe viwekewe makisio ili kile kinachokipitishwa tuweze kukipitisha tukijua kwamba, barabara hii kweli itaanza kujengwa, inakamilika lini na ina kiasi gani cha pesa. Vilevile hii ambayo nimeitolea mwongozo nayo haina makisio, haina makadirio, ipo tu kwamba ni bilioni kadhaa; je ni hizo hizo au zinahitajika nyingine?

Mheshimiwa Spika, napenda nipate ufafanuzi wa kina juu ya mambo niliyoyasema asubuhi na haya ambayo nimeyatamka hivi sasa na hasa barabara ambazo zinasisimua mambo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, Waziri Mkuu alitoa ahadi hapa hapa Bungeni alisema kuwa, Barabara ya kutoka Manyoni, Itigi mpaka Tabora, ameitengea shilingi bilioni tano; ukiangalia kwenye kitabu cha nne zimetengwa shilingi bilioni 5.7. Yeye aliahidi shilingi bilioni kumi, sasa hizo shilingi bilioni nne na *point* zimeenda wapi? Ningependa hizo shilingi bilioni kumi ambazo zilitengwa mwaka jana, ziwekwe bayana ili watu wote tuweze kufahamu zimefanya nini.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limepigiwa kelele sana na Viongozi wa Dini ni hili la kufuta kodi. Mimi kule kwangu kuna Hospitali ya Wilaya, lakini zipo hospitali mbili ambazo ndio tegemeo la Wananachi wa Nzega na Wananchi wa Wilaya ya Uyui; kuna Hospitali ya Kinga ambayo ipo Igunga na kuna Hospital ya Ndala ambayo ipo kwenye jimbo langu.

Maaskofu na Madaktari wa pale, wamenipigia simu kutaka ufafanuzi wa kina juu ya jambo hili. Ningekuomba Mheshimiwa Waziri, useme bayana; ni vitu gani hasa ambavyo vimefutwa na vitu gani ambavyo vitalipiwa kodi kwa hosptali hizi ambazo ni za huduma ya jamii na zinaisaidia sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu ambao wamezungumzia juu ya mafuta ya kula na petroli. Wachimbaji wa madini tumewapa fursa miaka yote na tumekuwa tukipiga kelele toka mwaka 1998, badala ya Serikali kuwaondoshea hii, walichokula kimetosha bado inataka waendelee kula; mimi ningeshauri hii fursa ambayo wameifanya imetosha, waanze kulipa kodi kama tunavyolipa sisi wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, wao wana kipato kikubwa sana; siku moja nilisema hapa Bungeni kwamba, wachimbaji hawa wanachimba wenyewe, wanajikagua wenyewe, wanasafirisha wenyewe, wanauza wenyewe, wanarudisha wenyewe; hivi hawawezi kudanganya kweli? Unategemea mfanyabiashara awe mwaminifu; amekuwa Askofu au amekuwa Sheikh! Haiwezekani, hata vitu ambavyo tunaviweza tukiviwekea kodi bado tumewasamehe.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kodi hii iwabane wote, kwa sababu kama ni fursa imeshatosha, kama ni mahali pa kufanya biashara tayari wameshafanya vya kutosha; walipe kodi na kuiendeleza nchi yetu kama nchi zao zilivyoendelea. Sambamba na hivyo, lazima tukumbuke …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Hiyo ni ya pili. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68; Bunge linakataza kauli za kuudhi wakati Mbunge anapozungumza ndani ya Bunge. Mheshimiwa Mbunge, ambaye amemaliza kuzungumza, ametoa kauli ambayo kwa maoni yangu naona siyo nzuri. Amesema Mungu awalaani. Hii ni kauli nzito sana na ni ya kuudhi.

Mheshimiwa Spika, amesema Mungu awalaani Baraza la Mawaziri lote. Kila siku tunaomba dua hapa, kuliombea Bunge na nchi yetu ili tuliongoze Bunge hili kwa maslahi ya wananchi wetu. Sasa kwa maoni yangu, hii ni kauli ya kuudhi na tunaomba mwongozo wako katika hili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani uhuru wa kuongea tulionao hapa ulioko kikatiba, unaruhusu pia mtu akiwa amepandwa jazba itakuwa kazi ngumu kwa sisi tunaoongoza mjadala hapa kuzuia watu kutoa hisia zao kamili. Faraja tu kwa Waheshimiwa Mawaziri ni kwamba, dua la kuku halimpati mwewe. *(Kicheko)*

Mimi ninamuelewa Mheshimiwa Selelii; alichokitamka kwamba Mungu awalaani watu fulani, hakifikii kilichotajwa kwenye kanuni kwamba ni lugha ya kuudhi; hili ni jambo la hisia tu.

Yamewahi kutokea mambo makubwa sana humu watu wakipandwa na jazba, lakini tutaendelea kuulinda uhuru wa kusema Bungeni. Kwa hiyo, nashukuru kwa hilo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tusiwe tunafikia kuwaombea wengine laana. Tujitulize tu, tushauriane na tujenge hoja inatosha, lakini siwezi kuchukua hatua yoyote afute usemi kwa sababu hizo ni hisia zake.

Msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, sidhani kama mimi nitalaani au nitamwomba Mungu awalaani Viongozi wengine, naomba usiweke maneno.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii na kwa niaba ya ndugu zangu wa Bariadi, nataka kutumia nafasi hii kuweka kilio chao juu ya pamba.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2008, ndio tulipoanza kuona mtikisiko wa uchumi wa kiulimwengu na ndipo pale tulipoanza kuona bei za pamba zikiteremka kutoka senti themanini kwa latili mpaka kufikia thelathini na nne. Kipindi hicho pia ilikuwa ndio wakati ambapo wakulima wa pamba walikuwa wameanza kupanda na ndio kusema walikuwa wamewekeza. Ninataka kusema kwamba, katika msimu huu wa pamba, kwa sababu bei ilikuwa nzuri katika msimu uliopita, wengi badala ya kulima chakula walilima pamba.

Kwa hiyo, bei zilipoteremka hawa watu wameathirika vibaya sana, kwa sababu mbegu walizopanda hawawezi kuziondoa, nguvu zao walizoweka hawawezi wakarudishiwa na mtu yeyote na mategemeo yao kwa mwaka huu bado hayajaelezwa na mtu yeyote; ndio maana Mheshimiwa Rais alipozungumzia juu ya namna ya kuwafidia wanunuzi wa pamba, mimi nilijua kuwa angefika mpaka mwisho wa hadithi hii.

Waliofurahi kwa Hotuba ya Waziri ni Mabenki, kwa sababu mikopo yote ambayo imechukuliwa na watu na wameshindwa kuirudisha, itafidiwa na Serikali. Waliofurahi zaidi ni wale ambao wamesema kwamba, hata hasara ambayo wamepata wale ambao wamenunua pamba itafidiwa na Serikali.

Serikali haikusema baada ya kutoa unafuu wote huu kuwa, fedha inarudishwa hata mikopo inasimamishwa kwa miaka miwili. Hakuna riba ambapo kuna mikopo zaidi ya bilioni mia mbili na arobaini na saba; riba tu hata kwa asilimia kumi kwa miaka miwili ni zaidi ya bilioni hamsini na saba. Hizi ni fedha nyingi sana ambazo zinapelekwa kwenye sekta hiyo ndogo ya wanunuzi wa pamba. Kinachonisikitisha, ni vipi wale ambao ndio tunawategemea kutuleta hapa, zaidi ya watu milioni kumi wanategemea pamba, zaidi ya milioni saba ndio wanatupigia kura na wanampigia kura Rais; mbona hapakuwa na neno hata moja kwamba maana ya misaada yote hii ni wewe mkulima kuongezewa bei yako ya pamba?

Sikulisikia hilo kwa Waziri wa Fedha wala kwa Mheshimiwa Rais; sasa ninashangaa, Bunge hili bila kuwasaidia wale ambao wametuleta hapa; hivi ni kweli tutawekwa humu na wafanyabiashara tu au mabenki?

Mimi ninashauri Serikali iangalie upya hii *package* ambayo tumepewa na Mheshimiwa Rais na kwa vyovyote vile, wahakikishe kwamba, wanaweka angalau shilingi mia moja kwa kilo mwaka huu ili mkulima apate kati ya shilingi mia nne na hamsini na mia tano. Hii inawezekana kabisa, kama tumeweza kusema mwaka huu tutatoa bilioni mia moja kwa ajili ya kufidia madawa, pamoja na mbolea; ni kigugumizi gani ambacho Serikali inakuwa nacho kutamka bayana kabisa kuwa mwaka huu tutatoa bilioni ishirini tu kwa ajili ya kufidia wanunuzi wa pamba?

Mnapataje milioni ishirini? Mwaka jana tulipata kama tani mia mbili elfu za *cotton seed* au pamba ya mbegu; kwa hiyo, ukiweka shilingi mia moja, hata kwa kutumia takwimu za mwaka jana ni bilioni ishirini tu; kwa nini usitoe hizo bilioni ishirini kutoka kwenye mia moja ukawapatia hawa wakulima ambao zaidi ya watu milioni kumi wanategemea hili zao?

Zaidi ya wapiga kura milioni saba ndio wanaomuweka Rais katika madaraka, kwa hiyo, kwa hali hiyo nafikiri ni vizuri ukaangalia upya hii bajeti na utupe uhakika kuwa hiyo pesa itapatikana. La sivyo, tunaweza tukajikuta hatuna shilingi mia tano kwa kilo na kwa baadhi yetu pia kura hazitakuwepo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ninafikiri tungelitilia maanani. Nimekuja kugundua kwamba, kwa miaka mingi tumewapunja wakulima wa pamba; kwa miaka yote tunapoangalia bei tunaangalia bei ya uzi tu; kwa hiyo, bei ya uzi tunayouza nje ikishuka, ndio kusema na bei ya wakulima inashuka pia.

Ukweli mwaka jana ambapo tulilima tani laki mbili za pamba, ndio kusema pia tumepata tani za mbegu za mafuta zaidi ya laki moja na ishirini elfu na hizi mbegu za mafuta zinaliwa hapa hapa nchini, ambayo ni sawa sawa na asilimia sitini na sita ya mazao yote. Mbegu ya mafuta ndio tunapata mafuta, mbegu hiyo hiyo ya mafuta ndio tunapata sabuni na mashudu na yote yanaliwa hapa hapa nchini.

Kwa hiyo, ndio kusema kama Wizara ya Kilimo ikiangalia vizuri, hakuna haja ya kutafuta hela ya ruzuku ili kuwapatia fedha ya kutosha hawa wakulima. Leo tumeelezwa na Mheshimiwa Msindai hapa na pia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa, imebidi muweke *zero rating* kwa ajili ya mafuta kutoka Malaysia. Ungewaambia wakulima wa pamba leo watapata mia tano kwa kila kilo, mimi nafikiri mbegu utakazopata kutoka kwenye pamba utazikimbia na kama utapata mbegu za kutosha, kutakuwa na mafuta ya kutosha nchini na hakuna haja ya kutafuta mafuta kutoka nje. Kwa hiyo, tuwaangalie Wakulima. Hii ndio rai ya kwanza, natumaini sijatoa laana kwa mtu yeyote. *(Kicheko)*

Jambo la pili, nimeangalia vitabu hapa kitu kimoja katika bajeti ambacho kinanipa wasiwasi ni mwenendo wa madeni yetu. Ukiangalia mwenendo wa madeni yetu ambayo yanatoka nje, yanaonesha kama kuna unafuu kwa sababu tunarudishiwa fedha na wale ambao tumewakopa. Sasa tumeanza mtindo wa kukopa ndani, mpaka 2008 tulikuwa na deni tayari ambalo ni trilioni 1.9, ambayo ni karibu nusu ya fedha zote tunazozikusanya ndani ya nchi au tulizozikusanya mwaka jana. Hizi zote tunaambiwa sijui kama ni sawa au kitabu hakiko sawa sawa; asilimia 99 ya hii mikopo yote ni dhamana ya Serikali kwa mambo mbalimbali ya kiuchumi. Kwanza, ninachojiuliza; mwaka huu Rais ametuambia anataka kukopa ndani karibu trilioni moja na ushee, kwa hiyo na ilyobakia itakuwa karibia trilioni tatu.

Ukiangalia kwenye vitabu vyako, miaka iliyopita tulikuwa tunalipa madeni kama bilioni mia tano, billioni mia sita, mwaka huu tunalipa trilioni 1.5 kwa madeni; kwangu naona hii ni sehemu ambayo Bunge hili linapaswa kuelezwa bayana; hivi hakuna mahali ambapo Bunge hili linaweza kuelezwa moja kwa moja kuwa katika miaka hii sisi

tutakuwa na *commitments* au tutakuwa na miadi ya kiasi hiki na Bunge hili likasema ok! *ceiling* ni yenu mbona kila siku mnatuambia kuna bajeti ya *ceiling,* Bunge hili ndio liiambie Serikali kwamba hamuwezi kutuendesha kwa kutuwekea mikopo, mwisho wenu ni hapa? Mimi naona bila hivyo tutarudi tena kule nyuma, ambapo nchi hii inakuwa ni ya mikopo kila siku. Naomba jambo hilo tuelezwe vizuri na liwe bayana.

Jambo la tatu, nataka kuzungumzia juu ya muundo wa vitabu vyetu; kusema kweli vitabu vyetu havituoneshi hali halisi ya fedha ya Serikali. Ukisikiliza Hotuba ya Serikali, hakuna mahali ambapo tumeambiwa kuwa, Serikali itamaliza mwaka wake tarehe 30 Juni na bakaa au *balance carried forward* itakuwa kiasi hiki au tutamaliza mwaka na madeni kiasi hiki, ukiacha madeni ambayo ni ya Taifa. Hakuna anayetuambia na vitabu vyote hivi havioneshi.

La pili, unaambiwa kwamba, kilimo tutaweka bilioni sitini na sita, lakini ukiangalia kwenye kitabu unakuta kuna bilioni mia mbili. Ukidhani kwamba, labda utaikuta kwenye miundombinu kwa ajili ya umwagiliaji, unakuta kuna bilioni ishirini tu ya kujenga miundombinu ya *irrigation!* Fedha haionekani kufuatana na vitabu hivi, mimi naona kwa miaka ishirini na tano, tumeendelea na mtindo huu wa *budgeting* na namna ya ku-*report* Bungeni. Mheshimiwa Mkulo, una wataalamu wa kutosha kuweza kuangalia njia ya kujieleza vizuri zaidi ili Bunge liweze kuelewa mambo yalivyo.

Kilichonisikitisha katika bajeti yetu hii, ulimwenguni kote sasa watu wanakopa, haiwezekani kuamini kabisa kuwa nchi yetu tutaendelea kuwa tegemezi kwamba watu wakope kule halafu watupe sisi fedha. Mwaka jana nilikusifu kwa sababu tulikuwa tumepunguza utegemezi, lakini mwaka huu tumeongeza utegemezi na kuwa na bajeti tegemezi sio sifa.

Mwisho, nimeangalia katika miuondombinu, hakuna Barabara yetu ya Ngw’igumbi - Maswa – Bariadi; imekwenda na kitabu au imefanya nini? Kabla sijamaliza Bunge hili, nitapenda Watanzania na Watu wa Bariadi waelewe barabara hii ipo au imeenda na mtikisiko wa Uchumi wa Dunia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nangojea kwa hamu kupata majibu zaidi juu ya ruzuku kwa pamba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo. Waheshimiwa Wabunge, kwa mchana huu nadhani hatuna muda wa kuendelea kwa sababu zimebaki dakika kama tano tu. Ninalo tangazo moja; mwenzetu Mheshimiwa Paschal Degera, amefiwa na mama yake mzazi huko Dar es Salaam leo asubuhi na mazishi yatafanyika Kijiji cha Bonga, Wilayani Kondoa, keshokutwa, Siku ya Jumatano. Katibu na wenzake upande wa Utawala, wanamsaidia Mheshimiwa na sasa hivi tayari yupo Dar es Salaam kwa ajili ya kuuchukua mwili wa marehemu na kuupeleka Kondoa.

Waheshimiwa Wabunge, ambao wangependa kushiriki katika mazishi keshokutwa, wanaweza kupeleka majina yao kwa Katibu ili mwenzetu asiwe mpweke.

Kondoa siyo mbali sana, tutatoa usafiri. Mwenyezi Mungu, aiweke mahali pema peponi roho ya Marehemu Mama yetu huyo. *Amina.*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na tunaanza na Mheshimiwa Lekule Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Salehe.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kutoa ufafanuzi na mwelekeo wa nchi yetu, kuhusu tatizo la msukosuko wa uchumi. Alisema mambo makubwa sana na alitueleza mikakati ya Serikali yake, kuweka namna ya kuinusuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alizungumzia jinsi ya kuimarisha ununuzi wa pamba, kahawa, madini, miundombinu na kilimo kwa ujumla, lakini kuna jambo moja limesahaulika; siwezi kusimama hapa bila kuzungumzia suala la mifugo kama Mheshimiwa Cheyo anavyozungumzia pamba na Wabunge wa Kusini wanavyozungumzia korosho. Siwezi nikaacha kuzungumzia mifugo, kwa sababu wafugaji ndiyo walionileta hapa na nasimama kuwatetea wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, Wafugaji wana bahati mbaya sana kwa sababu Serikali hii inawa-*ignore*, haiwatambui na pia haiitambui mifugo; ni kama vile tumekuja hapa Tanzania kwa bahati mbaya; sijui na nitasema sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wamenyang’anywa maeneo yao yote, hawana tena maeneo ya kufuga, ndiyo *National Parks* zilizopo Kaskazini. Ninashangaa, msukosuko wa ukame ulioingia nchini na kuathiri mifugo na wafugaji, Serikali imekaa kimya haizungumzii; ni jambo la kusikitisha hata Serikali yetu haina Wizara ya Mifugo kwa sababu mabwawa ya mifugo hayapo katika Wizara ya Mifugo, yapo Wizara nyingine. Majosho hayapo katika Wizara ya Mifugo yapo TAMISEMI, fedha za *PADEP* zinazotumika kwa ajili ya mifugo zipo TAMISEMI; sasa kuna nini Wizara ya Mifugo, kuna fedha za madawa tu. TAMISEMI inawasahau wafugaji, Wizara ya Maji inasahau Mifugo, Wizara inayotamkwa kwamba ni Wizara ya Mifugo ni madawa tu na hayo madawa hayatoshelezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu tuna majosho 20, lakini hakuna linalotumika; yameharibika, hakuna ukarabati wala madawa. Sasa hii Wizara ya Mifugo ni ya kufanyia nini mifugo? Naiomba Serikali iirekebishe Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za ukarabati wa majosho na fedha za kujenga majosho ziende kwenye Wizara ya Mifugo, inatawanywa na tunashindwa kuielewa kwamba Wizara hii imekaaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ukame; mifugo katika Jimbo langu imehama na imekufa kwa wingi sana, wafugaji wengi wamehamia Monduli katika Tarafa moja ambayo imepata neema. Mifugo ya majimbo yote mawili na Wilaya zote mbili; Longido na Monduli, wamerundikana huko, malisho yameisha na hatujui waende wapi. Naomba Serikali iruhusu mifugo iingie katika baadhi ya maeneo yenye mbuga za wanyama; kwa nini Kenya wanaruhusu mifugo yao wakati wa ukame hata ukienda Jomo Kenyatta Airport unakuta mifugo iko ndani. Kwa nini katika maeneo ya wafugaji wanyamapori wanachanganyika na mifugo wakati wa masika, lakini maeneo yale tuliyonyang'anywa ambayo wanafungiwa wanyamapori, sisi na mifugo haturuhusiwi kuingia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaokoe wafugaji, mifugo ikiisha hamuwezi kuwalisha. Kwa hiyo, naomba mifugo iruhusiwe kuingia maeneo ya Tarangire na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu; tunakubaliana sote kwamba, maisha bora hayawezi kupatikana bila elimu na ndiyo maana asilimia kubwa ya watu wenye maisha bora katika nchi hii ni wasomi, hakuna mtu anayekataa, lakini hatuwezi kupata maisha bora bila elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie suala la elimu kwa sababu umaskini umejaa sana nchini na hasa vijijini. Katika Jimbo langu hatuna shule za kutwa, shule zote za sekondari ni za bweni na ada yake siyo shilingi elfu ishirini ni shilingi elfu tisini kwa mwaka na wazazi wengi wanashindwa kuwalipia watoto.

Ninawaomba Wabunge wenzangu, jambo hili tufute kitu kinachoitwa ada kwa sababu Serikali hii ina uwezo wa kulipia na kuwasomesha bure watoto wote wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wameweza kulipa Dowans shilingi milioni mia moja na hamsini na mbili kwa siku, Serikali inaweza kabisa kuwalipia watoto ada ya shule; kama wameweza kulipa mishahara hewa ya wafanyakazi wengi, hizo fedha zinaweza zikalipa ada za wanafunzi; na kama watapunguza magari ya kifahari yanayonunuliwa kwa bei kubwa, hizo fedha zinaweza kulipia ada Watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanaweza kudhibiti mikataba mibovu na ujenzi wa barabara, fedha zinazolipwa kwa hongo kutoa asilimia fulani, zinaweza kulipia ada kwa wanafunzi. Kama wameweza kulipa bilioni mia sita kwa *Twin Towers*, wanaweza

pia wakalipia wanafunzi wote wa Tanzania na kusoma bure kuanzia *form one* hadi chuo kikuu. Naomba tukatae na tuishinikize Serikali ilipe ada za watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia, nadhani mimi sikutoa laana kwa sababu laana ya Kisukuma ikikutana na ya Kimasai, inawezekana Baraza likavunjwa tena. Kwa hiyo, acha mimi nipunguze jazba kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ujenzi wa Barabara ya Arusha – Namanga; mkandarasi aliyepewa barabara ile sijui ndiyo anaanza au vipi, kwa sababu ameharibu barabara, ameivunja yote, haiwezekani ukavunja barabara kilomita sitini bila kutengeneza. Magari yanaharibika kila siku, vumbi hadi kufikia magari yanawasha taa mchana, imekuwa ni usumbufu; ukiwa unasafiri kwenda Arusha unaanza kushtuka kwa sababu siyo barabara. Naomba Waziri utume timu wakaangalie hiyo barabara.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, ukienda Nairobi, mkandarasi aliyepo Namanga Nairobi amefanya vizuri sana, kwa sababu anakwenda kwa awamu; anatengeneza anaweka lami ndiyo anaweka *diversion* nyingine, haiwezekani ukaweka *diversion* kutoka Ngaramtoni mpaka unakaribia Longido; naomba hilo liangaliwe kwa sababu ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutupatia chakula, kwani Jimbo langu lilikuwa kwenye hatari kubwa, watu walianza kuzimia lakini Serikali iliwaokoa na kuwapatia chakula. Naomba Serikali ijue kwamba, Wananchi wa Longido wanategemea mahindi ya msaada; ukienda Longido huoni tena ng’ombe, mifugo yote imehamia Ngorongoro, Monduli na Simajiro. Serikali ikae na kutafuta namna ya kuwanusuru wafugaji. Wafugaji hawa ni Watanzania na wameshiriki kukiweka Chama cha Mapinduzi madarakani, ninaomba tuwakumbuke ili tusije tukageuka na kukosa imani kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lekule Laizer na kama nilivyosema mwanzo, anafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Salehe.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake Wakuu, kwa kututayarishia Bajeti ambayo tunaijadili hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kutoa pongezi za kipekee kwa Serikali ya Awamu ya Nne ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri inayofanya kwa kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi hii kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba, Tanzania imebadilika, mbali na msukosuko wa kifedha na kiuchumi ambao umeikumba dunia na athari zake kutugusa, lakini Bajeti imeendelea kuwa ya watu kwa sababu imegusa walio wengi ambao ni wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linathibitika ukiangalia vipaumbele vya Serikali vilivyowekwa katika Bajeti; elimu, maji, kilimo, afya na miundombinu, hivi vyote vinawagusa wananchi walio wengi moja kwa moja. Elimu ndiyo inaongoza kwa kipaumbele, lakini la kusisitiza hapa ni kuwa, fedha hizi zote ambazo zimepangwa zitumike moja kwa moja kama zilivyopangwa. Kwenye elimu kuna matatizo makubwa; madawati hakuna, maabara zipo chache, vitabu hakuna, kwa hiyo fedha zielekezwe huko ili vijana wetu wapate elimu nzuri. Afya bora; tuongeze waganga wawe wengi, tuwape motisha madaktari ili wasitukimbie kwenda nchi nyingine kutafuta *green pastures*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la maji safi na salama, kwa hiyo, pesa zielekezwe huko kwa ajili ya uchimbaji wa visima ili watu wetu wapate maji. Dar es Salaam kuna matatizo, vijijini kote kuna matatizo na kwenye miji mingine wananchi wetu wakipata maji safi na salama, tutapunguza mzigo kwa Wizara ya Afya, kwani watoto wanaougua maradhi ya kuharisha watapungua na vifo vitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya bajeti yetu ya mwaka huu hairidhishi sana, kwa sababu ukiangalia ukurasa wa sitini na tano imeoneshwa kuwa, kuna mapato ya ndani na makadirio ya matumizi ya maendeleo na makadirio ya matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, mapato yetu ya ndani hata ukiunganisha na mikopo kutoka ndani, hayawezi kabisa kugharimia matumizi ya kawaida; kuna *deficit* ya bilioni 356.5, hii haileti sura nzuri kwa sababu tunategemea zaidi wafadhili kutugharimia miradi yetu ya maendeleo, hakuna senti hata moja ya ndani iliyokwenda kule na isitoshe hata matumizi ya kawaida tumeshindwa kuyafadhili kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatari kwa sababu wafadhili wetu likitokea jambo lolote; lile liwe la ndani au la nje, wanaweza wakazuia kutupatia hayo mapato, kwa maana hiyo, maendeleo yetu yatayumba. Ninavyoamini, picha hii imekuja kwa sababu ya msukosuko na zile hatua ambazo Serikali imeziweka za kuweza kukabiliana nazo, picha hii isiwe ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali ijitahidi kubana matumizi yale ambayo si ya lazima na upande wa mapato tujitahidi kukusanya na yatumike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri inayofanya ya kukusanya mapato. *Trend* ya ukusanyaji mapato, ukiangalia mwaka hadi mwaka inaenda vizuri sana, isipokuwa 2008/09 kutokana na msukosuko ulioingia, lakini hata hivyo, kukusanya kodi kwa asilimia 90 ya lengo pia si jambo baya sana, wanastahili kupongezwa. Jambo la msingi hapa ni kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato, wajitahidi walipa kodi walipe kwa hiari, kuwe na *voluntary compliance,* wapunguze gharama za ukusanyaji kodi ili watu walipe kwa hiari. Vilevile wajitahidi kutafuta vyanzo vipya vya ndani, ambavyo haviwakandamizi walipa kodi ambao ni wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la ushirikiano wa Wizara ya Fedha ya Muungano na Zanzibar, naomba hapa niipongeze Serikali ya Muungano kwa kutenga katika bajeti yake ya mwaka huu asilimia 4.5 ya mikopo kupeleka kwa Serikali ya

Mapinduzi Zanzibar. Naomba jambo hili liwe endelevu hadi hapo Tume ya Fedha itakapokuja na *formula* mbadala, ambayo itakubalika na pande zote mbili. Hili ni jambo la kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naupongeza utaratibu ambao upo baina ya Wizara zote mbili za kukaa kufanya kikao chao kabla ya bajeti kutangazwa, wanaita *pre-budget meeting* kwa sehemu zote mbili; hii inasaidia sana kuangalia sera za kikodi na za kibajeti na matumizi ambazo zitakuwa zimeandaliwa kwa upande mmoja haziwezi kuathiri upande mwingine. Kwa hiyo, wakikaa pamoja wanaweza wakagundua athari hizo na kuziweka sawa, kabla pande moja kati ya pande zote mbili haijaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ambalo hata katika hotuba ya mwaka jana nililizungumza; mbali ya ushirikiano huo mzuri, lakini kuna mambo mengine tunaomba yaangaliwe; mmoja nilizungumza mwaka jana na mara hii nalizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taasisi zenye sura ya Kimuungano na Idara ambazo Makao Makuu yake yapo Tanzania Bara, lakini idara nyingine au matawi yake yapo Visiwani; kodi inayokusanywa kwa zile idara za wale ambao wako kule Tanzania Visiwani, kodi inayokusanywa kwa zile idara kwa wale ambao wako kule Visiwani zinaletwa katika Mfuko wa Hazina huku Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya uchumi mkubwa kusaidia uchumi mdogo unaangalia mambo kama haya; tutasaidia vipi upande wa pili. Kwa hiyo, nasisitiza kuwa kodi zinazokusanywa kwa wale wanaofanya kazi kule Visiwani zilipwe kule Zanzibar, kwa maana kuwa hata huduma za barabara, afya, wanatumia kule upande wa pili; kwa nini na wao wasichangie; hivi kutakuwa na athari gani kubwa kwa Serikali ya Muungano kuliangalia hilo na kuliruhusu lifanyike? Naendelea kushauri Serikali ya Muungano ifanye tathmini na iliruhusu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine taasisi hizo mfano wake Polisi, Jeshi, Uhamiaji na nyinginezo zinazohusiana na hizo, kuna haya makampuni ya simu ambayo Makao Makuu yake yapo Tanzania Bara, lakini vile vile kule wana matawi. Kwa hiyo, iruhusu wasajiliwe ili walipie Zanzibar kwa sababu kuna *air time* inanunuliwa kule na watu wa kule wanatumia; hilo lifikiriwe. Hata kwa Zantel ambayo Makao Makuu yake yapo Zanzibar na tawi lipo huko, lisajiliwe tu walipe huku kwani kuna tatizo gani, naomba hilo lifikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ya Muungano inafanya utafiti kuona athari za msukosuko kwa uchumi wa Zanzibar, iliona pia kuna athari za kiutalii na kule Zanzibar Sekta ya Utalii ni tegemeo kwa vile imeathirika pia. Kwa hiyo, naomba hapa Serikali ya Muungano ifikirie kupunguza *corporation tax* kwa makampuni hayo ya kitalii ili yaweze kupata nafasi pana ya kujipanua pengine yanaweza kupunguza gharama ili kuwavutia vilevile watalii waingie katika nchi yetu na kuweza kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengine madogo madogo, sijui kwa nini yanakuwa magumu kutekelezwa; kwa mfano, kule Zanzibar kodi za ndani zinakusanywa Bodi ya Mapato ya kule Zanzibar lakini Kamishna wa Bodi ya Mapato siyo Mkurugenzi katika Bodi ya Wakurugenzi ya *TRA,* kwa maana hiyo Uwakilishi wa Zanzibar katika sera za kodi na maamuzi ya kodi ya Kitanzania kule yanakuwa hayafiki kwa sababu anaingia, lakini si kwa nafasi yake. Kwa hiyo, naomba sana sheria irekebishwe ili huyu Kamishna wa Bodi ya Mapato aingie kwenye Bodi ya Wakurugenzi wa *TRA* kwa nafasi yake; kwa nini *Deputy Commissioner TRA* anaingia kwenye Bodi ya Mapato moja kwa moja kwa nafasi yake kule Zanzibar na ishindikane kuingia katika Bodi ya Wakurugenzi huku Bara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linawezekana kwa sababu tutapata uwakilishi mzuri; maamuzi yatakayofanywa pale yatakuwa ni rahisi kutekelezwa kwa upande wa pili, kwa sababu yule *commissioner* naye atakuwa sehemu ya maamuzi yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya *TRA* Zanzibar kuna idara mbili ambapo huyu *Deputy Commissioner* niliyemzungumza, ndiye anayesimamia Idara ya Kodi za Ndani na Idara ya Forodha. Huyu *Deputy Commissioner* haingii kwenye vikao vya *management team,* kwa maana hiyo mawazo na matatizo ya *TRA* Zanzibar, naomba huyu apewe nafasi awe *full commissioner* na aingie kwenye *management* ili ayawasilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunahitaji kuongezewa *staff,* kuna watumishi wachache katika Kitengo cha *TRA* na wale waliopo wanahitaji kupatiwa mafunzo hasa katika mambo ya *international taxation,* kwa sababu wana-*deal* na *multination companies*. Wanatoka nje huko wanakuja na utalaamu na kijielimu walichopewa; waelimishwe na kupatiwa mafunzo ili waweze ku-*deal* sawasawa na watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wanawake wa Tanzania, pamoja na wanawake wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kilimo. Tanzania hii sote tunaelewa, wanaolima ni wanawake, akina mama wa Kaskazini wanalima mpunga zaidi kuliko hata wanaume, wanaume wanasubiri wali tu kwenye sahani wale, chakula ambacho ndio muhimu kwa kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kitawakomboa hawa akina mama. Wapatiwe mbolea, *scheme* za umwagiliaji zianze kwenye mashamba yao, wapatiwe mbegu bora na mikopo midogomidogo ili waweze kununua madawa ya kuua wadudu, kwani wanateseka sana katika upaliliaji; wakipewa hiyo mikopo watanunua dawa watalima, watavuna na watanunua dawa za kuulia wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi wa mwambao wa Pwani Tanzania Bara na Zanzibar, wanalima kilimo cha mwani kama zao lao la biashara, lakini wanunuzi ni wachache, wanawapa bei ndogo kabisa, kazi wanayoifanya ni kubwa na hawanufaiki kabisa. Wakulima hao hawana uwezo wa kujipangia bei. Kwa hiyo, tuwasaidie hawa watu, tuwasajili nao waunde ushirika na wajipangie bei, vinginevyo tuwahamasishe wawekezaji waje waweke viwanda humu ndani vya kusindika mwani ili wapate soko na wafaidi nguvu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni zao la asali; tunahamasisha vikundi na watu wamehamasika kufuga nyuki, lakini watu wengi wana asali ndani ya mapipa na madebe yapo uvunguni hawajui pa kwenda kuuza na hawajui wafanye nini!

Soko kubwa sana lipo, kwenye hoteli kubwa kubwa kila unapokwenda unakuta kwenye meza kuna vikebe vya asali, kwenye ndege unakuta kuna asali; kwa nini watu wetu tusiwasaidie kupata hilo soko na asali yetu ni nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi kutafuta mitambo midogo midogo ambayo itatumika hata katika *level* ya *household*, wasafishe asali na watafutiwe mikebe ambayo inayokubalika wafungashe asali yao wauze. Vilevile tuwape masharti wenye hoteli zetu hapa kwamba, hakuna ruhusa ya kununua asali kutoka nje wakati inapatikana humu ndani.

Ninaamini tukifanya hivyo, inawezekana kuwasaidia wakulima wetu na ule umaskini tunaouzungumza kuwa tunahitaji kuupunguza, utapungua kwa misingi hiyo. Watu wetu ukiwaelekeza wanafuata na wanakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya mashamba darasa ni nzuri sana na inawaelimisha sana wakulima wetu; wanakwenda wanaona mambo mazuri yanayofanywa pale na wao wanaiga wanalima, wanapata mazao mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwaelekeza watu wetu wanafahamu; tukiwasaidia kwa kuwapa mafunzo, zana bora na mbolea na tukiwasadia katika *skills* za umwagiliaji, watazalisha vizuri zaidi na Tanzania hii tutazalisha chakula cha kututosha kula sisi wenyewe na tutauza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililobakia viongozi wajipange vizuri, watekeleze kama walivyo jipangia. Fedha zitumike kama zilivyopangwa, kusitokee kusema hizi zimetumika hivi, zile zimetumika vile, hatutaelewana wakati wa kufanya tathmini kama zile fedha zimetumika kinyume na ilivyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nishukuru kwa kupata nafasi siku ya kwanza katika kuchangia bajeti yetu. Naomba nianze kwa kutoa shukrani na pongezi nyingi sana kwa Serikali, kwa kazi kubwa inayofanya katika kutekeleza Ilani ya CCM. Kimeainisha maeneo mengi na Kitabu cha Ilani ninacho hapa, nataka kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, kwa kazi kubwa anayofanya kwa faida ya Taifa na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaomba niboreshe tu baadhi ya maeneo, lakini kwa kweli naiunga mkono bajeti. Kabla ya kuiunga mkono hoja, yapo maeneo ambayo nitayazungumzia kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kilimo; kilimo tumeanza kuona kwamba kinahitaji kipewe kipaumbele cha kipekee na kwa utaratibu tuliokwenda nao tunaweza kufanikiwa. Mimi naomba nitumie dakika chache nizungumzie kilimo katika Mkoa wa Morogoro. Mkoani Morogoro, kilimo ni dhahabu ambayo hatujaanza kuichimba. Morogoro ina mito zaidi ya 140, maji yanatiririka mwaka mzima, mabonde ya umwagiliaji ni mengi, ardhi ina rutuba safi na mazao yote twende, mpunga, mahindi, maharage, mbogamboga, matunda, machungwa, maembe na mananasi. Morogoro kuna neema kubwa, sisi tunasema tunamshukuru Mwenyezi Mungu, lakini tunaomba nchi sasa ipige tochi Morogoro. Kwa utaratibu huu tunaokwenda nao, tutaendelea kuwa ombaomba wa chakula. Nawaomba Serikali wafanye kazi ya ziada, kama walivyofanya kwa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga; Morogoro ipewe fursa ya kipekee.

Mwanza na Shinyanga kulikuwa na tatizo kubwa sana la maji, bajeti ikaletwa zaidi ya bilioni 260 zimeingizwa pale, lakini kwa kuwa ni suala la kitaifa, sote tukaliunga mkono. Sasa mambo yanapokwenda kwenye Mikoa mingine kama Morogoro, basi tunatakiwa na Wabunge wengine tuyaunge mkono kwa faida ya nchi na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba kupitia Bunge lako Tukufu, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu; amefanya vikao na ametushirikisha Wabunge wa Mikoa sita, mambo mengi yamezungumzwa, lakini bado naomba Morogoro kama Morogoro ipewe kipaumbele. Kuna mpango wa Mkoa kuwa Ghala la Taifa la Chakula; ni Mpango Maalumu wa Mheshimiwa Rais, tuunge mkono tutaondoka na njaa kwenye Taifa letu. Morogoro ipo katikati; kulia inapakana na Dar es Salaam na kushoto inapakana na Dodoma. Tunaweza kupeleka chakula kikafika maeneo yote katika nchi yetu. Maji yanatiririka mwaka mzima, lakini bado Morogoro kama Morogoro haijafanyiwa kazi sawasawa. Naomba kupitia Bunge hili Tukufu, niwaombe Wabunge wenzangu katika hili tuwe pamoja, faida itakayopatikana ni ya Wabunge wote na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo nina mengi ya kusema, lakini kwa kuwa na mimi nina mambo mengi ya kuzungumza, naomba niishie hapo, nina imani ujumbe utakuwa umefika.

Nirudi kwenye suala la barabara; kwenye mkono wangu nina Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi wa CCM, hiki hapa nakuonesha. Ninatumai unakiona, unakifahamu na wewe ulikinadi. Sisi sote tulikinadi kitabu hiki katika Wilaya ya Mvomero. Katika ukurasa wa 54, Serikali kupitia Ilani hii imesema, Barabara ya Mvomero itajengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hiyo inaanzia Korogwe - Handeni - Mziha - Turiani - Mvomero, inakwenda moja kwa moja hadi Dumila - Kilosa - Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, niishukuru sana Serikali; barabara hii imewekwa kwenye mpango baadhi ya maeneo. Eneo la kwanza ambalo limewekwa kwenye mpango ni Korogwe - Handeni, lina zaidi ya bilioni nane.

Eneo la pili, ambalo limewekwa kwenye mpango ni Dumila kwenda Kilosa, ina bilioni nane, lakini kipande cha katikati kwa maana ya Magole - Mvomero - Turiani sijui

kimesahauliwa au kuna mchezo umechezwa? Wenzangu hawakuniona, sasa mimi sina la kusema, lakini kilio changu na machozi yangu yatatoka tarehe 1 Julai, wakati wa Bajeti ya Miundombinu. Hii ni *package* moja, sielewi kwa nini barabara za wilaya mbili zimepata fedha na wilaya moja haikupata?

*Package* hii naizungumzia Wilaya ya Handeni, Wilaya ya Korogwe, Wilaya ya Kilosa na Wilaya ya Mvomero. Wilaya tatu zimeingizwa, lakini Wilaya ya Mvomero kwenye *package* hii haimo. Nimezungumza kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, nimezungumza kwenye Kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa na leo kwa kuwa Waziri wa Fedha yupo hapa, naamini yeye kama Waziri wa Fedha, barabara yake ya kutoka Dumila kwenda Kilosa hakufanya upendeleo; ile barabara ipo kwenye Ilani, wanaosema Mheshimiwa Mkulo kajipendelea sio sahihi, hakuna aliyejipendelea. Hapa tunazungumzia Ilani ya CCM, kama kusema basi tuseme Mheshimiwa Saddiq kaonewa, lakini tusiseme nani kapendelewa.

Barabara hii ni moja na ipo kwenye Ilani, vipande vyote vitatu vinatakiwa vipate fedha mwaka huu. Mimi niliona kuna bilioni 6.9 zinakwenda Mvomero, lakini ghafla sizioni. Sasa ngoja nikatafute miwani wakati wa miundombinu nije na miwani yangu hapa toka asubuhi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nakuomba sana kaka yangu Waziri wa Miundombinu, chondechonde siku hiyo nitataka kuona Barabara ya Mvomero iwe imekamilisha *package* ya barabara hii. Kuna Ahadi ya Rais, kuna Ilani ya Uchaguzi, mimi nasema yote ni heri, ninachoomba barabara hii kama imesahauliwa basi sasa ikumbukwe.

Ninajua jungu kuu halikosi ukoko, Hazina ni jungu kuu, lakini barabara hii niizungumzie kwa dakika moja. Barabara hii haipiti maporini, inatoka Magole - Mvomero - Tuliani - Mtibwa, ambayo ina urefu wa km 45, inapita kwenye vijiji vyenye watu wengi. Barabara hii inakwenda kwenye Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, inakwenda kwenye shamba la Mitiki Mtibwa, kiuchumi barabara hii inatakiwa ipewe kipaumbele, haipiti kwenye miembe wala mapori. Ukitoka Magome, Kijiji cha kwanza Mgudeni, kijiji cha pili Mvomero, kijiji cha tatu Msufini, cha nne Hembeti, Dihombo, Mkindo, Turiani, Mziha, moja kwa moja mpaka Handeni. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali itakuwa imejiimarisha kiuchumi; kuna kiwanda cha Sukari, kuna Shamba la Mitiki, kuna Chuo cha Kilimo cha Mkindo na mabonde mazuri ya umwagiliaji na ndio mana Serikali ikaiweka kwenye Ilani.

Hapendelewi mtu ila tunachotaka, barabara isaidie nchi katika masuala ya uchumi. Tunapozungumzia uchumi tusiseme mkoa fulani wala mkoa fulani, lilipokuja suala la maji la Mwanza - Shinyanga sote tulipitisha, leo ikitokea Barabara ya Segera, Barabara ya Mvomero, Dumila ni Uchumi wa Nchi. Tuzungumzie uchumi kwa faida ya Taifa. Mimi naunga mkono hoja moja kwa moja, sina kinyongo na barabara nyingine zote, lakini bado nasema tarehe 1 Julai kuamkia tarehe 2, mimi nitakuwepo humu ndani mapema ili nipate nafasi ya kuchangia. Kuanzia kesho sitaomba kuchangia Wizara yoyote, natulia kimya nangojea Wizara ya Miundombinu. Kaka Shukuru Kawambwa, nitaomba unipe taarifa mapema. Hii ni *package* moja, nafikiri nimeeleweka.

Sasa naomba niingie katika kuwasaidia Wabunge wenzangu, hakuna Taifa Duniani linaloendelea bila ya kodi.  Lipo suala la *exemption* kwenye Taasisi za Dini, limezungumzwa sana na mimi naomba nilizungumzie kidogo hili.

Jambo ambalo nimeliona katika Hotuba ya Waziri ukurasa wa 52, nikafuatilia misamaha ya dini, nimekwenda kwenye *VAT Act, Special Relief, third schedule, item number 10*, ile *item* ina mambo mengi; ninachotaka kusema, Wabunge wenzangu, hakuna misamaha ya kodi iliyofutwa kwa Taasisi za Dini, kilichofutwa ni *item number 10* tu. Ninachotaka kusema, niwalaumu wenzetu wa Serikali, hawakutoa elimu kwa Wabunge; leo Wabunge wamepata jazba kwa sababu wanaona misamaha yote inafutwa; *item number 10*, inazungumzia magari ya kifahari na makontena ya mitumba.

Zipo Taasisi za Dini zinazoagiza mzkontena mia moja ya mitumba, nyingine zina agiza VX 10, 20, 30, Serikali inakosa mapato; lakini bado zipo *exemption* nyingine zinaendelea.  Ningeshauri Serikali ifanye haraka sana, itoe Waraka Maalumu kutuelimisha sisi Wabunge.  Mimi naunga mkono kabisa suala la kodi na kila mmoja alipe kodi kwa faida ya nchi yetu.

Bila ya kodi, hakuna Barabara ya Mvomelo, hakuna maji Shinyanga, hakuna mbolea ya ruzuku, wala hakuna *voucher* za mbolea.  Lazima tujipange, katika *item number 10* ya *VAT Act, Special Relief*, kuna mambo mengi yamezungumzwa, sasa pale wenzangu naona wamefanya jazba sana. Sasa ninachoomba, *TRA* wapo, kama inawezekana suala hili ungetafutwa muda haraka sana Wabunge tukaelimishwa.

Misamaha mingine nimeipitia, nimeona bado ipo; misamaha ya mabati, simenti, kwa maana ya ushuru mwingine wa forodha, hakuna ushuru ambao umeondoka. Hapa tunazungmzia *VAT* peke yake, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nawaombeni sana tuangalie suala hili lakini bado Serikali itoe elimu ya kutosha.

Naomba nirudi kwenye suala la ushindani wa kibiashara, nao unatakiwa uangaliwe.  Ushindani wa biashara unaleta manufaa; kuna kipindi katikati, bei ya simenti ilipanda sana, lakini Serikali iliporuhusu simenti kutoka nje bei imekuwa *stable,* sasa hivi simenti utakuta ni elfu shilingi 10, 12, 13.  Mikoa mingine bei iko juu kwa sababu ya usafiri; sasa kama ushindani wa biashara umeruhusiwa kwenye simenti, kwa nini maeneo mengine nako usiruhusiwe?

Leo kwenye sukari bei ni kubwa, kwenye mchele kutoka nje ushuru ni asilimia 75, huku tunalia tuna njaa, lakini tukipunguza ushuru kwenye vyakula na tatizo la njaa litaondoka.  Serikali iangalie maeneo haya, lakini mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nilitoa mchango wangu kwenye maeneo ambayo tunataka tuboreshe na Serikali ipate kodi ambapo hata *TRA* walikuwepo maeneo yote niliweza kuyazungumza.

Jambo lingine ambalo ningependa kulisema ni suala ambalo lipo katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 28; Serikali inakosa mapato sana katika eneo la mafuta.  Leo asubuhi mwenzangu amelizungumza na mimi kama mdau, naomba ku-*declare interest*, kwenye

mafuta mimi ni mdau mzuri. Wapo wafanyabiashara ambao hawana huruma na Taifa letu wala wananchi wetu; wanachanganya diesel na mafuta ya taa. Suala hili, inabidi EWURA sasa watumie meno waliyopewa. EWURA peke yao bila ya TRA, bila ya mkono wa Serikali, hawataweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya nchi yetu, zoezi maalumu linahitajika kufanyika katika Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani, ndiyo unaoongoza katika matukio yote ya uchanganyaji wa mafuta ya taa, diesel na petroli. Ushahidi upo; Kamati mbalimbali zimefanya kazi, mimi kama mdau na kama Mbunge wamekuja kwangu; kuna mfanyakazi mmoja mzuri sana wa TRA, naomba kumtaja jina, anayeshughulikia sekta ya mafuta anaitwa Masamaki. Huyu baba anafanya kazi nzuri sana; anafuatilia magari, vituo vya mafuta na anaokoa mamilioni ya fedha. Kinachotakiwa, watu wa aina hii ya Masamaki wawe wengi. Tumsaidie Mheshimiwa Rais kuokoa mapato, kuongeza mapato, lakini pia kuwaonea huruma Watanzania wanaokimbilia bei za mafuta ambazo ziko chini, matokeo yake wanaumiza magari yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuunga mkono hoja, kwa leo sina tatizo nalo lakini kazi itakuwepo Miundombinu. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Suleiman Saddiq na hiyo tarehe 1 shughuli itakuwepo. Baada ya hapo, nilisema atafuatia Mheshimiwa Ahmed Salum na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae. Mheshimiwa Ahmed Salum, Mbunge wa Solwa.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, nami nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa namna alivyohutubia pale Kilimani. Alitupa sura nzuri sana sisi Wabunge na Wananchi kuona nchi yetu ipo kwenye msimamo gani kwenye mwaka huu wa fedha. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa bajeti yake nzuri na kabla sijaanza kuchangia, niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Kabla sijaendelea, nilikuwa naomba niseme suala moja; kuna fedha zimefika kwa ajili ya kurekebisha umeme katika sekondari tatu za Jimbo la Solwa zikiwemo Sekondari ya Kituli, Samuye na Njwange. Mchakato huo sasa umechukua muda mrefu sana, naomba Wizara ifuatilie, fedha tayari zipo, *TANESCO* wahimizwe kazi hiyo itendeke mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, katika Bunge hili hili, Mheshimiwa Waziri wa Nishati aliniahidi kwamba, Jimbo la Solwa sasa litapata umeme kwenye mwaka huu wa fedha (2009 - 2010). Sasa katika hoja yake, ningemwomba anieleze kama tumepata fedha au ana maana gani, kwa sababu kama ameahidi kwenye Bunge hili na kwenye Bunge hili siku zote huwa hatusemi uongo. Ninasubiri majibu yake na yawe mazuri. Vilevile nipende kusema tu, hata Mheshimiwa Rais alipokuja kuzindua Mradi wa Maji, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Solwa, nilimfahamisha kwamba, mchakato mzima wa suala zima la mradi wa umeme tulishaumaliza na nikamwomba anikandamizie, nipate

fedha Wizarani. Aliahidi kwamba, akija tu Ikulu ataongea na Mheshimiwa Waziri akandamize nipate fedha mradi huo ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nianze na kilimo. Katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, wamesema kwamba, vipaumbele vya pembejeo vitapewa Mikoa ya Kusini kama Ruvuma, Iringa na kadhalika. Hatuna tatizo, maeneo hayo ni mazuri na mazao yakipatikana yatasaidia kwenye maeneo ambayo hayana kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi sisi Shinyanga kwenye maeneo makavu inakuwaje, maana mara nyingi ukame ukitukumba huwa ni ukame kweli kweli inaweza ikafika mahali mpaka ng'ombe anauzwa shilingi elfu ishirini au thelathini; sasa mkitusahau namna hii tutakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuijulisha Serikali kuwa, nilipotembelea Jimbo langu hali siyo nzuri, njaa katika Jimbo la Solwa inanukia. Kata ya Sarae ilinyesha mvua kubwa ikaharibu mazao yote na Kata ya Pandekichiza ilinyesha mvua kubwa mno ya mawe ikaharibu mazao yote. Maeneo mengine yote wanalima mazao yanakua vizuri, inafika mahali labda kiangazi, jua kali au inanyesha mvua kubwa inaharibu mazao. Napenda kuijulisha Serikali kuwa hali siyo nzuri na nimeshamwandikia Mheshimiwa DC, pamoja na Mkuu wa Mkoa na nina imani kabisa Serikali inalifahamu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Shinyanga iko kwenye maeneo ya ukame, naishauri Serikali ijikite kwenye suala zima la kilimo cha umwagiliaji, tupate fedha zinazoweza kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Shinyanga na Jimbo la Solwa kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama China ya Kaskazini, imeweza kupiga hatua kubwa mno kwenye kilimo cha umwagiliaji kinachotumia pampu za umeme. Nitoe mfano mmoja tu, nina *scheme* ya umwagiliaji katika Kata ya Tinde, zaidi ya milioni 250 sijui 400, mvua ikinyesha ndiyo inafanya kazi, lakini kama hakuna mvua haifanyi kazi. Kwa hiyo, utakuta tunapoteza mabilioni ya fedha kwenye *scheme* na haisaidii wananchi wakati tunahitaji kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Lowassa, alikuja kuitembelea Kata ya Samuye. Tulimwambia kuwa gharama ya kutengeneza bwawa ili maji yale yahifadhiwe ni shilingi milioni mia tisa. Mimi naona ni gharama kubwa mno, lakini kama tungeweza kupeleka umeme na *scheme* ya umwagiliaji ikawepo pale, tukachimba visima vitakavyotumia umeme, vitaweza kumwagilia maji wakati wa kiangazi na wakati wa masika bila kujali kwamba tunavuna maji kwa wakati gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijikite sana kwenye suala zima la umwagiliaji wa kutumia umeme au kutumia visima vinavyotumia pampu za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mkulima mmoja tu kati ya watu laki nne, yupo kwenye Kata ya Imesela katika Jimbo zima, aliyeweza ku-*qualify* kupata mkopo wa trekta na leo ana mwaka mzima na ame-*qualify* na sasa hivi anachosubiri ni kupata

mkopo wa trekta. Mkulima huyo anaitwa Gadi Mbindikilo, ambaye anakaa kwenye Kijiji cha Mwamajuda na mpaka sasa hajapata. Kwanza, nimwombe Waziri wa Wizara husika, anieleze kwa nini hajapata na ali-*qualify* na kila kitu kilikamilika anachosubiri ni kupata trekta tu?

Kwa hiyo, ninachoiomba Serikali ni kwamba, mtindo huu wa mikopo umekaa kibenki benki, kwa hiyo, wakulima ambao ni walengwa hawatapata hii mikopo ya pembejeo. Watapata wachache tu wenye ufahamu, ambao tayari wana dhamana, lakini niiombe tu Serikali ione namna ya kuzishirikisha Halmashauri zetu ziweze kushiriki vizuri ili hawa wakulima waweze kupata pembejeo vizuri, kinyume na hapo haiwezekani. Mimi nimetoa mfano wa mkulima mmoja, leo kwenye bajeti hii nasikia kuna TIB nayo inaongezewa fedha, yale yale mabenki tu; hivi Wakulima wa Mwakitoro, Lyabukande, sijui wa Didia, hawaelewi chochote, hawana dhamana ni kazi nzito kweli. Kama kweli tunakusudia kilimo ni kwanza, basi naomba tuone namna nyingine ya kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye elimu. Mkoani Shinyanga au Jimbo la Solwa, tatizo kubwa ni upungufu wa walimu. Moja kati ya sababu inayosababisha upungufu wa walimu ni kwamba, kwa mfano, tulipangiwa walimu 110, lakini walioripoti ni 70 tu, wengine wote wameondoka wameshindwa kuishi kwenye mazingira yetu. Sasa moja kati ya ushauri ninaoutoa ni kwamba, kwanza, hii Shelcom iharakishwe iwe kituo cha kufundishia walimu ili walimu wapatikane kwenye maeneo yetu. Wakipatikana kwenye maeneo yetu ni rahisi kwenda kufundisha, kwa sababu tayari maeneo hayo wamekwishayazoea. Unamtoa mwalimu Ilala au Kinondoni unampeleka Lwakitoryo; ni ngumu kweli kweli lazima ataondoka tu na hiyo ni moja ya sababu za upungufu wa walimu katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tuliyopata mwaka huu Mkoa wa Shinyanga ni kidogo mno, ukilinganisha na jinsi inavyochangia kwenye Pato la Taifa. Mwaka jana ilichangia shilingi bilioni 90, mwaka huu shilingi bilioni 165, lakini fedha tunazozipata katika Mkoa mzima wa Shinyanga hasa katika suala zima la miundombinu. Nitoe mfano wa Barabara ya Old Shinyanga – Sarawe; kwanza, imeharibiwa na wakandarasi wa China hawa katika suala zima la mradi wa bomba la maji. Barabara wameiharibu kweli kweli na kila tukiomba fedha za kutosha, tunaletewa fedha utadhani za kuomba, hailingani na Mka wa Shinyanga. Naiomba Serikali ituongeze fedha Mkoa wa Shinyanga, hasa kwenye suala zima la miundombinu na barabara zake ili mwaka ujao tuweze kuchangia zaidi ya shilingi bilioni 165 kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala zima la bandari. Niliongea kwa muda mrefu mwaka jana nikasema, bandari hii imewashinda na nasema itazidi kuwashinda na hawaiwezi, kwa sababu tunaichukulia kama kitu kidogo mno kana kwamba labda sijui ni kitengo tu kwenye Wizara wakati nchi nyingine wanaitumia bandari kama pato kuu. Haya yote tunayoyaongea Waheshimiwa Wabunge, upungufu na ufinyu wa bajeti, kama bandari peke yake ingekuwa inasimamiwa vizuri, ingeliweza ku-*raise* mpaka shilingi trilioni 14 na uwezo huo upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya matatizo ya Bandari yanaletwa na TRA; *procedures* ni ndefu. Sasa naomba niongelee maeneo mawili; mizigo ya ndani na maeneo ya *transit.*

Mizigo ya ndani kuna TISCAM na kuna *pre-lodge* ambayo una-*lodge* ndani ya TRA, ile mizigo ambayo ipo *under value 2500.* Sasa hivi wame-*introduce system* ya ASISCAN, mimi nadhani ni muhimu kabla haja-i*ntroduce* chochote, kwanza, mnaifanyia kazi. Sasa hii *system* mpya imekoroga kuliko ilivyokuwa kwanza; una-*lodge document*, TISCAM wanakufanyia *price verification*, wanauliza kwenye nchi husika ili kujiridhisha ile bei ya ama mzigo, kontena au gari, hiyo *process* peke yake si chini ya siku 10 au siku 14. Wakati data zote za bei ziko ndani humu humu, sasa wewe unauliza kule data wakati ziko pale unauliza nini?

Kwa hiyo, tungekuwa na *cash program* ya kuondoa mizigo yetu kutokana na *record* ya bei ambazo tayari tunazo, mtu una-*lodge document*, TISCAN wanakufanyia *price verification*, wanauliza kwenye nchi husika kujiridhisha ile bei ya ama mzigo, kontena au gari.

Kwa hiyo, mizigo inayokuwa *off-loaded* kutoka kwenye meli, *containers* zinaweza zikatoka 100, zinatoka 20, halafu tena zinatoka 70, zinatoka 10, kutaacha kuwa na mrundikano wa makontena pale bandarini na *data base* wanazo zina faida gani? Kwa hiyo, mrundikano wa makontena bandarini, unasababishwa na *process* za TRA kwa asilimia 70 au 80.

Sasa hivi mizigo yote ya wafanyabiashara wa Burundi, Rwanda na hata Tanzania, inakwenda Mombasa, sio kwamba wanakwepa kodi, wanachokitaka kule ni uharaka. Mafanyabiashara anachokijali ni muda, akienda Mombasa kontena siku mbili linatoka. Akifikisha *border* kutoa mzigo wa kontena pale Mombasa ni milioni tano, mtu analipia *on transit fee*, analipia lori, yupo tayari kulipa milioni tano lakini mzigo wake aupate haraka. Anakuja *border* analipia ushuru zaidi, ukija kupiga gharama zile ni zaidi ya ushuru anaolipia Dar es Salaam, lakini anachofuata kule ni uharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari imewashinda. Mimi nashauri kitu kimoja; kwanza, *TRA* watafute njia zitakazowawezesha kuondoa mizigo haraka. Pili, niishauri Serikali, kwa sababu sasa hivi Miundombinu na *TRA* wanatupiana mzigo; Miundombinu anasema *TRA*, *TRA* wanasema Miundombinu; Serikali ifikirie kuwa na muundo wa Wizara ya Bandari. Bandari ni kitu kikubwa, sio Wizara tu sijui ya Michezo, lakini inatakiwa kuwe na Wizara Maalum ambayo tunaweza tukamkamata hapa Waziri wa Bandari akatujibu, lakini leo unamkamata nani sasa? Waziri wa Miundombinu atakwambia bwana ni *TRA* wanachelewesha mimi sina tatizo, ukienda *TRA* watakwambia Miundombinu bwana wale sijui nini; sasa utamakata nani? Halafu juu ya hivyo, bandari ni kitu ambacho tukikikamata vizuri, tuka-*specialize*, itatuongezea zaidi ya shilingi trilioni 14 na kuondoa matatizo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninadhani ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nikupongeze kwa kunipa nafasi jioni hii ya kuweza kuzungumzia bajeti yetu. Pili, naomba nimpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba yake ya kilimo ambayo aliitoa mbele ya Wabunge na Wazee wa Dodoma. Naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu masuala ya mabenki. Bajeti ya mwaka jana, nilizungumzia sana kuhusu Mabenki ya *CRDB*, *NBC* na *NMB* kuwa, yamejikita sana mijini na wilayani. Tunasahau kuwa, kama Serikali ingeweza kuiwezesha na kuipa mtaji Benki ya Posta, ambayo iko katika wilaya zote nchini na sehemu nyingine iko sehemu za Tarafa; kwa sababu kuna watu wanaoitwa walimu, wako sehemu mbalimbali vijijini mwetu, kila kona ya nchi hii yuko mwalimu, lakini huyo mwalimu hana huduma bora, tunamsahau kabisa na vilevile watendaji wengine ambao wanaishi ndani ya Tarafa na ndani ya Kata na sehemu nyingine za vijijini ambao wanapata mishahara kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mwalimu tunayempa mshahara, kwa mfano kule kwetu Mkoa wa Rukwa, anatokea Kasanga na Kasanga haishi pale Tarafani, anaishi ng'ambo ya ziwa; kuna sehemu wanaishi kwenye vitongoji vya ziwa; avuke maji aje Tarafani, atoke Tarafani aje mpaka Mkoani Sumbawanga, hapo anaweza kuchukua siku mbili na ametumia pesa yake ya mshahara. Akifika pale Sumbawanga aende Benki na mwisho wa mwezi benki moja tu ya *NMB* ndio ambayo inatoa mishahara ya walimu; anakaa kwenye foleni kuanzia asubuhi mpaka saa 12 jioni, hapo huyo mwalimu anashindwa kurudi nyumbani kwake Kasanga inabidi alale, anatumia mshahara wake. Akitoka hapo akirudi mpaka anafika katika kijiji anachofundisha, ameshatumia nusu ya mshahara wake aliopewa na Serikali.

Serikali ikijipanga vizuri na kuweka mikakati mizuri na kusema kuwa sasa hivi ni lazima tuweke mabenki katika Tarafa, huyu mwalimu atapata huduma bora pale pale Kasanga, lakini bado haijaweka misingi mizuri ya kuweka Mabenki ndani ya Tarafa. Tutakuwa tunalaumu walimu hawataki kwenda vijijini, wanakosa vyanzo vingi vikubwa ambavyo ni vya kuwatunza katika matumizi yao. Huyu mwalimu ana watoto anataka kusomesha, ana familia yake; ana baba na mama ambao wanamtegemea; ule mshahara ambao umeshatumika nusu kwa ajili ya kwenda kufuata mshahara wake; ndio maana anakata tamaa ya kwenda sehemu ambazo hazina huduma. Ninaiomba Serikali iongeze mtaji katika Benki ya Posta ili iweze kutusaidia Tarafani na ndani ya Kata zetu ili watu wanaoishi kule, waweze kupata huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha *SACCOS*, lakini haziendi vijijini kwa kuwa wanakaa na zile pesa majumbani kwao na wanaji-*risk*. Wewe utakaaje na pesa nyumbani, maana unajua saa yoyote utavamiwa na majambazi utaibiwa wana-*SACCOS* watakuja watakudai wewe muweka hazina wa *SACCOS*. Ndio maana *SACCOS* zetu haziendelei vijijini. Ninaomba Serikali ijipange vizuri, hii Benki ya Posta iende vijijini ili wananchi wanaoishi maeneo yale waweze kufaidika. Wanaofaidika sasa hivi ni watu wa mijini tu; vijijini pia kuna wafanyabiashara ambao wanakaa kule hawana sehemu ya

kuweka pesa zao. Hata Bunge lililopita nilisema kuwa, tunasema uchumi haukui, pesa zipo. Nilisema kuwa, sisi kule kwetu Mpanda, Wilaya ya Mpimbwe, kuna wakulima wazuri wanafukia hela zao; utakuta mkulima ana milioni 30 anaitia chini ya udongo anaizika; sasa ile hela aipeleke wapi?

Hakuna kitu chochote ambacho kinamuwezesha kwenda kuzipeleka zile pesa. Ninaomba Serikali mjipange, muweze kuiongezea mtaji Benki ya Posta iweze kufika katika kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera yetu ni kilimo kwanza. Katika maeneo yetu ya vijiji, vitongoji na kata; baadhi hatuna Mabwana Shamba na tunataka kilimo bora. Sasa huyu mkulima wa kijijini Ilunde, hana hamasa ya Kilimo na wala hajui vocha inatoka lini na mbolea inatoka lini kwa sababu hakuna Bwana Shamba aliyeko maeneo ya kule. Huyu Bwana Shamba yupo katika maeneo machache na vilevile hana pikipiki wala baiskeli. Tutamuwezeshaje huyu mwananchi ili aweze kulima kilimo ambacho kinaweza kumletea manufaa katika nchi hii? Ninaiomba Serikali ijipange; kuna chuo cha Uyole kiko Mbeya kinatoa Mabwana Shamba wachache sana na kuna wengine wamemaliza chuo lakini mpaka leo hawajachukuliwa wala hawajui waende wapi. Sasa kama tumeamua kweli kilimo kwanza, vile vyuo vyote ambavyo vinafundisha Mabwana Shamba, wanapotoka pale wachukuliwe wapelekwe kwenye maeneo mbalimbali ili waweze kwenda kuwasaidia wananchi ni jinsi gani ya kujipanga ili waweze kulima kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kusema kama Mheshimiwa Selelii kwamba, Hazina walaaniwe, hapana, lakini Hazina ni tatizo na wana urasimu mkubwa mno. Pesa za maendeleo ambazo zinapelekwa ndani ya Halmashauri yetu *(OC)* ni lazima zichelewe. *OC* zozote zinazokwenda hata kwenye mashirika ambayo yako ndani ya Wizara zinachelewa. Hazina wanachelewesha hata fedha za madeni ya Wazabuni wa Shule za Sekondari, kiasi ambacho wazabuni hao wanakata tamaa. Tutabadilika lini? Kama Hazina hawana kitengo kikubwa cha kushughulikia masuala ya maendeleo, waongeze staff. *OC* ya mwezi uliopita mpaka sasa hivi kuna sehemu nyingine bado hawajapata; kuna nini Hazina?

Miradi ya Maendeleo kuna sehemu mpaka leo hii haijaisha na ukiuliza unaambiwa hela hazijafika kutoka Hazina. Hazina huyo huyo, pensheni kwa wastaafu ni shida. Unakuta mstaafu amekaa miaka miwili, mitatu, minne, hajapata pensheni yake. Mtu amestaafu tangu mwaka 2000, mpaka leo hii pensheni yake hajapata, tatizo Hazina. Hazina wana urasimu mkubwa mno, tunaomba Serikali mjipange upande wa Hazina kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa zahanati *(dispensary),* katika tarafa zetu. Katika zahanati au *dispensary* kuna muuguzi mmoja au mganga mmoja na kuna semina iko wilayani au mkoani; yule mganga anaenda wilayani au mkoani huku *dispensary* inafungwa; hivi kweli tutakwenda na semina ile inaweza ikakaa siku saba? Lazima Serikali ijipange vizuri, wananchi wengi wanapoteza maisha yao kwa sababu ya huduma finyu ambazo zinatokea maeneo ya vijiji vyetu. Kuna pesa za akina mama na vijana, ambazo tunaambiwa zinatoka katika Halmashauri zetu, mimi sijawahi kuona hata

siku moja katika Wilaya ya Mpanda kama vijana wamepata hela kutoka Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache kwenye bajeti hii. Kwanza, nasimama hapa kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Babati Mjini na hivyo nataka kuwahakikishia kwamba, yale yote ambayo nimezungumza nao ya kuletwa ndani ya Bunge hili, nitayafikisha katika kipindi hiki kwa njia mbalimbali na njia moja ni nafasi niliyoipata leo. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Pili, bila shaka tuna haja ya kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo imeifanya katika kipindi kilichopita, tuna miradi ambayo inaendelea katika majimbo yetu na katika maeneo yetu mbalimbali, ambayo mingi inaendelea vizuri na kwa hiyo, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi unakwenda vizuri katika maeneo hayo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitumie nafasi hii kwenda moja kwa moja kwenye bajeti yenyewe. Naomba nianzie ukurasa wa 40 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu Wizara ambazo ambazo zimepata kipaumbele. Mheshimiwa Waziri, ameeleza Wizara ambazo zimepewa fedha kama kipaumbele kuwa ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Afya, Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati na Madini. Sasa kwa ajili ya uzoefu mdogo nilionao, naomba nizungumzie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ukurasa wa 40 mpaka 41, Mheshimiwa Waziri amesema, Sekta ya Elimu imepewa kipaumbele kwa kutengewa shilingi trilioni 1.7 au shilingi bilioni 1,743.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuwe wazi zaidi katika eneo hili la kusema kwamba Sekta ya Elimu imepewa kipaumbele. Kuwa wazi maana yake ni nini? Maana yake Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ameomba shilingi bilioni 377.6 kwa matumizi ya kawaida na mishahara. Ameomba pia shilingi bilioni 129.8 kwa Miradi ya Maendeleo, jumla ya fedha ambazo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ameomba ni shilingi bilioni 507.4, huku tumesema Sekta ya Elimu imepata kipaumbele kwa kupewa shilingi trilioni 1.7 au shilingi bilioni 1,700.4. Sasa ni vizuri tukapata ufafanuzi na jambo hili likaeleweka kwa wananchi kwamba unaposema Sekta ya Elimu umeipa kipaumbele wakati Waziri mwenye dhamana ya Elimu umempa shilingi bilioni 507 tu, hizi nyingine shilingi trilioni 1.2 au shilingi bilioni 1,236.5 zimekwenda wapi; zipo kwenye Wizara zipi; na je, ni Elimu ambayo inatekelezwa chini ya Wizara ya Fedha; mambo ya elimu ambayo yanatekelezwa chini ya Wizara ya Afya; au ni mambo ya elimu ambayo yanatekelezwa chini ya Wizara ya Miundombinu au Kilimo?

Lazima tujue hizi zimekwenda wapi, kama Wizara ya Elimu yenye dhamana ya kusimamia elimu na ubora wake tumeipa shilingi bilioni 507, shilingi trilioni 1.2 ziko kwenye Wizara nyingine; tunataka kujua kipaumbele hasa maana yake ni nini hapo? Najua nyingine zitakuwa TAMISEMI na sehemu nyingine, lakini tunataka tupate ufafanuzi kwa maandishi kwamba zimekwenda wapi ili sasa tuzifuatilie na tuone kama

kweli zinatumika kwenye Sekta ya Elimu au namna gani. Kwa hiyo, vilevile katika Wizara nyingine ambazo zimepewa kipaumbele ni vizuri tukajua mambo haya yamekwenda namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kila mtu hapa anafahamu, hakuna nyumba ambayo mtoto haendi shule; kila nyumba mtoto anakwenda shule na ndio jambo ambalo linamgusa kila mwananchi. Karibu kila kaya kuna watoto wanakwenda sekondari na sasa hivi tunao wengi. Katika Kitabu cha Hali ya Uchumi na Mipango, Waziri amekiri kwamba, sasa hivi wanafunzi wa elimu ya juu wameongezeka kutoka elfu sitini mpaka karibu laki moja na kitu. Sasa ni lazima tujue kwamba, tunaposema kipaumbele kipo kule, tuone Wizara hii inapewa fedha namna gani na tunasimamiaje hiyo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nihame hapo, lakini nataka nikubaliane na watu wanaosema zipo shule zina walimu wawili au watatu. Matatizo haya ni ya kweli kabisa, sasa tunajielekeza vipi kule; nyumba za walimu hakuna, vifaa vya maabara hakuna, tunayo matatizo makubwa kwenye Sekta ya Elimu. Kwa hiyo, tunaposema tunatoa kipaumbele tunapeleka fedha namna gani kule?

Nataka niendelee na eneo hilo hilo la elimu kwamba, katika bajeti ipo miradi ya elimu ambayo ipo kwenye taasisi zote; iwe ya elimu ya juu, sekondari na kila mahali. Ipo miradi ambayo fedha tumezipitisha hapa, lakini taasisi hizo au vyuo hivyo vikuu havikupata fedha zote hizo. Wengine wamepata 20%, wengine 50% na wengine 70%, sijui ni vigezo gani vinatumika kwa sababu kama tunatenga fedha hapa na haziendi zote kule zinakotakiwa kama zilivyoombwa na Waziri muhusika, basi tunalo tatizo. *Performance* inakuwa ni 50% au chini, sasa tutaimarisha namna gani? Kwa hiyo, lipo hilo tatizo na nina hakika kwenye Wizara nyingine vilevile tatizo hilo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililoliona ni ongezeko la mwaka jana na mwaka huu; Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi mwaka 2008/2009 kwenye miradi ya maendeleo aliomba shilingi bilioni 129.5, ndizo tulizopitisha hapa na mwaka huu zilizopo kwenye vitabu hapa ni shilingi bilioni 129.8, tofauti ni kama shilingi milioni 215.7 tu. Sasa hapo tumetoa kipaumbele wapi? Shilingi milioni 215.7 tu ndio tofauti kati ya bajeti ya miradi ya maendeleo ya mwaka jana na ya mwaka huu, kwa hiyo, kuna kazi ya kufanya hapo.

Lingine, kwenye sekta hiyo hiyo, madeni yanaathiri sana bajeti ya Wizara zote na kwa hii ya elimu nataka nitoe mfano kwamba, ukishaweka madeni ya mwaka uliopita unayapeleka kwenye mwaka unaofuata basi kuna tatizo kubwa sana. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, sote tunafahamu, wana madeni makubwa ya walimu na walimu ni zaidi ya 50% ya watumishi wote wa Serikali hii. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa sana hapo.

Pili, mwaka jana kipindi kama hiki Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilikuwa na mahitaji ya shilingi bilioni 29 kulipa madeni ya chakula. Nadhani Serikali iliweza kuonesha kama shilingi bilioni saba tu kwenye bajeti yake. Kwa hiyo, nina

hakika hii bajeti ambayo tumeendelea nayo, ambayo inakwisha sasa, bila shaka watakuwa wametumia fedha nyingine kulipa madeni. Je, wataendelea vipi kutoka pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya tatu ni mambo ya huduma na ya nne ambayo ndio ninataka niisemee kwa uzito zaidi ni Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Bodi ya Elimu ya Juu, kwa sasa hivi bado inadaiwa shilingi bilioni 23.3 na Vyuo Vikuu na Taasisi zake; tutaendeshaje Vyuo Vikuu na Taasisi zake kwa madeni ya aina hiyo? Serikali haikutoa hizi fedha. Mbaya zaidi, miaka mitatu mfululizo 2007/2008, 2008/2009 na sasa 2009/2010, Serikali imepanga fedha zile zile kwenye Bodi kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi (shilingi bilioni 177). Kwenye kitabu cha mipango, Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekiri kwamba, lengo moja ni kuongeza udahili katika mpango wa 20009/2010. Amesema kabisa sehemu ya pili, *"kuongeza usajili wa wanafunzi wa elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo."* Unaongezaje usajili; umepanga fedha zile zile na ni miaka mitatu mfululizo na sasa mapengo ni makubwa sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ilikuwa na lengo la kuwapa wanafunzi 65,000 na hapa tumekiri wanafunzi wa elimu ya juu wako laki moja na zaidi. 65,000 ni wale wanaokidhi vigezo vya kupewa mikopo, lakini wala haikuwezekana, Bodi waliweza kutoa mikopo kwa vijana 56,363 tu, kwa hiyo, bado tuna kazi kubwa.

Kwa wale ambao wanaendelea tu wanahitaji shilingi bilioni 119, wale wanaoendelea wa mwaka wa kwanza ongezeko ni shilingi bilioni 19.2. Wanaoendelea wa mwaka wa kwanza wa kozi ya sayansi na kozi ya ualimu, ongezeko litakuwa shilingi bilioni 44.2. Wale wanaoendelea na wa mwaka wa kwanza wa kozi ya sayansi na ualimu na wenye *Division I* na *II* watahitaji ongezeko la karibu shilingi bilioni 80, jumla Bodi ya Mikopo inataka karibu shilingi bilioni 197, sisi tunatoa shilingi bilioni 117, upungufu shilingi bilioni 80. Nataka kuiuliza Serikali; je, inashindwa kutafuta hizi shilingi bilioni 80 kwa ajili ya wanafunzi wetu kwa ajili ya kujenga rasilimali watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali inajenga majengo mengi sana, makubwa, mazuri na ya gharama kweli kweli, lakini huu si wakati wa kujenga majengo, huu ni wakati wa kuongeza rasilimali watu. Tuna upungufu, hatuna walimu kwenye shule za Kata kila mahali, tunataka tuwasomeshe watoto hawa waende Vyuo Vikuu, tuwapeleke kule wakaidie. Huu si wakati wa kuhangaika na rasilimali majengo, tuhangaike na rasilimali watu kipindi hiki.

Ushauri wangu, ninaiomba Serikali itafute shilingi bilioni 80 na mkiweza kutueleza kwamba zinapatikana wapi na isiwe tena maneno hapa, hatujui ziko wapi na tunataka Waziri atueleze anaipaje Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hizo shilingi bilioni 80 na pengo hili unaliziba namna gani; sio kwa kujibu tu kwamba, tutaziba, tutatafuta, hapana; kwa sababu bajeti ndio hii tunayoipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo katika mfumo wa ufuatiliaji wa tathmini ya miradi ya maendeleo; Waziri ametueleza kwamba, amewafundisha Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tarafa na Maafisa Bajeti 532, lakini bado ukiangalia Ripoti ya CAG, haitupi

matumaini mazuri; yapo matatizo makubwa; je, viongozi hawa wanasimamia vitu gani? *(Makofi)*

Wakienda huko bila shaka wanakuta mikataba mibovu, miradi imechelewa, uwezo mdogo, sheria za manunuzi zinakiukwa na mambo mengi na hata upatikanaji wa taarifa ni mgumu.  Tunataka kujua Wakuu wa Wilaya mliowafundisha wanasimamia nini? Maafisa Bajeti karibu 532 mliowafundisha wanafanya nini; na kwa nini haya mambo yanaendelea kujitokeza kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali?  Je, kwa nini hatufiki mahali tukasema sasa mwisho ni hapa, tunataka kama ni majengo yasimamiwe kweli kweli?  Yapo matatizo makubwa sana katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na kilimo kwanza, maana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kule naye kwenye shule zake wameandika elimu kwanza.  Waziri Mkuu naye amekuja na jambo zuri la kilimo kwanza, sasa vile vibao vilivyoandikwa sasa tunafanyaje.  Kwa hiyo, tuseme yote ni kwanza tu na tusisahau kuwa kilimo ni uti wa mgogo.  Vibao vya shule vimeandikwa elimu kwanza, maana wananchi wanaweza kuchanganyikiwa watasema sasa elimu kwanza basi tuondoe kilimo.  Vibao vingine vya shule vimeandikwa elimu ni ufunguo wa maisha, sijui elimu ni ukombozi, elimu kwanza, haya mambo lazima tuyaweke vizuri na wananchi wapate elimu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, suala la barabara tutalizungumza vizuri tutakapokuja kwa Waziri wa Miundombinu.  Tumesema kwenye Ilani kwamba, tutajenga barabara kwa kiwango cha lami.  Barabara ya Iringa – Dodoma - Arusha ipo ukurasa wa 156 kwenye Ilani, lakini kwenye bajeti shilingi bilioni tano; inaanza lini na mwaka ujao ndiyo mwisho wa hii Ilani; mmesema kabisa 2005 mpaka 2010 Barabara ya Iringa - Dodoma - Arush?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.  *(Makofi)*

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:**  Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika bajeti ya mwaka huu. Kwanza, ni-*declare interest* ya kuwa, mimi nipo kwenye utalii, kwa hiyo, nitazungumzia utalii kidogo.

Katika *speech* ya Mheshimiwa Rais, alikuwa anazungumzia njia ya kuweza kuvutia watalii waje Tanzania na nchi iweze kufaidika na pesa za utalii.  Kwa kufanya vile, alisema anapunguza gharama za *Visa* kutoka dola mia moja mpaka dola hamsini. Sasa mimi nashindwa kuelewa kama alikuwa *mislead* au ana maana gani, kwa sababu kwa mtu yeyote anayeingia Tanzania kwa sasa *Visa* ni *fifty dollars* na ile inalipwa *at the point of entry*.  Sasa kama ni kuwavutia watalii, nina imani kabisa kwa sababu alikuwa anasema mtalii hatalazimika kwenda kwenye mbuga zetu, kama Kenya anaweza kuwaona wanyama wale wale kwa dola 25, nadhani alikuwa anamaanisha ni *entry* au *park fee* ya kuingia kwenye zile mbuga za wanyama.  Kama maana yake ni ile haijavutia, kwa kuwa sasa hivi bado tunalipa *fifty dollars* kwa *park fee*, tunalipa *fifty dollars* kwa *entry* na *entry* ya kupanda Mlima Kilimanjaro ni *sixty*.

Kwa hiyo, sijui alikuwa ana maana gani, labda Waziri ataniambia hii ina maana gani; maana *Visa* kupungua kutoka dola 100 kuja 50, hapa haina maana, kwa sababu mtalii anakwenda mbugani kuangalia mnyama na kama anataka kupunguza ili watalii waongezeke, tulikuwa tunatumaini angepunguza kutoka ile hamsini ya sasa ije kwenye ishirini na tano, tuwe sawa na Kenya, ambazo ndizo wanalipa watalii wanapokwenda kuangalia wanyama porini. *(Makofi)*

Kwa hiyo ni matumaini yangu, Waziri atakapokuwa anaeleza, atatueleza maana ya *Visa* hapa ni nini kwa sababu sasa hivi tunalipa dola hamsini *entry* ya kuingia kwenye *national park*, kwa hiyo, inafanya ile *speech* ya Rais isiwe na maana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia hilo labda nije la pili, kuhusu kilimo kwanza. Tunasema kilimo kwanza, lakini katika bajeti yetu kama tukiangalia kwa mpangilio kwa ugawaji wa pesa kilimo ni namba nne. Sasa maana ya kilimo kwanza ni nini; kama kilimo ni kwanza ingepata *allocation* ya pesa kuliko Wizara nyingine zozote ndiyo tungeweza kusema kwa uhakika kilimo kwanza, kwa sasa hivi kilimo sio kwanza. Tukitaka kufanya uchumi wa nchi hii ufufuke au uendelee ni lazima tuwekeze kwenye kilimo, hiyo sina ubishi nayo. Lazima tuanze kuvisaidia vyama vyetu vya ushirika na hata kama ni kuwapa pesa, Serikali ingesaidia ili wakulima wetu waweze kulima na kuweza kujipatia kipato cha kutosha. Tukitaka kupata zaidi, lazima tufikirie kuanza kilimo cha kibiashara *(Commercial Farming).* Bila kuwa na walimaji wakubwa katika nchi hii, tukategemea mwananchi mmoja mmoja kutosheleza nchi hii chakula na ziada ya kuuza nje ipatikane hatutafika.

Tuna utata hata katika kilimo cha *commercial farming,* kwa sababu hatuna ardhi, tunasema Tanzania ni kubwa, lakini kila mahali ukienda kugusa utaambiwa ni ardhi ya kijiji. Sehemu zile ambazo sio eneo la vijiji ni maeneo ambayo hakuna mtu anayeweza kufika kufanya kilimo, sasa tunajikuta tuko kwenye matatizo. Labda tutakapoanza kutengeneza ile *land bank* ambayo tutaweza kuipangilia, tujue ni sehemu ngapi ambazo ziko wazi ambazo tunaweza kuanza kuwapa watu, labda hapo tutakuwa tumejikomboa. Hii nayo itatupa matatizo, kwa sababu ni ardhi gani ambayo Tanzania leo utaigusa mwenyeji asiseme ni sehemu ya kijiji, mimi sijui kama ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafuata Kitabu cha Bajeti, ambacho kimesema misamaha ya kodi itafutwa yote katika NGO na Mashirika ya Dini isipokuwa vile vifaa vya kiroho na ibada. Kitabu hiki kimeandikwa na mimi nakifuata kwa sababu ndiyo msahafu wenyewe wa bajeti. Hayo mengine wanayoyasema wenzangu mimi siyaelewi, lakini madhehebu ya dini yamejikita katika vijiji wanatoa elimu, wengi wetu tumesoma katika shule za misheni na wengi wetu tunakwenda kwenye hospitali za misheni. Wakinyimwa misaada hii ni kwamba, tunajijengea mazingira mabaya, ambayo hatutaeleweka kwa wananchi na Serikali itakosa uaminifu kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba Serikali ifikirie upya ni kweli kuna watu ambao wame-*misuse* hii misamaha, lakini kama kuna mtu ame-*misuse* ni jukumu la Serikali kuwakamata na kuwashtaki wakati hakuna aliyekwishashtakiwa, maana yake ni kwamba, hakuna mtu aliyekwisha *misuse.* Mimi naamini hivyo, kwa sababu nchi yoyote ina sheria zake na kama mtu akivunja sheria au kanuni, lazima akamatwe. Huwezi kuniambia kuna *NGO* zimeagiza

makontena mia moja wakaja kuyauza barabarani, wameagiza magari wameyauza kwa nani; ile misamaha ina sababu zake na kanuni zake na kama mtu akivunja kanuni zile anawajibika kwa Serikali na Serikali ingetuambia inafuta hii misamaha kwa sababu fulani.

Hivi sasa huduma inayotolewa na haya madhehebu ya dini ukitizama Hospitali za Mwanza zile za Wakatoliki acha zahanati ambazo ziko vijijini, acha *universities* ambazo zipo tayari sasa zinahudumia wananchi wote bila kubagua dini wala rangi ya mtu; mimi nadhani itakuwa ni kosa kubwa na Serikali itakuja kubeba mzigo mkubwa ambao utawashinda. Sasa turudi katika migodi ambayo tumesema tunataka kufuta msamaha wa *petrol*, mimi nafuata hiki kitabu tumesema tunafuta msamaha wa *petrol*, lakini mitambo yote kule inatumia *diesel*, *unless* kuna *interpretation* nyingine hapa; ni kwamba, hatujafanya chochote, *petrol* inatumika katika vigari vidogo vidogo na ni *very specific*. Wamesema *petrol*, wangesema angalau *petroleum product* yote labda ningeelewa, lakini ukisema ni *petrol* wale kule watakuja kugeuka ile *diesel* bado wao wanaendelea kutumia na mtu asibishe ndiyo iliyoandikwa, huku kumeandikwa *petrol* hapajaandikwa *diesel*. Kwa hiyo, lazima tuwe *very careful*, Waziri atakapokuja ku-*windup* aseme ana maana gani; ana-*define petrol* kama kitu gani, asipo-*define* ni kwamba, wale mabwana wakubwa wanaochimba bado tumewaacha na *diesel* yao na mafuta. Mafuta ya taa na mafuta machafu yote yale bado yataendelea kuwa yanaruhusiwa, watakuwa wamekatazwa *petrol* peke yake. Kwa hiyo, tuwe *very careful* katika kutafsiri haya tunayoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, lazima tugusie Bandari yetu ya Dar es Salaam. Mheshimiwa mmoja amezungumza vizuri sana, tumekuwa na *mind-set* inayosababishwa na kufikiria msongamano wa makontena pale kwenye Bandari ya Dar es Salaam, TICTS lakini sio TICTS; tuna mawazo mabaya kabisa, msongamano wa pale unatokana na *TRA documentation*. Mimi ni mtu wa *shipping*, naelewa ninachokizungumza; *documentation* tuna matatizo, Enzi za Mwalimu ilikuwa mzigo unatoka kwenye meli unautia kwenye gari moja kwa moja unaupitisha *documentation* wiki mbili kabla meli haijafika, unakuta umeshapata *manifest* ya mizigo ya meli yote na ikifika inakwenda kwenye lori moja kwa moja, sasa hivi haifanyiki hivyo. *(Makofi)*

Sasa hivi utakwenda kwa kijana wa *declaration* pale *custom* atairudisha itakaa wiki moja. Tumeweka makampuni ya ajabu ajabu, bila sababu tunatengeneza njia za watu kula; *port auth*ority ilikuwa inatosha kabisa hawa watu wengine tumewaweka wa nini? Tunaweka mlolongo wa kuchelewesha, ndiyo unaofanya ile bandari inazidi kuwa imejaa, halafu ndiyo bandari pekee katika eneo letu hili ambayo ingeweza kutupatia mapato makubwa ya ajabu.

Tumeambiwa Mombasa sasa hivi imepanua bandari yake, zinaingia meli mpaka zinazobeba tani laki tatu, sisi Dar es Salaam, tunafikiria kwenda kujenga bandari nyingine Bagamoyo; maana yake nini hii hapa hatujamaliza kuijenga tunakwenda Bagamoyo? Jamani tufikirie *priority* zetu, tunaacha ku-*improve* Kiwanja cha Ndege Dar es Salaam ili ndege ziweze kuja nyingi, tunasema tunataka kwenda kujenga Kiwanja cha Ndege Bagamoyo. Tuna Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro hakitumiki *even five percent*. Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam ambacho kingetuletea mapato makubwa

hakitumiki *even fifteen percent,* kinatakiwa kuwa *improved* hatujafikia Jomo Kenyatta Airport, ndege zinaruka pale Kenyatta Airport kila dakika sisi Dar es Salaam tuna nini, badala ya kufanya kile kilichoko pale sasa kitufaidishe kituletee mapato, tunazunguka tunasema tunakwenda kujenga Bagamoyo kwa kuwa Mheshimiwa Kikwete anatoka Bagamoyo ndiyo tunapeleka kiwanja kule? Kwa kuwa Rais anatoka kule tunasema tunataka kwenda kujenga bandari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi angalau na mimi nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Awali ya yote, baadaye unipe mwongozo wako Mwenyekiti juu ya kutenguliwa kwa kanuni na kwamba baada ya kupitisha Hotuba ya Bajeti tutapitisha pia Muswada wa Fedha. Kwa maana hiyo, Bunge hili litakuwa limeidhinisha matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010; kunakuwa na maana gani tena baada ya kupitisha *Finance Bill* halafu tuanze kuzipitia Wizara moja moja ambazo tayari matumizi yake tumeshaidhinisha? Nitaomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nilikuwa na mambo mawili, matatu, hivi ambayo nataka niyazungumze. Kwanza, yako maeneo ambayo napenda sana kuipongeza Serikali, kwa hatua ambazo wamechukua na hasa eneo la kuondoa ushuru kwa dawa za binadamu. Nawapongeza sana katika hatua hiyo ni kwamba, itawasaidia sana wananchi kuweza kupata dawa kwa bei nafuu ili hata wale maskini pia waweze kupata matibabu. Hofu yangu, sijui Serikali imejipanga kiasi gani katika kusimamia eneo hili, vinginevyo msamaha huu utawanufaisha wafanyabishara na bila kumnufaisha huyu ambaye tunamkusudia kwamba ndiyo anufaike kutokana na msamaha utakaotolewa. Kuna mtu ambaye atakuwa anasimamia bei za madawa, hofu yangu ni kwamba, wafanyabiashara wata-*enjoy,* lakini bei pengine zisiweze kuteremka hata kidogo. Hilo lilikuwa ni eneo moja ambalo nilikuwa na mashaka nalo, lakini naipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo.

Aidha, nilikuwa na mashaka pia juu ya msamaha utakaotolewa kwenye magari makubwa; ni kwamba, unalenga magari gani; magari mapya au tunalenga mitumba ya magari? Hii ni kwamba, sasa waende wakaokote magari yaliyotupwa kule Uingereza, Ulaya na Uarabuni, yaletwe Dar es Salaam kwa sababu hakuna ushuru; ni lazima tuangalie pia katika eneo hilo kwamba, kama hili litaruhusu magari chakavu, bado Serikali haitakuwa imepata nafuu yoyote, tutaendelea kubeba mzigo katika njia nyingine kwa maana ya vipuli na gharama za kuendesha yale magari. Hatari iliyopo ni kwamba, inawezekana sasa Tanzania ikawa ndiyo jalala la magari makubwa ambayo yameshatoka kabisa. Nilikuwa napenda tu kutahadharisha katika maeneo hayo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lilikuwa bado linanitia mashaka ni hali ya mfumko wa bei. Kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi iliyotolewa na Waziri, sasa hivi tuko kwenye asilimia 12; hali si nzuri ni lazima ziwepo juhudi za makusudi kabisa za kutaka kudhibiti kabisa mfumko wa bei. Mashaka yanaongezeka zaidi pale bei ya mafuta inapoanza kuongezeka; leo asubuhi Dar es Salaam lita ya diesel ilikuwa shilingi 1300,

sasa kama Dar es Salaam ni shilingi 1300, Mpanda itakuwa shilingi 1600 au 1700. Hali ya mfumko wa bei na uwezo wa watu wetu kununua vitu, bado inanitia mashaka kwamba safari yetu ni ngumu sana huko tunakokwenda.

Lingine, pamoja na uhuru mkubwa ambao umetolewa wa kuruhusu bidhaa ziingizwe nchini, ifike mahali kama Watanzania pia tuangalie kwamba ni bidhaa gani ziingizwe, zipi tunazihitaji na zipi hatuzihitaji; sio kila aina ya bidhaa ya mfanyabiashara anayofikiria kutaka kuileta katika nchi hii anaileta. Nimefadhaishwa sana nilipokwenda kwenye duka moja pale Kariakoo, nikakuta fagio za nyasi zinaagizwa kutoka India; hivi kweli Tanzania tumefikia kiasi hicho kwamba sasa hata fagio za kufagilia nyumbani tuagize kutoka India? Lazima Serikali iangalie maeneo hayo, vinginevyo uchafu wote utaletwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye eneo la kilimo; nazipongeza jitihada za makusudi kabisa zinazochukuliwa, pamoja na kaulimbiu ya kilimo kwanza, napenda nichukue fursa hii kuikumbusha Serikali kwamba, kama hatutakuwa na mipango endelevu, basi kila wakati tutakuwa tunakuja na mipango mipya. Kilimo kwanza ni kaulimbiu ambayo inaweza ikaleta tija na pengine isiweze kuleta tija hata kidogo kwa sababu tumeanza kuzungumzia kilimo toka tumepata uhuru wa nchi hii.

Katika awamu hii ya nne ya uongozi wa nchi yetu, kulikuja Mpango wa Maendeleo ya Kilimo *(Agriculture Sector Development Program),* ambayo tuliambiwa hapa Bungeni, trilioni za fedha zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kilimo, lakini hatujui zimetumika kiasi gani, tumepata mafanikio kiasi gani, tumeshindwa wapi na tujisahihishe vipi. Tunakuja na mpango mwingine; ni vizuri hii mipango tunayoibuni ifike mahali tujaribu kujitathmini kwamba tumefanyaje vizuri katika maeneo haya, labda tutazame mpango wa elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa elimu ya msingi ulikuwa mzuri sana, lakini leo ukiihoji Serikali kwamba tumefanikiwa kwa kiasi gani; watakwambia suala la watoto waliosajiliwa *(enrolment)* basi, lakini hawawezi kusema tumefanikiwa kiasi gani katika elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nitumie hili Gazeti la Mwananchi la Alhamisi Juni, 4; hapa pana Shule ya Msingi ya Tandahimba, hii ndiyo shule ya Tanzania katika Karne ya 21. Siwezi kusema kwamba, shule zote za Tanzania zinafanana na hii Shule ya Tandahimba, lakini tatizo la upungufu wa madarasa katika shule za msingi bado ni kubwa. Tumesahau tumeacha wala hatuzungumzii tena habari ya elimu ya msingi, watoto wanasoma hawana madawati wanakaa chini, kuna msongamano na walimu hawatoshelezi, lakini tunaona tumepiga hatua kwa sababu tume-*enrol* zaidi ya asilimia mia moja. Sasa mafanikio ya aina hiyo yanatutia upofu wa kutokuona matatizo yetu, kwa hiyo ni vizuri wakati mwingine tukae tuangalie hizo *programs* zetu ambazo tunazitengeneza; matatizo yake ni nini, tusijivunie yale mafanikio.

Mfano, katika Halmashauri yangu ya Mji wa Mpanda, nina upungufu wa madarasa ya shule za msingi yanayokaribia zaidi ya mia moja, uwezo wa wananchi

kujenga madarasa hayo haupo tena. Mwananchi huyo huyo unataka ajenge zahanati, ajenge barabara, ajenge sekondari, ajenge nyumba ya mwalimu, ajenge hiki na kipato chake kinapungua. Kwa hiyo, lazima tufike mahali sasa tuangalie na hawa tu ambao tunawabebesha mizigo. Lazima tuwahimize wananchi wachangie katika maendeleo yao, lakini pia tuangalie na uwezo wa watu wetu, pale ambapo Serikali sasa inaweza kuweka juhudi zake isaidie mahali ambapo wananchi wameshindwa kukamilisha. Hivyo hivyo ukienda katika elimu za sekondari nako ni matatizo, hatuna vyumba vya kutosheleza vya maabara, hatuna madarasa ya kutosheleza na kadhalika na kadhalika na sasa tunakuja katika elimu ya juu; ni lazima tufikie mahali kama taifa tuangalie kwamba tumekosea wapi na ili mipango yetu iwe endelevu ni lazima tuwe na mipango ya kuendelea.

Kwa mfano, huko nyuma mara baada ya uhuru, mwaka 1965 walianzisha mpango wa kwanza wa maendeleo ya miaka mitano na ukafuatia na awamu ya pili. Kwa hiyo, walikuwa wanajua wanaanzia wapi, wamefika wapi na wanakwenda wapi, lakini baada ya mpango wa pili wa maendeleo ya miaka mitano mitano, nchi hii imekuwa haina mipango yoyote ya maendeleo; kila mmoja anakuja na mpango wake kwa kadiri anavyoona inafaa. Kwa hiyo, tunaweza kwenda hivi kwa karne nzima bila kufikia maendeleo ambayo tunayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie umuhimu wa vipaumbele vyetu; ni kweli tumeamua kuweka vipaumbele katika kilimo, elimu na miundombinu, nakubaliana navyo; lakini tunaposema kwamba tumewekeza katika elimu, tunatoa elimu ya namna gani?

Hili eneo ni lazima tuliangalie, nchi zile za *mini-tiger* zimeweza kufaulu na kufikia hatua waliyofikia kwa sababu waliwekeza katika elimu. Elimu waliyokuwa wameijenga ilikuwa ya kumuwezesha anayeipata aweze kufanya kazi ya kujiajiri. Elimu tunayoitoa leo Tanzania haimuwezeshi huyo aliyeipata kuweza kujiajiri. Kwa hiyo, lazima tubadili mitazamo ili tuwaandae hawa vijana waweze kwenda katika soko la ajira bila kutegemea kupata kazi maofisini. Kwa kufanya hivyo, naamini kabisa tutapiga hatua mbele zaidi katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho na la umuhimu zaidi ni Barabara ya Tunduma - Sumbawanga, najua katika bajeti ya mwaka jana ilionekana na mwaka huu imeonekana tena; hela za MCC hebu Serikali ituambie, hatuwezi kila mwaka inajenga mazingira magumu hasa katika Mkoa wa Rukwa.

Kwa bahati mbaya sana, Mheshimiwa Rais, ameizungumzia barabara hiyo, Mheshimiwa Makamu wa Rais ameizungumzia barabara hiyo, aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lowassa, aliizungumzia barabara hiyo, Mheshimiwa Pinda ameizungumzia barabara hiyo, lakini haijaanza kujengwa. *Position* ya hizi hela za MCC iko vipi; waambie wananchi ukweli kuliko kuwapa matumaini kwamba barabara itajengwa leo, itajengwa kesho; inawajengea mazingira magumu na kutokuaminika kwa viongozi mbele ya wananchi. Mheshimiwa Rais, amekuja amesema mwaka huu itajengwa, mwaka wa fedha wa Serikali umeisha barabara haijaanzwa kujengwa!

Nitapenda nipate maelezo ya kina, juu ya fedha hizi ambazo zinatoka kwa hawa Wamarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia ni kuhusu kilimo cha mikataba. Bahati nzuri sana, kaka yangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ana uzoefu wa kutosha kabisa juu ya kilimo cha mikataba, kwa sababu kimefanyika katika jimbo lake kwa zaidi ya miaka 40. Anajua hali ya Wakulima wa Tumbaku; Wakulima wa Tumbaku wanaendelea kuyanufaisha makampuni, wanalima kwa mikataba, kwa hiyo, tahadhari zichukuliwe wasiingie katika mikataba kama hiyo ambayo inawatesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni reli. Mheshimiwa Lucas Selelii, aliizungumzia kwa mapana sana lakini nisipoisemea kwa kweli najiona kama vile sijajitendea haki mimi mwenyewe. TRL wakati inaanza ilianza na mabehewa zaidi ya 1300, leo ina mabehewa yanayotembea chini ya 600.

Bahati nzuri, juzi Mheshimiwa Rais aliposema kuhusu reli kule Kilimani watu walishangilia, akasema tatizo kubwa ni *management* na mtaji. Sasa kama tatizo limefahamika wamechukua hatua gani? Nataka Serikali inieleze hatua ilizochukua juu ya *Management* ya TRL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Arfi, katika mchango wake ametaka maelezo kuhusiana na suala ambalo tulilifanyia maamuzi juzi; la kwamba, baada ya kupitisha *Finance Bill*, kutakuwa na mantiki gani kuendelea kujadili Wizara moja moja.

Kwanza, nimjulishe kwamba, jambo hili ni maamuzi ambayo Bunge liliyafanya juzi baada ya mawasilisho yaliyofanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Philip Marmo. Pili, pamoja na sababu nyingine, sababu ambayo ilitolewa ni kwamba, kwa kodi ambazo mabadiliko yake yanaanza tarehe 01 Julai, 2009, jambo hilo litaiwezesha Serikali kuanza kukusanya fedha Julai Mosi.

Tukienda kwenye Kanuni; Kanuni ya 97 inasema: “Katika hatua hii ya majadiliano tunayoifanya, majadiliano yatahusu mambo ya jumla kuhusiana na hali ya uchumi na Mbunge yeyote hataruhusiwa kupendekeza mabadiliko katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali.”

Kanuni ya 98 inasema: “Mjadala huu wa hatua ya bajeti utakapomalizika, Spika atalihoji Bunge litoe uamuzi wake wa kupitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya ibara ya 90(2)(b) ya Katiba.”

Ibara ya 98(2) inasema: “Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.” Jambo ambalo litafanyika mwishoni mwa wiki hii.

Kanuni ya 99: "Jumla ya siku zisizozidi hamsini ambazo tumezitengua, zitatengwa kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa Wizara zote." Kwa hiyo, kitakachofuata ni kujadili utekelezaji zaidi.

Mwisho, nimkumbushe kwamba, kifungu cha 105 kimeweka utaratibu na hakijatenguliwa; nacho kinasema kwamba: "Tutakapofika mwisho, *Appropriation Bill* itasomwa na itapitishwa kwa utaratibu wake kama kawaida kama inavyofanyika siku zote."

Baada ya hapo, naomba sasa Mheshimiwa Herbert Mntangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kwanza, kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa somo alilotupa kuhusu mtikisiko wa uchumi duniani, lakini pia mwelekeo katika Sekta ya Kilimo. Nawashukuru sana Wizara hii ya Fedha, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa maandalizi ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza pale nilipoisoma taarifa ya hali ya uchumi na nimevutiwa sana na kupata matumaini nilipolisoma eneo moja katika hotuba hiyo. Mimi nilitazama hali ya mikopo. Katika taarifa hiyo ya uchumi, inaonekana kwamba, hali ya mikopo imeanza kubadilika na mabadiliko ambayo yamenivutia ni pale nilipoona mikopo imeanza kutolewa katika sekta mbalimbali na katika sekta binafsi imechukua nafasi ya juu zaidi.

Ukitazama mchakato ulivyo pale, mikopo katika sekta binafsi imechukua 19.6% wakati mikopo inayokwenda katika sekta ya biashara ni 16.1%, lakini katika uzalishaji viwandani ni 13.1%. Kwa nini nafurahia mikopo kupanda katika sekta binafsi ?

Nafurahi kwa sababu moja kubwa; Watanzania wengi pamoja na mimi, kwa mfano, katika ujenzi wa nyumba tumekuwa tukizoea kujenga kwa fedha taslimu *(Cash Basis).* Unajenga nyumba lakini fursa za mikopo zinapoanza kutoka na zikafikia sekta hii binafsi, maana yake ni kwamba, tutapunguza kasi ya ujenzi wa kutumia fedha taslimu katika uwekezaji wetu na fedha hizi tutazigawa ili tuweze kuziwekeza katika sekta nyingine zitakazosaidia kuinua uchumi wa nchi. Naomba hili liendelezwe na mikopo iendelee kuwa wazi, mingi na kwa kiasi kikubwa zaidi kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazame sasa suala la Mapato ya Taifa. Taarifa zinatuonesha hapa kwamba, Mapato ya Taifa yamekuwa yakishuka; kwa mwaka wa 2008 yameshuka kwa 9% na mwaka huu wa 2009 inaelekea yanazidi kushuka pengine kwa 10%. Unapozungumza asilimia haiingii vizuri, hebu tutazame kwa tafsiri ya fedha, mapato yatakuwa yanashuka kwa kiasi cha shilingi 480 bilioni.

Kwa tafsiri hiyo, hiki ni kiasi kikubwa sana na kinagusa mwenendo mzima wa Taifa letu. Kwa hiyo, lazima tujiulize hivi tunashuka kwa kiasi kikubwa namna hii kwa sababu tu ya mtikisiko wa fedha wa dunia peke yake? Kwangu mimi hapana; yapo mambo muhimu ambayo ni lazima tuyatazame; kwa mfano, mbona katika Bandari yetu ya Dar es Salaam kuna ongezeko kubwa sana la makontena pale; hivi tunayafanyia tathmini vizuri na kukusanya kodi ipasavyo?

Leo ukienda kwenye Bandari ya Dar es Salaam kila mahali pamejaa magari tu, hakuna hata mahali pa kuweka makontena; hivi magari yote yale yanatozwa ushuru unaostahili ?

Lazima vilevile tujiulize kwamba; kuna nini kwenye sehemu ya kushushia mafuta pale Kurasini Oil Jet; na kwa nini mara kwa mara *flow meter* inaharibika? Kwa hiyo, mafuta yanapita bila kurekodiwa pale. Lazima tujiulize na mambo mengine; hivi kweli tunaposema tunatoa misahama ya kodi kwenye mafuta kwa mfano kwa hawa watu wa Sekta ya Madini na tunaposema kwamba msamaha huo utaanza tarehe 01 Julai, 2009 maana yake tumefanya mabadiliko ya Sheria? Tunapofanya mabadiliko ya Sheria maana yake ni kwamba, kila mtu anapaswa kuifuata Sheria hiyo kuanzia tarehe 01 Julai, 2009.

Suala la kusema kuna wengine huko walikuwa na mikataba na hizi kauli ambazo tunazisikia eti Serikali itakwenda kuzungumza na wale wanaohusika, nataka niwaambie ndugu zangu kwamba, tuna uhakika na tumeona jinsi watendaji wetu walivyokuwa dhaifu katika *contract negotiations*. Tunakwenda kujadiliana nao nini wakati sisi ni dhaifu katika majadiliano? Hapa tunaacha mianya ya rushwa kwa sababu watakwenda kupiga mahesabu, sisi tuta-*save* kiasi gani kama tutaendelea kuwa *exempted* mabilioni ya fedha. Wewe huna uwezo wa *capacity negations;* hivi utakwenda kumwambia nini huyo ambaye anapaswa kulipa?

Mnafanya *negotiations* ili asilipe, atakushawishi na utashawishika, jibu tunaloliona ni kwamba hawatalipa. Sheria imebadilika, Sheria ni ya nchi na sote tunapaswa kuifuata kwa tarehe tutakayokubaliana, *exemptions* hapana sisi ni wadhaifu kwenye *negotiations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale ndugu zangu wa madini walipe, kwa sababu Sheria inasema sote tunalipa; hakuna *exemptions* wala hakuna masuala ya mijadala hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la miundombinu, yaani Wizara ya Miundombinu. Wizara ya Miundombinu wanaanza bajeti mpya ya mwaka 2009/2010, wakiwa na upungufu wa fedha ambazo hawakuzipata katika bajeti iliyopita. Sasa upungufu huo ni zaidi ya wastani wa shilingi bilioni 90, wanaingia mwaka mpya wa fedha wakati shilingi bilioni 90 za kipindi cha bajeti iliyopita hawakuzipata, tunategemea nini ? Tutafika mwaka 2010 asilimia kubwa ya kazi zilizopangwa hazitakuwa zimetekelezwa, lazima tuiangalie hali hii.

Hebu tuangalie Wizara hiyo makadirio yake katika Sekta ile ya Maendeleo, wametarajia kupata shilingi 13.6 bilioni kutoka ndani na fedha kutoka nje shilingi 33.9 bilioni. Historia inaonesha miaka miwili iliyopita fedha hizi tulizokuwa tukitegemea kutoka kwa wahisani, zilifika kwa kiasi kidogo na kwamba mwaka huu tunaouzungumza, wahisani wameongeza fedha kidogo. Tuna uhakika gani kwamba katika kipindi kinachokuja wahisani kutoka nje watatupatia fedha kama walivyoahidi? Mimi nawafahamu ndugu zangu wa Norway ni watu waaminifu sana, tunaweza kuwategemea lakini tusiweke 100% katika makadirio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala moja dogo, lakini kwanza nimalizie suala la miundombinu. Mkoa wa Tanga ulikuwa miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa iingizwe katika Mpango Maalum wa PMMR, lakini kwa bahati mbaya haukupata fedha katika kipindi kilichopita kutokana na utekelezaji wa wasiwasi katika mikataba. Sasa lazima tukubaliane, wenzetu wa mikoa mitatu wamepata fedha, sisi Mkoa wa Tanga hatukupata; maana yake ni kwamba barabara zetu zimeathirika sana hasa barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani na barabara inayotoka Pangani kuja Mkuzi hadi Kilulu na Muheza Mjini zimeathirika sana. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea kabisa kwamba, *Tanga East na Tanga West* katika mpango huu, mwaka huu tutapewa kipaumbele na barabara hizo zitatengenezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze machache kuhusu misahama ambayo imekwishaanza kuleta wasiwasi. Ukiisoma taarifa kama ilivyo katika Kitabu cha Bajeti, utaona kauli iliyotolewa na Kiswahili kilichopo pale, inaleta picha kama misahama yote imefutwa. Watu wangu wa Muheza, ambao wanaitegemea sana Hospitali Teule ya Taasisi ya Dini, wamenipigia simu wakiwa na hofu kwamba gharama zitapanda, kwa sababu hiyo, nikafanya jitihada za kutafuta tafsiri halisi.

Kimsingi, alichokizungumza Mheshimiwa Mbunge wa Mvomero ni sahihi. Ukienda kwenye eneo lile la VAT, utakuta kuna jedwali pale linaloonesha vifaa vyote ambavyo vitapata msamaha katika Sekta ya Afya na anayetengeneza jedwali hilo ni Waziri wa Afya. Bahati mbaya, Maaskofu, Masheikh na hata sisi Waheshimiwa Wabunge, jedwali hilo hatuna. Nina uhakika kama tungelipata vifaa vyote muhimu vya kupimia na kadhalika, vimeainishwa na vimeorodheshwa kwamba vitapata msahama wa kodi; ningeomba Mheshimiwa Waziri utusaidie hilo jedwali ili liende kwenye Taasisi za Dini na Waheshimiwa Wabunge pia walipate. Msimamizi wa Jedwali hilo ni Waziri wa Afya, nina imani Waziri wa Elimu vilevile katika eneo lake naye atakuwa na jedwali lake.

Upande mwingine wa jedwali, ukienda katika kodi hizi za Afrika Mashariki katika eneo lile vilevile Sekta zile zimeainishwa kwamba, Taasisi hizi za Dini katika Sekta ya Elimu vifaa gani vitakuwa *exempted* na ni vyote muhimu mpaka chaki zimo mle. Watu hawajui hilo na kwa sababu hawalijui ni haki yao kulalamika. Tutoeni hofu kwa kutupatia vielelezo vya uhakika ili tuweze kusema kwamba, kwa kweli hakuna aliyeonewa. Taasisi za Dini zinasema sasa Serikali imetugeuka wamesahau tulikotoka na kwamba, hamthamini tena kazi kubwa waliyoifanya.

Nadhani Shule za Kata tulizojenga zinatosheleza, lakini vilevile tusisahau kwamba bado wanatupenda na bado wanaendelea kutusaidia, wametuunga mkono hapa Dodoma kwa Vyuo Vikuu na wanaendelea kutuunga mkono katika maeneo mengine mbalimbali. Nina uhakika, taarifa sahihi zikiwafikia basi huu mgongano utakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa leo niishie hapo, ninakushukuru sana na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Herbert Mntangi, kwa mchango wako. Kama nilivyosema, anayefuata ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo atakuwa Mheshimiwa Bernadeta Mushashu.

Mheshimiwa Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, karibu.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na jopo lote la Wataalamu wa Wizara ya Fedha, kwa matayarisho mazuri ya Bajeti. Mwisho na siyo kwa umuhimu, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa jinsi alivyotuelezea ile tunaita Mkakati wa Kunusuru Uchumi wetu, alitupa somo zuri na tulilielewa. *(Makofi)*

Kabla sijasahau, ningependa nisisitize kwamba, Hotuba ya Mheshimiwa Rais kuhusu Mkakati wa Kunusuru Uchumi wetu, ingelipaswa kuwa sehemu ya majadiliano pekee, yaani isichanganywe na bajeti kama hivi; ingelikuja kama ilivyo, tukaichambua kama ilivyo na hasa *financial implications* zake kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo; ni kwamba, taarifa mbalimbali tulizokwishazipata ainaonesha kwamba, kasi ya ukuaji wa uchumi wetu kufikia mwishoni mwa mwaka huu itateremka kuanzia 7.4% ya mwaka 2008 mpaka kufikia 5%. Hii inatisha kwa sababu ili nchi yetu tuweze kuondoa umaskini, tunahitaji kasi ya ukuaji wa uchumi wetu isiwe chini ya 8%.

Kwa hiyo, kama tutakuwa tumekwenda kufikia 5%, maana yake tuna kazi ya ziada na hususan tutakapokuwa tumeelewa kwamba ili uchumi wetu uweze kuuondoa umaskini chini ya MKUKUTA ni lazima ukue kwa 8% - 10%, sasa hivi tuko kwenye 5%; hiyo inaonesha jinsi tulivyo na kazi kubwa ya kuweza kuuondoa umaskini katika nchi yetu. Sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea na kazi kama kawaida, kwa lugha ya kigeni ina maana kwamba, *business as usual;* tutakwama. Lazima tuwe wabunifu na tuangalie ni maeneo gani yanaweza kusaidia uchumi wetu kukua haraka, pamoja na mtikisiko wa uchumi duniani. Maeneo haya ni pamoja na yale ambayo yamekwisha orodheshwa na wenzangu waliotangulia kuongea, mimi ninayasisitiza, kweli kilimo kwanza kwa sababu 80% ya Watanzania wanaajiriwa katika Sekta ya Kilimo.

Pili, limezungumzwa suala zima la Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; hii ni rasilimali na huu ni mgodi wetu wa dhahabu mwingine tunachotakiwa ni kuuuchimba tu. Bandari iko pale, watumiaji wako DRC, Uganda, Rwanda na Burundi, suala ni kwamba tunawafikiaje? Lazima tuwe na reli madhubuti na barabara madhubuti zinazokwenda huko. Sasa huu ni uamuzi ambao uko wazi na dhahiri, tunapata kigugumizi sana kutengeneza barabara inayodumu kuanzia Dodoma mpaka Kigoma, kupanua Bandari za Kigoma na Dar es Salaam, kuongeza ushindani katika Bandari ya Dar es Salaam kwa maana ya kuruhusu makampuni mengine yafanye kazi ya kupakua na kupakia mizigo. Sasa hili lina tatizo gani? Uamuzi ni wetu, nchi ni yetu, barabara ni zetu, ardhi ni yetu, reli ndiyo hiyo mbovu, sasa tatizo ni nini mpaka tunaachia watumiaji wa Bandari wanakwenda Mombasa, wanakwenda Afrika ya Kusini ili waje Congo? *It is a shame!*

Kwa hiyo, tukiwekeza huko kwa haraka zaidi tutauamsha uchumi wetu tena mara moja, kwa sababu kama ni mzigo Congo upo, Rwanda upo na Uganda upo, kwa hiyo hilo hebu tulichukulie hivyo na tuelekeze uwekezaji wetu kwenye maeneo haya.

Kabla sijasahau, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kulitambua tatizo la Shirika letu la Reli. Shirika letu la Reli lina matatizo mengine mengi, licha ya tatizo la ukongwe wa reli nyenyewe wala si mwekezaji peke yake. Mwekezaji anaweza kuwa ni sehemu ya tatizo, lakini huyu tuendelee kuongea naye tena kwa haraka. Kwa habari nilizonazo ni kwamba, Serikali inaongea naye, lakini nahisi inaongea naye kwa *speed* ya taratibu hebu tuongeze *speed*. Hata zile dola 44 milioni ambazo Mheshimiwa Rais ametamka kwamba, zitapatikana kutoka World Bank, haziwezi kupatikana kama hatujawekana sawa na mwekezaji huyo ambaye ndiyo Meneja. Kwa hiyo, hilo tulimalize sambamba na kuzisubiri pesa kutoka IFC.

Vilevile naipongeza Serikali kwa kuelewa kwamba, reli yetu imechoka na kwa sababu imechoka inahitaji mawekezo makubwa katika kipindi cha muda mfupi; tunazungumza na *World Bank* na nchi nyingine watatusaidia. Katika kipindi cha muda mrefu, ninafurahi vilevile kufahamu kuwa Serikali ina mpango wa kuitengeneza reli hii upya tena kwa geji pana kuliko ya sasa hivi hiyo. Naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo hili la barabara ya kutoka Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma kwa nini inakuwa ni dondandugu? Bahati mbaya sana kuna barabara fupi kutoka Nzega mpaka Tabora, ukiweka lami pale unaiunganisha Tabora na barabara kubwa inayotoka kule Mwanza mpaka Dar es Salaam (kilomita 115) Tunahangaika nazo miaka nenda rudi, tunafanya uchambuzi yakinifu, kilomita 115 jamani tunangojea msaada kutoka nje; nani aje kukusaidia kujenga kilomita 115 *as a country?*

Watu wa Tabora wana matatizo kulia na kushoto, wakitaka kupita njia ya Itigi tabu, kupanda treni tabu, kupita Nzega tabu, sasa hawa watu wa Tabora wakiwanyima kura kama Serikali mtawaambia nini mtawalaumu? Wana kila sababu ya kuisema hii Serikali imetusahau na imetuacha. Kwa hiyo, wakifanya maamuzi ya kusema hapana, tunajaribu chama kingine tunafanyaje? Mimi kama Mwana-CCM nasema hatujachelewa,

bado tuna miezi 18 ya kurekebisha hali hii ili Wana-Tabora warudishe mioyo yao kwa CCM. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya Bajeti kwa muhutasari inatoa picha ambayo si sahihi, inaonesha kwamba, safari hii matumizi yetu ya ndani ni makubwa kuliko mapato yetu ya ndani. Ukiangalia katika muhtasari wake, inaonesha kwamba, hatutakuwa na mchango kwenye bajeti ya maendeleo, lakini je, hili ni kweli? Si kweli; ukienda kwenye Kitabu cha Maendeleo, utakuta maeneo mbalimbali ya maendeleo yanaonesha *foreign component* na *local component.* Sasa hii *local component* inatoka wapi kama kwenye Kitabu cha Bajeti inaonesha *there is no surplus* kutoka kwenye *Recurrent Budget* kwenda kwenye *Development Budget?* Rekebisheni hilo ni tatizo, mtu akisoma sura ya bajeti kama inavyoonekana inaonesha wazi kabisa kwamba, hakuna mchango wa *Recurrent Budget* kwenye *Development Budget,* sura hii iko wapi? Siyo sahihi irekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakopa kama sehemu ya kuboresha mapato yake ya ndani, lakini mikopo hii ya ndani ina sehemu mbili; sehemu moja takriban shilingi bilioni 576 ni kwa ajili ya kulipia dhamana zilizopevuka, shilingi 506.0 bilioni ni kwa ajili ya kuziba pengo la bajeti. Suala la msingi la kujiuliza ni kwamba, hizi za kuzibia pengo la bajeti hivi tunazikopa kwa utaratibu gani; utaratibu wa *Treasury Bills* au utaratibu wa *Government Bonds?* Uelewa wangu ni kwamba, kama ni *Treasury Bills,* muda mfupi zitakwenda kwenye *recurrent expenditure*, kama ni *Bonds*, muda mrefu zitakwenda kwenye *development*, lakini tuambiwe basi.

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, amesema katika hotuba yake kwamba, tutaanza kuuza *bonds* zetu za ndani kwa ajili ya miundombinu, lakini *budget speech* hii iko kimya! Mimi nilidhani hii *budget speech* ingesaidia ku-*link* maelezo ya Mheshimiwa Rais na jinsi tunavyozungumza hapa ndani; *Infrastructural Bonds* ziko wapi hapa? Hazipo! Kwa maana ya kusema hizi nyingine 506 bilioni zitakuwa *Treasury Bills* tu au zitakuwa *Bonds*, lakini tuzitumie kwa kuziba pengo la matumizi ya Serikali; *that is bad planning*, huwezi kukopa muda mrefu kutumia matumizi ya muda mfupi, kopa muda mrefu uwekeze kwa maana ya *investment* ndicho kinachotakiwa. Kwa hiyo, turudi kwenye meza zetu, tuangalie hizi *Infrastructural Bonds* ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baya zaidi ambalo nataka niitahadharishe Serikali ni kwamba, hizi pesa zitakazokopwa hapa chonde zisikopwe kutoka *Central Bank*, tukope kutoka kwenye pesa zinazozunguka katika uchumi, ambazo tayari zipo katika *circulation.* Hilo nalo liko kimya, kwa hiyo, tujihadhari mwisho wa siku tunaweza kujikuta Serikali imekopa kutoka Benki Kuu ya Nchi, hiyo itakuwa tunazidisha mfumko wa bei, tatizo tulilonalo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashangaa, Kiwanda cha Matairi cha Arusha kwa nini tumekitupa? Kama kiwanda chochote ili kiweze kufanya kazi ni lazima kiwe na *local base*, hivi hatuna *local base* ya matairi Tanzania? Kwa nini matairi yote yanayotumika Tanzania ni *imported?* Hivi sisi tuna pesa za kigeni za kutosha kununua matairi? Hivi hatuna haja ya kuwaajiri watu wetu katika viwanda vyetu na wao

wakaajiriwa, yaani sisi tuwe tunawaajiri watu wa nje tu wenye viwanda vyao vya nje watuletee mali sisi tutumie basi?

Tumeondoa ushuru kwa 10% kwenye mafuta ya kupikia, *import duty*, lakini hao watengenezaji wa mafuta hapa nchini tunawasaidiaje, maana huwezi kuleta mafuta yanayotoka nje halafu unayondolea ushuru wa 10% halafu huyu mtangenezaji anayetengeneza kwa kutumia mbegu zako za nchini anawasaidia wakulima wako yeye unamuwekea VAT, maana yake nini? Hakuna usawa, kwa hiyo, lazima mambo haya tuyatengeneze kwa usawa. Unaondoa ushuru kwa yale yanayotoka nje, kwanza, tuhakikishie kama kweli ni mafuta ghafi yale. Kuna fununu kwamba yale mafuta yanayotoka nje si ghafi. Kwa hiyo, hapo muweke wapimaji wazuri, waone na wajihakikishie kwamba yale mafuta ni ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mining Act* imechelewa. Mheshimiwa Jaji Bomani, amemaliza kazi yake vizuri sana na ametoa mapendekezo mazuri sana. Leo hii kama tungekuwa tuna sheria mpya ya madini, matatizo haya ya kuwa na upungufu wa kodi yasingekuwepo kwa kiasi hiki ambacho tunayaona. Eneo la kupatia kodi ni la madini, lakini mpaka leo tunasema bado tunaangalia rasimu ya sheria; rasimu ya sheria mpaka lini? Hivi hii sheria ina ugumu gani?

Mheshimiwa Mntangi, katoka kueleza sasa hivi hapa kwamba, hata yale tunayotaka kubadilisha tunasema wengine tutazungumza nao, alah! sasa tunabadilisha nini? Tukienda kuzungumza nao watasema hapana kwa sababu ulisaini *on the doted line* kwamba, unakubali hayo ndiyo masharti ya mimi kuja kama mwekezaji, akikataa ana haki. Kwa hiyo, hapa na sisi tuseme tu kwamba, tumebadili mtazamo, sheria zetu mpya ni hizi, wewe ulikuwepo basi tuendelee halafu tuone hataki aondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mfupi mambo ni marefu, lakini nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia. Ahsante sana. *(Makofi*)

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hii. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji, kwa kuandaa Bajeti hii. Bajeti hii ni nzuri ila ina baadhi ya maeneo ya kurekebishwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Bajeti hii ni nzuri kwa sababu imeendelea kubainisha elimu kama kipaumbele cha kwanza cha Taifa hili, ndiyo maana ikaipangia shilingi trilioni 1.7. Sote tunatambua kwamba, elimu pekee ndio itakayoweza kutuvusha kutokana na dimbwi hili la umasikini. Pili, vipaumbele vya taifa ambavyo ni sita, vimepangiwa bajeti kubwa. Kwa hiyo, hiyo inaonesha *seriousness* ya Serikali kwamba, kweli imevitambua hivi kama vipaumbele vyake na kuvipangia bajeti asilimia 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Bajeti hii ni nzuri kwa sababu imezingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na imesema kwamba, itaanzisha Benki ya Wakulima, kitu ambacho tulikuwa tunakitafuta. Kitu cha pili, Waziri

amesikia kilio cha Wabunge wengi, pamoja na Wastaafu; kwa mara ya kwanza wameamua kwamba, sasa kima cha chini cha pensheni kitapanda. Mnakumbuka wengine walikuwa wanapata shilingi 21,000, lakini nasema ni nzuri kwa sababu Bajeti hii haitawaongezea Wafanyakazi kodi, kwa hiyo inawajali Wafanyakazi. (*makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Bajeti hii ni nzuri kwa sababu sote tuna matatizo, tunaona wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanagoma kila siku, lakini kwa sababu sasa Serikal imeamua kurejesha Mafunzo ya JKT, nina uhakika kwamba, vijana wetu watajifunza na wataacha migomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nafikiria kwamba, hii Bajeti ni nzuri kwa sababu itaboresha kilimo na tunapozungumzia kuboresha kilimo ina maana tuna-*target* zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania. Kwa hiyo, pamoja na mambo hayo mazuri, kuna mambo kadhaa ya kurekebisha.

Naanza na Miundombinu, Serikali iliwaahidi Watanzania ambao ni Wakazi wa Mkoa wa Kagera kwamba, itawajengea Uwanja wa Ndege kwa kiwango cha lami ngumu. Mwaka jana zilitolewa hela kidogo tu, mwaka huu kwenye *Vote* 98, kipengele cha 4687, pale kuna Uwanja wa Ndege wa Mpanda na Uwanja wa Ndege wa Bukoba, yote imeunganishwa kwenye kipengele kimoja na imekasimiwa shilingi bilioni 4.56. Sasa mimi ningependa kujua, kati ya hizo ni ngapi za Bukoba na kwa nini Serikali isitenge hela za kutosha kusudi ule Uwanja uweze kukamilishwa, watu waondokane na adha na uweze kuchochea maendeleo katika Mkoa wa Kagera? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya ndani ambayo imeelezwa kwamba ni asilimia 0.4; katika Mkutano wa 15, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alisema, madeni ya wazabuni waliotoa huduma ya vyakula katika mashule mwaka 2007 mwishoni na mwaka 2008 toka mwezi wa Tatu mpaka Desemba, Wizara ilikwishayahakiki na yangelipwa katika muda wa wiki mbili, lakini hadi leo hayajalipwa. Muda umekuwa mrefu, hawa wazabuni wamefilisiwa na serikali. Nilipouliza walisema haya madeni yote sasa hivi yamehama, yamehamishiwa Hazina. Ninapenda kujua, hawa Watanzania ambao wameshateseka kwa zaidi ya miaka miwili, wametoa huduma kwa serikali; ni lini watalipwa madeni yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada ya kodi Tanzania imefikia asilimia 30 ya mapato yote yatokanayo na kodi, yaani asilimia 3.5 ya Pato la Taifa, wakati Kenya ni asilimia moja tu na Uganda ni asilimia 0.4, sisi ndio maskini zaidi lakini ndio tunaotoa misamaha zaidi. Ningeomba hii misamaha mikubwa itazamwe upya, lakini upande wa kutazama ni wa madini, kule ndiko kuna misamaha mikubwa ambayo imesamehewa, ambayo inaweza ikaliletea taifa letu pato kubwa.

Ndugu zangu upande wa Mashirika ya Dini, pamoja na *NGOs*, haitakuwa sawa. Nasema hivyo kwa sababu, kwa miaka mingi, madhehebu yalikuwa yanajishughulisha katika kujenga shule. Nyote mnakumbuka, kwa mfano, kwa Mkoa wa Kagera, shule kama Rugambwa, Ihungo na Kahoro, zilijengwa na Madhehebu ya Dini.

Hospitali zimeendelea kuendeshwa vizuri na kwa gharama nafuu na Mashirika ya Dini, hawa hawana miradi mikubwa wana miradi midogo midogo na uwezo wanaoupata huko ndio unaendesha vituo vya watoto yatima, mashule, hospitali na huduma zote hizo mnazoziita za kiroho.

Vilevile hawa wanaendesha hizi shughuli kwa kutumia misaada kutoka nje, sasa tukiwatoza kodi ina maana nani atalipa sasa; aliyetoa msaada au anayeupokea?

Ukienda hadi leo huduma nzuri za kiafya zinatolewa katika Taasisi za Kidini. Sisi kwetu kule Kagera, utasikia mtu anakwenda Kashozi Hospital, Mugana, Kagondo, Rubya, Ndorage, kule ndiyo utapata *good nursing care.* Watu wanakujali, upendo na hata siku moja Daktari hawezi kukuandikia dawa ukaenda kwenye dirisha usiikute.

Sasa ninachoomba ni kwamba, wasikatishwe tamaa, haikuniingia akilini nikasema Serikali kama Serikali ya Tanzania inayojali; hivi kweli inaweza kuwaondolea misamaha hawa watu ambao wameshirikiana nao kwa miaka yote hii kutoa huduma?

Sasa nimechanganyikiwa, nimekwenda kusoma Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura ya 148, nikasoma na Sheria ya Mapato, Sura ya 332, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashirika ndani ya ile Sheria ya VAT, sasa ukisoma pamoja na yale majedwali, naona hii misamaha bado ipo palepale haijaondolewa.

Tatizo ninaloliona ni kwamba, Waziri ameshindwa kutueleza; yeye ndiye ametuchanganya mpaka watu wamepandisha jazba. Tunaomba atueleze vizuri; misaada gani hii aliyosema imefutwa kwa sababu mimi nikisoma kwa uelewa wangu naona kama yote bado ipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misukosuko na kuporomoka kwa uchumi; labda kabla sijalisema hilo, nilichotaka kuongezea pale mwisho ni kwamba, sote tunatambua kwamba, tumekuwa tukifanya kazi vizuri na Mashirika ya Dini na NGOs, hatuwezi kuwageuka sasa hivi, sana sana tunachopaswa kufanya ni kuwamotisha, ikiwezekana tuwape na ruzuku ili waendelee kushirikiana na Serikali kutoa huduma nzuri zaidi.

Misukosuko ya kuporomoka kwa uchumi; Wakulima wa Kahawa katika Mkoa wa Kagera, huwa wanauza kahawa yao kwa kutumia Vyama Vikuu vya Ushirika ambavyo ni *Kagera Cooperative Union (KCU)* na *Karagwe District Cooperative Union (KDCU),* lakini vyama hivi vilikopa mikopo benki vikanunua kahawa, walipokwenda kuuza kwenye Soka la Dunia, bei ikawa imeporomoka wakauza kwa hasara.

Matokeo yake ni kwamba, hadi leo *KCU* ina mkopo wa benki usiopungua shilingi bilioni 1.6 na hasa kwa sababu waliuza kwa hasara, wana hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 1.4. *KDCU* wana mikopo ya benki ambayo hailipiki na inaendelea kuongezeka ya shilingi bilioni 2.9 na hasara ya shilingi bilioni 2.2, hizo hapo tunazungumzia hali ngumu ya karibu shilingi bilioni 7 ambayo imevikumba vyama hivi vya ushirika.

Pili, kuna Kiwanda cha BUCOP, ambacho ndio kinachokoboa kahawa ya KCU nacho kimekumbwa na msukosuko huo, kwa sababu wao walikopa mkopo kutoka benki, wakaboresha mashine zao na kununua mitambo ili waweze kukoboa kahawa zilizotoka KCU kwa makubaliano kwamba, KCU ingewalipa kwa kila kilo waliyokoboa.

KCU imepata hasara, wameshindwa kuwalipa BUCOP na BUCOP wameshindwa kulipa benki, kwa hiyo, mpaka sasa hivi wanadaiwa sio chini ya milioni 525, ambazo zinazidi kuongezeka kwa sababu riba inazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde, ili Vyama vya KCU na KDCU ambavyo ni mfano uliobaki kama mfano wa Vyama vya Ushirika ndani ya Tanzania, ninaomba visife, vinusuruni kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais.

Naomba madeni yote ya mabenki yalipwe. Niliposoma kwenye Hotuba ya Bajeti, nimeona kwamba, hizo pesa zinapitia benki kwa maana hiyo ni kwamba, zitalipwa kama mikopo kutoka benki.

Naomba na ile hasara waliyoipata wailipe kwa sababu wameshindwa sasa kupata hela za uendeshaji wa vyama vya ushirika, wameshindwa kulipa malipo ya pili ambayo wanalipa kwa wakulima na wameshindwa kulipa ushuru wa mazao ambao wanalipa kwenye Halmashauri husika.

Kama kuna watu waliopata hasara na kuathirika na kuporomoka huku kwa uchumi ni hawa wakulima kwa sababu bei ya kahawa imeporomoka kutoka shilingi 700 hadi 350 au kahawa safi kutoka shilingi 1600 hadi 750.

Kwa bei hii, Mkulima hata gharama zake alizotumia ameshindwa kuzirudisha, kwa hiyo, wamepata hasara kubwa na wanaendelea kuwa maskini.

Nilikuwa naiuliza serikali; je, inasemaje kuhusu huyu mkulima mmoja mmoja ambaye amepata hasara kiasi hiki?

Je, isingekuwa busara na Serikali ikakubaliana na mimi kwamba, sasa na hawa wakulima mmoja mmoja warejeshewe au wapewe hela kiasi fulani kwa kila kilo waliyouza kwa hasara ili na wao waweze kufaidika na mfumo huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nasema Bajeti ni nzuri kama hayo marekebisho yatafanywa na naomba nipate majibu kwa hayo maswali niliyoyauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tutakubaliana kwamba, kiwango cha majadiliano katika Bunge hili kiko juu sana, nawapongeza Wabunge wote ambao wamechangia kwa siku ya leo. Mjadala utaendelea kesho ambapo tutaanza na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatia Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa William Kusila na wengine. Baada ya hapo, nina tangazo moja tu kwa Wabunge wote

wa CCM kuwa, leo hakutakuwa na Kikao cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM, kimeahirishwa hadi mtakapotaarifiwa hapo baadae.

Kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwenye *Order Paper* ya leo zimekwisha, basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 07.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 16 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*